ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani
12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais.
13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
17.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/\Jimbo la Jang'ombe
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni

19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni
23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
32.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais

37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
56.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
57.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
58.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
59.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
60.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
61.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
62.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
66.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
67.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
68.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
69.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
71.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
72.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Kumi na Tatu - Tarehe 3 Juni, 2014

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika (Ali Abdalla Ali) alisoma dua

Maswali na Majibu

Nam. 49

Fidia kwa Walioharibiwa Vipando vyao Vitongoji

Mhe. Jaku Hashim Ayoub (Kny. Mhe. Saleh Nassor Juma) - Aliuliza:-

Kwa kuwa lengo la Serikali yoyote iliyopo madarakani ni kuondoa kero za wananchi katika kipindi chake husika cha uongozi. Kwa kuwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa ya Zanzibar ipo ukingoni kumalizia kipindi chake cha miaka mitano.

Na kwa kuwa wananchi wa Jimbo la Wawi hadi leo hii bado wana kero kubwa ya kutolipwa fidia ya mali zao katika eneo la Vitongoji baada ya vipando vyao kukatwa, pale ulipopelekwa umeme katika maeneo ya Kwareni, Makaani, pamoja na kutomaliziwa malipo yao kutokana na mazao yao kuathiriwa katika ujenzi wa Chuo cha Mafunzo ya Amali Vitongoji.

Na kwa kuwa Waziri husika wa Miundombinu na Mawasiliano ametoa ahadi kadhaa ambazo hadi leo hii ameshindwa kuzitekeleza.

Je, ni lini Serikali itatekeleza wajibu wake kwa kuwalipa fidia wale wote walioathirika kwa kukatiwa mazao yao kwa kupisha upelekaji umeme Kwareni, Makaani, Vitongoji sambamba na kuwamalizia fidia zao wale waliokatiwa na kuathiriwa mashamba yao katika ujenzi wa Chuo cha Mafunzo ya Amali Vitongoji.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 49 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye mfumo wa Umoja wa Kitaifa kwa kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010 - 2015 ina lengo la kuwapatia wananchi wake maendeleo ikiwa ni pamoja na kuwapelekea huduma mbali mbali za jamii kama vile afya, elimu, umeme, barabara na kadhalika katika maeneo yao.

Mhe. Naibu Spika, Serikali ikiwa inatekeleza malengo hayo wakati mwengine inatulazimu kuvunja majengo au kukata miti na vipando vyengine vya wananchi ili huduma inayokusudiwa iweze kuwafikia pale walipo na waweze kufaidika nayo. Kawaida Serikali huwa inawajulisha wananchi ili kuweza kuwatambua watakaoathirika na kutia thamani mali zao na baadae huwa wanalipwa kwa mujibu wa tathmini iliyofanywa na Serikali.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba kuna wananchi wa Vitongoji walioathirika kwa kukatiwa mazao yao kwa kupisha upelekaji umeme Kwareni, Makaani na Vitongoji. Serikali imefanya tathmini kwa wale wote walioathirika na ina nia nzuri ya kuwalipa wananchi wote waliotambuliwa na kutathminiwa mali zao.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa Wizara husika imo katika maandalizi ya kuwalipa walioathirika.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa fidia ya wananchi walioathirika kutokana na ujenzi wa Chuo cha Mafunzo ya Amali Vitongoji, Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imefanya tathmini ya mali iliyokuwemo kwenye eneo hilo na tayari wameshaanza kulipa fidia kwa baadhi ya wahusika na itaendelea kufanya malipo kwa wale wote waliotambuliwa kadri ya fedha zitakapopatikana.

Mhe. Naibu Spika, awali lilijitokeza tatizo la utiaji thamani kubwa sana isiyolingana na uhalisia wa mali husika. Serikali ilipitia tena na kutathmini upya thamani halisi za mali hizo na sasa kazi imekamilika na zoezi linaendelea vizuri na malipo hayo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Serikali yoyote duniani inaendesha mambo yake kwa mpango. Kwa nini suala la kulipwa fidia lifanyike zito wakati hili jambo lilihitaji kufanyika mwanzo kabla ya utekelezaji wa mradi. Hii ni sawasawa na ujenzi wa Uwanja wa Ndege. Kipi kinachokuja mwanzo kati ya ramani na ujenzi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, ningependa arudie lile la pili sikulisikia vizuri.

Mhe. Naibu Spika: Lile la pili usijibu maana halihusiki na swali mama. Jibu la kwanza.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, ni kweli upo umuhimu wa kufanya tathmini kwanza na kulipa fidia kwanza kabla ya utekelezaji kuanza. Lakini kutokana na hali halisi ya uwezo wetu wa kiuchumi wakati mwengine mahitaji ya wananchi wa sehemu husika ndio hutubidi kufanya ile shughuli iliyokusudiwa na baadae kulipa fidia. Lakini ushauri alioutoa Mhe. Mwakilishi mzuri tutaufanyia kazi ili matokeo kama haya yasitokee kwa mara nyengine.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri katika majibu yake amesema kuwa makisio yaliyofanywa mwanzo yalionekana ni makubwa kama nimemsikia vizuri, badala yake Serikali ikafanya makisio mengine halisi kutokana na mali iliyoathirika. Ambapo suala kama hili lilitokea katika eneo la Bungi ulipojengwa mnara makisio aliyofanya Afisa wa Kilimo wa Wilaya kule badala yake yalionekana ni makubwa Wizara ya Habari ikafanya makisio mengine madogo. Mimi swali langu lipo hivi; inakuwaje makisio yanafanywa na mtaalam na ni kwa Serikali tu yakaonekana makubwa halafu watu wakalipwa mali yao chini ya bei.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa nadhani kabla hajajibu Mhe. Waziri nikusaidie. Mhe. Waziri hakusema kwamba makisio yalikuwa makubwa yanafanyiwa masahihisho. Kasema fedha hazijapatikana umefanywa kwanza mradi halafu baadae ndio wanalipwa. Sasa kama na yeye anaweza kulijibu namruhusu Mhe. Waziri ajibu.

UTARATIBU

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, mimi ni binadamu kama sivyo nilivyosema naomba Mhe. Waziri akanushe halafu ndio maelekezo yake yafuate.

Mhe. Naibu Spika: Unasemaje. Wewe ulisema Mhe. Waziri kasema kwamba makisio yalikuwa madogo yanarekebishwa tena, hakusema hivyo. Kasema Serikali haina uwezo kwanza wamefanya mradi halafu wanalipa kidogo kidogo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Naibu Spika, ni kweli wakati mwengine kama binadamu, na hata wataalam huwa binadamu hufanya makosa katika kufanya tathmini. Na pale inapoonekana kwamba makosa yametokea ndio Serikali huamuru kufanya tena tathmini ili thamani halisi ipatikane. Na inapatikana thamani halisi ya pesa za umma ndio malipo hufanyika.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kabla ya kuuliza swali langu naomba niipongeze sana Serikali ya Mapinduzi kwa kuleta maendeleo ya wananchi.

Mhe. Naibu Spika, barabara ya Kinyasini/Dunga tangu kujengwa kwake inafika miaka 7 hadi 10 hivi sasa. Tatizo lililojitokeza wananchi wa Kinyasini hadi hivi sasa hawajalipwa fidia zao, lakini maeneo mengine yote ya huko ambako barabara hii imepita tayari wameshalipwa.
Je, ni lini Mhe. Waziri wananchi wangu wa maeneo haya watalipwa fidia yao.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe swali lilikuwa linahusu Vitongoji na Wawi Pemba. Kama Mhe. Waziri anaweza kujibu na ajibu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, hata hili spika ilikuwa halitaki kujibu kwa sababu ilichelewa kuwaka taa hapa kuonesha kwamba swali hili linamhitaji Wizara husika. Naamini Wizara husika imesikia na wataleta majibu yao kwa maandishi ili kuwaambia lini malipo yao yatafanyika.

Nam. 28

Kero ya Wingi wa Matuta katika Barabara ya Mazizini Kituo cha Polisi kuelekea Baraza la Wawakilishi

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Barabara inayotokea Kituo cha Polisi cha Mazizini kuelekea Baraza la Wawakilishi imewekwa matuta mengi kiasi ya kuleta udhia kwa wananchi na vyombo vyao wanaotumia barabara hiyo, wakiwemo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

(a) Je, kigezo gani kilichotumika kuweka matuta mengi kwenye barabara hiyo ambayo haina shughuli nyingi badala ya matuta hayo kuwekwa maeneo ambayo yana skuli na vyuo.
(b) Ni lini matuta hayo yatapunguzwa ili kuondoa udhia kwa madereva na vyombo vyao.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 28 lenye vifungu (a) na (b). Lakini kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mhe. Naibu Spika, barabara ni miundombinu na muhimu sana kwa maendeleo ya jamii na taifa kwa jumla. Lengo la kujengwa kwa barabara ni kurahisisha usafiri na usafirishaji wa bidhaa kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyengine. Kwa kuwa barabara hutumiwa na vyombo vya moto, waendao kwa miguu na kwamba huwa kuna maeneo yenye msongamano wa watu ambao hukatisha barabara kutoka upande mmoja kwenda upande wa pili. Suala la usalama kwa watumiaji wa barabara hiyo huwa ni la umuhimu sana na ndio maana huwekwa alama tofauti za barabarani yakiwemo matuta. Japokuwa suala la uwekaji wa matuta barabarani si muafaka sana lakini hulazimu kutokana na madereva kutokufuata sheria za barabarani pamoja na baadhi ya watu kuharibu kwa makusudi alama husika za kuongozea safari za barabarani.

Baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, uendeshaji wa kasi wa magari na vyombo vyengine vya moto usiozingatia usalama wa watu wengine watumiao barabara hiyo, watu wengine huomba kuwekewa matuta baada ya kujitokeza ajali za mara kwa mara za kugongwa watu na kwa kuzingatia kuwa barabara hiyo sio barabara kuu ndio inayosababisha kuwekwa kwa matuta hayo.
(b) Mhe. Naibu Spika, suala la udhia wa madereva wa magari yao na vyombo vya moto halina uzito ukilinganisha na uhai wa wanadamu. Hivyo kwa sasa matuta hayo ambayo tayari yameshafanyiwa marekebisho ambapo awali yalikuwa ni ya rasta yataendelea kuwepo kwenye maeneo hayo kwa ajili ya usalama wa watu wa maeneo hayo na watumiao barabara hizo hadi pale njia mbadala ya usalama watumiao barabara itakapopatikana.
Aidha, nachukua nafasi hii kuwaomba madereva kufuata taratibu za usalama barabarani na kwa wananchi kutoharibu samani za barabara kwa makusudi ambazo zimewekwa kwa ajili ya usalama wao.

Kwa hivi sasa cha msingi tunaendelea kuweka alama maalum za kuonesha uwepo wa matuta hayo na alama za kuongozea usalama barabarani.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Nchi gani duniani inayotumia utaratibu kama wetu wa kujenga barabara nzuri na baadae kuweka matuta na kutokujali sheria za usalama barabarani.

La pili, wananchi wa Jimbo la Muyuni wamekuwa wanatumia kwa muda mrefu hasa Skuli ya Kitogani na Skuli ya Muyuni baada ya kupoteza maisha ya wanafunzi. Kwa nini wengine wakawekewa matuta na wengine wasiwekewe matuta. Mfano hai pale pale Jimbo la Muyuni, kimapunju wa Jozani walikuwa na thamani zaidi kuliko wananchi wa Jimbo la Muyuni. Je, Serikali inatoa kauli gani.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe swali mama lilikuwa linahusu njia ya Chukwani. Sasa njia ya Muyuni na huku kwengine kama una uwezo jibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, nchi zote duniani jambo la msingi ni kuona kwamba taratibu husika za barabara na Sheria za Kimataifa zinazingatiwa. Zanzibar ni sehemu ya ulimwengu tunalazimika kufuata taratibu husika zikiwemo alama za barabarani, michoro, usimamizi wa sheria na taratibu zote za kimataifa.

Lakini kama alivyoeleza Mhe. Mwakilishi kwamba Zanzibar tumekuwa tuna desturi ambapo madereva wetu wengi sijui kwa sababu gani za msingi tumekuwa hatuheshimu taratibu na maelekezo pamoja na alama za usalama barabarani. Kama tungekuwa madereva wetu wanaheshimu taratibu hizo na alama za barabarani uwekaji wa matuta usingefanyika. Tumeeleza kwamba uwekaji wa matuta hatuna jinsi, yangehamishwa tu lakini kwamba usalama wa watumiaji wa barabara uwepo ndio maana tunalazimika kuweka matuta. Kama madereva wetu, kama wasimamizi wa sheria watasimamia vizuri majukumu yao uwekaji wa matuta hautokuwepo.

La pili, anaulizia suala la uwekaji wa matuta katika Skuli ya Muyuni na Skuli ya Kitogani na mfano wake ametolea suala la kimapunju. Mimi nimuombe tu Mhe. Mwakilishi watu wa kwetu Bwejuu asiwafananishe na kimapunju. Watu wa Bwejuu wana akili, wanaelewa, wanatambua wajibu wao, wanajua kuvuka barabara, wanajua taratibu za sheria za usalama barabarani. Uwekaji wa matuta katika kimapunju ni mahitaji maalum kwamba wale ni wanyama, na ni wanyama ambao Serikali inalazimika kuwalinda kama kitega uchumi lakini pia katika namna ya kuona kuhifadhi haki za wanyama.

Kwa hiyo uwekaji wa matuta katika Skuli ya Kitogani tutalizingatia kwa kuanza kuweka alama kabla ya kuweka matuta kutoa zile alama pamoja na michoro. Tukiona kwamba alama hizi hazijafanya kazi tutafikia hatua ya uwekaji wa matuta. Lakini utaratibu wa kuweka matuta upo wazi unaanzwa na maombi, Bodi husika inamshauri Mhe. Waziri. Tukiona kwamba kuna haja na ulazima wa kufanya hivyo tutaweka matuta.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Natumia kanuni ukurasa wa 44 kifungu cha 8 ni marufuku kwa Mjumbe yeyote kutumia lugha ya matusi au kashfa. Amewakashifu wananchi wangu wa Bwejuu. Mhe. Naibu Waziri aombe radhi. Huwezi kuwafananisha na kimapunju wale watu.

Mhe. Naibu Spika: Amewakashifu vipi mbona sikuelewi.
Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Anasema wale watu ni kimapunju hawana akili watengenezewe matuta nilivyomfahamu mimi Mhe. Naibu Waziri alipotoa kauli hiyo.

Mhe. Naibu Spika: Mimi nilivyomfahamu Mhe. Waziri kasema hivi kwamba kimapunju wamejengewa matuta kwa sababu hawana akili kama binadamu. Lakini huko kwako ataanza kuweka alama kwanza watu wasipozifuata wataweka matuta. Mimi ndivyo nilivyofahamu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Sawa Mhe. Naibu Spika, kama ni hivyo nimuombe radhi mimi sasa, ndio uungwana kuomba radhi Mhe. Naibu Spika.

Swali langu la msingi hakulijibu nilimuuliza ni nchi aliyotembea duniani akaona utaratibu kama huu, anitajie kama Marekani, Afrika Kusini.

Mhe. Naibu Spika: Na hilo amejibu hukusikia lakini ongeza tena Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, namthibitishia Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwamba samahani yake nimeipokea kwa moyo mkunjufu.

Tumeeleza kwamba Zanzibar ni sehemu ya ulimwengu tunalazimika kufuata taratibu za msingi za usalama barabarani hatuna ulazima wa kutaja nchi. Sisi kama sehemu ya ulimwengu tunalazimika kufuata taratibu husika za kiulimwengu zenye kuhusiana na usalama wa barabarani, alama, michoro na maelekezo.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mahiri sana yenye ufanisi na upeo mkubwa wa taaluma ya hii ya Sekta ya Mawasiliano.

Naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza lenye a, b, c na d kama ifuatavyo.

Kwanza kabisa Mhe. Naibu Spika, anachukua hatua gani Mhe.Naibu Waziri...

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa swali (a) na (b) basi (c) na (d) uache.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kumuuliza (a) na (b).

(a) Barabara zote za mji wa Zanzibar tunavyofahamu zina majina yake na barabara hii iliyouliziwa swali hapa imeandikwa barabara inayotokea kituo cha Polisi cha Mazizini kuelekea Baraza la Wawakilishi, ina jina lake. Jina lake ni *Bakari Jabu's Road* katika kuwaenzi wazee wetu waliotukomboa katika nchi yetu.

Sasa Mhe. Naibu Waziri kwa nini haya majina hayatumiki wakati wa kujibu maswali na pia barabarani hakuna alama yoyote ya kuweka majina haya ambapo barabara zote hizi zimepewa majina hayo. Huhisi kama hatufanyi hivi tutapoteza majina ya barabara hizo.

(b) Mhe. Naibu Waziri kuna hizi alama ambazo zinaekwa kwa viwango katika haya matuta. Matuta haya yaliyokuwemo katika barabara hii ya *Bakari Jabu's Road* au *Mhe. Bakari Jabu's Road*. Je, matuta haya yapo katika kiwango na pili muna utaratibu gani wa kuyatia rangi na tatu alama zile za pembeni kuonesha kwamba matuta hayo unayakaribia.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa majibu, japo yale uliyoyakataa umeongeza yote umemaliza.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundumbinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi maswali yake ya (a) na (b) ya nyongeza kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba barabara zetu nyingi ziliopo Zanzibar zimekuwa hazina *sign*. Kwa maana kwamba ya zile alama zinazoainisha majina halisi ya barabara hizo. Lakini kwa upande wetu sisi serikali tumekuwa na desturi ya kuweka. Bahati mbaya wananchi wetu ninadhani hawazifahamu umuhimu wake, wamekuwa wakiziondosha kwa makusudi.

Hivyo malengo makubwa yaliyopelekea Mhe. Mwakilishi kuuliza swali pasi na kutaja jina lake, ninadhani kwa sababu kwamba alikuwa haifahamu lakini sisi kama serikali tunaona umuhimu huo, tutaendelea kuyaweka, tutaendelea kuwaelimisha wananchi wetu. Kwanza wafahamu umuhimu wa kuitambua barabara kwa jina lake lakini la pili umuhimu wa kuiacha ile alama ili mwengine ambaye hafahamu lile jina aweze kufahamu na yeye aweze kutambua barabara hiyo inaitajwe kama alama yake husika.

(b) Suala la pili amezungumzia suala la matuta. Ni kweli kwamba matuta haya yameekwa kwa viwango na kabla ya matuta haya yalikuwepo matuta mengine ambayo wataalamu wanaita *matuta rasta*, yale ambayo ukipita yanakuwa kama mifilimbi mifilimbi, kama minne mpaka mitano. Yale tumefuta tumeeka haya na matuta haya tulipoweka tuliweka na rangi, sasa hivi rangi imetoweka.

Kwa hivyo sisi wajibu wetu tutayarejeshea rangi, tutaweka na *sign* zile za pembeni ambazo ijapokuwa wananchi wamekuwa na desturi ya kuzing'oa. Kwa hivyo tutarejeshea tena, rangi na tutaweka na zile *sign* pembeni ili ziweze kumuongoza mtumiaji aweze kutambua kwamba urefu fulani mbele kuna tuta na rangi iweze ku-*reflect* wakati wa usiku ili anapoendesha gari lake aendeshe vizuri kwa kuwa na tahadhari zote za usalama wa barabarani.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, mbali na kadhia hii ya barabara ya *Bakari Jabu's Road* lakini kuna kadhia ya barabara la Wawakilishi kuelekea *airport* ambapo kuna sehemu huwa wakati wa mvua kunatwama maji na huwa inawapa mashaka na taabu sana kwa wananchi wanaopita magari yao na vile vile na wananchi ambao wanaoishi jirani.

Je, wizara ina mpango gani wa kuifanyia miundombinu eneo hilo ambalo lipo mbele ya Baraza la Wawakilishi kuondoa kadhia hiyo ya kutwama kwa maji.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, eneo ambalo analolizungumza Mhe. Mwakilishi ni kama mita 30 ama 40 ukitoka mlango mkuu wa Baraza la Wawakilishi. Lakini sote ninadhani ni mashahidi kuona wembamba wa barabara ambayo inazungumziwa.

La pili utaona namna majengo kwa maana ya kwamba nyumba zilivyoifinya hiyo barabara. Sasa sisi kama wizara wajibu wetu kujenga barabara iliyokuwa katika kiwango kizuri. Suala la kutwama kwa maji tunahitaji kutengeneza mtaro. Lakini unapozungumzia kutengeneza mtaro eneo lile, maana yake unazungumzia kuvunja nyumba za watu, suala ambalo kwenye serikali fedha hatuna mpango huo. Sisi wajibu wetu kuona tu maji yale tunayatafutia utaratibu wa kuweza kuondoka barabarani, yakiingia kwenye nyumba ya mtu, yeye atakuwa suala lake la kujenga katika maeneo ambayo ni hifadhi ya barabara.

Sisi kama wajibu wetu tunaona kwamba kuna eneo ambalo limejifinya sana na maji yanatwama na maji yale hayana pa kwenda. Hivyo aidha maji yale yabaki pale ama yaingie nyumbani kwa mtu.

Nam. 2

Kuanzishwa Shahada za Sayansi ya Siasa na Uhusiano wa Kimataifa Chuo cha *SUZA*

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

SUZA ni chuo pekee cha serikali kinachotoa mafunzo ya shahada *(First Degree)* hapa nchini na kwa kuwa Zanzibar inakuwa na uchache wa wataalamu katika fani ya Diplomasia na Mahusiano ya Kimataifa pamoja na sayansi ya siasa.

Je, ni lini chuo chetu cha *SUZA* kitaanza kutoa taaluma ya mafunzo ya sayansi ya siasa na mashirikiano ya kimataifa *(Political Science and Internationa Relations).*

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 2 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) pamoja na Chuo cha Uongozi wa Fedha ni taasisi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zinatoa mafunzo katika ngazi ya shahada. Taasisi hizo zina wajibu mkubwa wa kutoa mafunzo wa fani mbali mbali kulingana na mahitaji ya maendeleo ya nchi kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Pamoja na kuwa mahitaji ya mafunzo ni mengi lakini taasisi zetu zinatoa mafunzo kulingana na vipa umbele vya maendeleo ya nchi. Kwa hivi sasa vipaumbele vya elimu ya juu ni katika fani za ualimu hasa wa sayansi, ufundi, udaktari, uchumi, utalii na uchimbaji wa mafuta na gesi.

Ninakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa nchi yetu ina uchache wa wataalamu katika fani ya Diplomasia na Mahusiano ya Kimataifa pamoja na Sayansi na Siasa.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-
Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar hakina mpango kwa sasa kuanzisha mafunzo ya shahada katika fani ya Diplomasia na Mahusiano ya Kimataifa kutokana na kutokuwa na wataalamu wa kutosha wa maeneo ya kufundishia wa fani hizo na kutokuwa na kutokana na kuwa kwa sasa si kipa umbele cha Zanzibar, pia mafunzo kama hayo

yanatolewa katika vyuo vyengine viliomo nchini kama vile Chuo cha Utumishi wa Umma (*IPA*) na Chuo cha Diplomasia ya Uongozi Dar es Salaam.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri sana aliyotoa Mhe. Naibu Waziri, naomba niulize swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Zanzibar ni nchi na kwa kuwa hivi sasa tumo katika suala zima la mkakati wa Katiba na kwa kuwa wakati wowote Zanzibar inaweza ikawa na Wizara yake ya Mambo ya Nje au ikawa na mambo ya *International Relations* ikawa na upande wake.

Je, hamuoni sasa serikali ni muhimu kuona kwamba haya mambo ya *International Relations* yanapewa kipaumbe na kuweza kukinasihi sasa chuo chetu cha *SUZA* kwa kuwapatia wataalamu katika fani hii ya *International Relations and Conflict Revolutions*.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri majibu ya kumuongeza majibu maana yale ulikuwa umeshajibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.:-

Mhe. Naibu Spika, kwanza ninakubaliana naye kama Zanzibar ni nchi lakini pia afahamu kama mambo ya mahusiano ya kimataifa mpaka hivi sasa ni mambo ambayo yanahusu Serikali ya Muungano. Umuhimu wa kuwafundisha wanafunzi wetu wa Zanzibar, umuhimu huo upo na ndio maana nikamwambia kama tuna Chuo cha Utumishi wa Umma ambapo kipo hapa Zanzibar.

Vile vile kwa wale wanafunzi wetu ambao wanachukua digrii hichi cha Diplomasia cha Dar es Salaam na wakimaliza hapo, wakitaka kwenda usoni Mhe. Naibu Spika, sisi huwa tunawapa mikopo hawa, haidhuru sio kipa umbele cha nchi lakini tunajua kama wataalamu wa fani hii ni wachache. Kwa hivyo huwa tunawapa mikopo kwenda kuendelea.

Mhe. Naibu Spika: Kwa kumuongezea Mhe. Mwakilishi tawi la chuo hicho lipo katika jimbo langu pale Mfenesini, pana tawi pale kozi hiyo inasomeshwa vile vile, tawi la Mwalimu Nyerere. Mhe. Waziri anataka kutoa maelezo ya ziada.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kny: Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali): Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri ninapenda swali la nyongeza juu ya wanafunzi ambao wanasomeshwa sasa hivi.

Kabla ya miaka miwili nyuma wanafunzi 19 walipelekwa katika Chuo cha Diplomasia kwenye fani ya digrii ya sheria na sasa wameshapata *Post Graduate Internation Relations.* Hivyo serikali ina mpango mkubwa wa kuwaendeleza na kuwaweka katika mabalozi mbali mbali. (*Makofi*).

Mhe. Ali Salim Haji: Mhe. Naibu Spika, ahsante. Wakati Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu swali lake alizungumza suala la kipa umbele kwa maslahi ya nchi. Lakini tunaelewa kwamba sababu ya kuwekwa kipa umbele, sababu moja kubwa inatokana na masuala ya uwezo wa kifedha, ndio tukaangalia kipaumbele ili nchi kuwa na uwezo.

Sasa nilikuwa ninataka Mhe. Naibu Waziri anisaidie kidogo, kwa kuwa *SUZA* hivi sasa imeanzisha kigoda cha Sultan Qaboos cha kusaidia wanafunzi wa elimu ya juu. Nilitaka kujua ni wanafunzi wangapi wamefaidika na kigoda hichi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, nina uwezo wa kujibu mwenyewe. Ninajua Mhe. Mohammed kwa sababu yupo *SUZA* anayafahamu haya mambo lakini pia nina uwezo wa kumjibu, ninamuomba nitajibu tu.

Naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli tumeanzisha kigoda hiki na kwa kweli kinatusaidia sana kwa wanafunzi wa Zanzibar. Mpaka hivi sasa kwa taarifa ambayo ninayo kuna wanafunzi 7 ambao hawa wanachukua *First Degree* katika nchi mbali mbali lakini pia kuna walimu wetu ambao wapo *SUZA* na hawa pia wanafaidika na fani hii.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, baada ya majibu mazuri sana ya kitaalamu ya Mhe. Naibu Waziri naomba niulize swali moja lenye kifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Naibu Waziri amesema sababu ya msingi ambayo wameshashindwa kuanzisha shahada ya diplomasia na elimu ya sayansi ni kwa sababu kozi hizi zinasomeshwa baadhi ya vyuo Tanzania na nje ya nchi. Na sababu ya pili akasema kwamba ana sababu hawana wataalamu wa fani hizo.

(a) Ni kwa nini wameshindwa kuwatafuta wa kozi hizo wakati hivi karibuni wameanzisha shahada ya udaktari katika *SUZA*, wataalamu walipata wapi.
(b) Kwani kozi zinasomeshwa baadhi ya vyuo hazistahiki kusomeshwa hapa katika *SUZA* na kama hii ndio sababu msingi, kwa nini watu wanasomesha udaktari Chuo Kikuu Dar es Salaam na vyuo vyengine China na nyinyi mukaanzisha udaktari hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali la nyongeza lenye (a) na (b):-

Mhe. Naibu Spika, kama ambavyo nilijibu katika swali langu mama na ni kweli kanukuu kwa kusema kama nilisema sababu kubwa ni uchache wa walimu ambao watafundisha fani hii. Lakini vile vile nikazungumza kama fani hii inatolewa katika vyuo ambavyo vipo Dar es Salaam.

Mhe. Naibu Spika, nilizungumza pia ninadhani Mhe. Mwakilishi hakunifahamu kama fani hii inatolewa katika chuo ambacho kipo Zanzibar, Chuo cha Utumishi wa Umma wanatoa mpaka ngazi ya diploma. Wakimaliza ngazi ya diploma ndio wanaotaka kuendelea wanakwenda kuchukua fani hii kwenye Chuo cha Diplomasia cha Dar es Salaam.

Sasa sio kweli kama hatutoi fani hii hapa Zanzibar, tunatoa lakini kutokana na uchache wa walimu ambao tunao tunawafundishia wanafunzi wetu kwa diploma tu kwa hapa nchini.

Nam. 33

Ukosefu wa Daktari Bingwa wa Mifupa Hospitali ya Mnazi Mmoja

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Hospitali ya Mnazi Mmoja inaelekea kuwa Hospitali ya Rufaa lakini kwa muda mrefu sasa imekuwa haina mpango maalum wa kuweka daktari bingwa wa mifupa wakati wote. Wagonjwa wengi wa ajali wanaofikishwa Hospitalini hapo wanapata usumbufu wa kumtafuta daktari kwa mawasiliano ya simu na mara nyengine hapatikani.

(a) Wizara inachukua hatua gani ya kuhakikisha anakuwepo daktari wa mifupa kwa muda wote wa saa ishirini na nne *(24hrs).*
(b) Ni lini Wizara ya Afya itatekeleza majukumu yake kwa kuyafuatilia kwa kuhakikisha kuwa mgonjwa wa ajali anapofikishwa hospitali anapata huduma ya haraka bila ya kusubiri daktari.

Mhe. Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 33 kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, madaktari wa Hospitali ya Mnazi Mmoja ni wafanyakazi wenye kazi zaidi ya moja katika shughuli zao kwa kila siku. Kazi za daktari bingwa, kwanza anakuwa ni msimamizi mkuu wa idara yake, anakuwa daktari wa zamu katika idara yake kwa siku zote za kazi, anakuwa msimamizi wa madaktari wanaojifunza kazi kwa vitendo katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, anaendesha kliniki za wagonjwa wa nje kwa utaalamu wa maradhi anayosomea, wengi wao wanafanya kazi wodini, kliniki na kumalizia kazi zao katika chumba cha upasuaji, kushiriki

katika mikutano ya kitaifa na kimataifa kulingana na fani zao, kushiriki katika huduma zinazotolewa nje ya hospitali au kikazi Unguja na Pemba, pia ni mwalimu hutunga mitihani na msimamizi wa mitihani wa masomo anayoyafundisha katika Chuo cha Afya Mbweni na hatimaye watafundisha *SUZA*.

Mhe. Naibu Spika, ukizingatia wingi wa madaktari bingwa hao ni mmoja mmoja tu kwa kila idara na wanakuwa na mzigo mkubwa wa wagonjwa kuliko uwezo wao, ukiachilia mbali wingi wa wagonjwa wanaowahudumia ndani ya wodi, kliniki, wodi ya *VIP* kama kuna kiongozi na pia *Fast Track*.

Nao pia kama binadamu wana sehemu yao ya maisha, ni baba, ni mama, ni watoto wenye wazee wao na wanapaswa kuishi kama watu wengine na si kufanya kazi tu.

Mhe. Naibu Spika, Hospitali ya Mnazi Mmoja ina daktari bingwa wa mifupa mmoja tu ambaye haiwezekani kupangiwa *call* za masaa. Lakini isitoshe kwa kawaida kuna utaratibu wa kupangwa madaktari zamu katika madaraja. Kwa siku kuna daraja la kwanza *first on call* ambaye yeye anakuwepo kwa masaa 24, mara nyingi hawa ni wale madaktari wapya wanaojifunza kwa vitendo.

Daktari wa daraja la pili, *second on call* anaitwa na daktari wa daraja la kwanza kwa dharura na *third on call* na yeye ataitwa na daktari wa daraja la pili kwa kubwa ambalo yeye liko nje ya uwezo wake na mara nyingi kama kunaitajika *operation* ya dharura na kuokoa maisha. Kwa mantiki hiyo daktari bingwa anakuwa *on call* siku zote ila kwa kusubiri nyumbani. Anayepaswa kumpigia simu ya kumtafuta daktari bingwa ni daktari wa daraja la pili na sio kila mtu.

(a) Jukumu la kupanga zamu za madaktari katika mahospitali ni la uongozi wa hospitali zenyewe, wakishirikiana na uongozi wa idara za hospitali hizo na sio la wizara. Utaratibu wa kutumia daraja za madaktari hospitali kupanga zamu na ndio utaratibu wa mahospitali yote ulimwenguni ili kukabili uhaba wa wafanyakazi wenye ueledi huo.

(b) Katika juhudi za kuboresha huduma hizo Mnazi Mmoja Hospitali imeshaanzisha kitengo cha huduma za dharura kwa masaa 24, *emergence unit* ambapo kipo katika idara ya wagonjwa wa nje MMMMM.

Kitengo cha dharura kinachofanyakazi ya kutoa huduma zote za dharura, zikiwemo wagonjwa wa ajali wa aina zote. Huduma za dharura zinazohusisha ni kumsaidia mgonjwa kuweza kupumua, kuzuwia kumwagika kwa damu na kuwekewa damu na maji vinapopungua.

Ikiwa kuna mgonjwa anahitaji huduma za ziada baada ya kupatiwa huduma za dharura kama zile za mifupa au upasuaji mwengine, hiyo itakuwa ni huduma ya kupangwa ambayo tunaita *elective operation*, kwa sababu sasa hapo panahitajika maandalizi ya wafanyakazi mbali mbali, madawa na vifaa vinavyohusika. Kwa hivyo, hii inakuwa sio huduma ya dharura.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Naibu Spika, nilichouliza mimi ni kwamba wizara inachukua hatua gani ya kuhakikisha anakuwepo daktari wa mifupa kwa muda wa masaa 24, hilo ndio swali langu niliilouliza na ndio hoja yangu hiyo. Sijui Mhe. Naibu Waziri kanisikia au hakunisikia.

Serikali au wizara inachukua hatua gani baada ya kutokea ajali mara nyingi akiwa huyo daktari hayupo. Mhe. Ali Salum Haji ni shahidi wa suala hili, anijibu tu kuwa wizara inachukua hatua hii na hii au kama hapana uwezo, serikali haijui kuwa kitengo cha mifupa ni muhimu sana kuwepo daktari masaa 24 pale. Wananchi wetu wanateseka. Swali langu liko hapa Mhe. Naibu Waziri aniambie kama wako njiani au wako mbioni kuajiri daktari wa saa 24 awepo wa mifupa, ananijibu daktari ni mmoja tu. Mimi naomba swali langu anijibu tena Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, nafikiri haya maneno yote niliyoyazungumza hapa ndio yanayoeleza utaratibu wa jinsi gani hospitali inafanyakazi. Suala la wizara nimelisema pia kwamba wizara haihusiki na kupanga madaktari, ni hospitali ndio inahusika na kupanga madaktari.

Mhe. Naibu Spika: Mnaye daktari wa mifupa au mtaalamu wa mifupa hospitali, mnaye mmoja tu?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ndivyo nilivyosema.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Jaku Hashim Ayoub, nadhani Mhe. Naibu Waziri kakueleza vya kutosha kwamba hospitali mtaalamu wa mifupa yuko mmoja tu, na ikitokea dharura au ikitokea ajali anafanyakazi saa zote hawana daktari wa pili.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuweza kumuuliza Mhe. Naibu Waziri wa Afya swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri wa Afya kutokana na maelezo yako ambayo ni mazuri sana, hivi karibuni kulitokea ajali wananchi wangu alianguka na kuumia na wengine wakaumia miguu na wengine wakaumia mbavu, lakini kwa bahati nzuri nilimkuta muhusika katika sehemu ile ambayo walipelekwa wodini.

Mhe. Naibu Spika, swali langu liko hapa Je, Mhe. Naibu Waziri hao madaktari bingwa ambao tunawaweka na wakatumika kwa muda huo wa usiku. Je, hii *night allowance* wanaendelea kulipwa?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, nashukuru Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kwa kuweza kufahamu kwamba hospitali kuna madaktari saa 24. Huo ndio ukweli hospitali imejipanga na saa zote kunakuwa na madaktari.

Madaktari wale wanapangwa *night call* na wanapaswa kulipwa *night call*. Wanalipwa *night call* baada ya kwishakufanyakazi wakawekewa hesabu zao yakapelekwa maombi Wizara ya Fedha. Wizara ya Fedha inakuwa inawalipa, lakini inategemea zikiwepo kwa kipindi kile kile wanalipwa kwa wakati ule, na ikiwa hazipo basi zinawekwa kama madeni baadaye wanakuja kulipwa.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali jengine la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwa sababu hospitali ya Mnazi Mmoja kama wanavyozungumza kama ni hospitali ya rufaa na kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri kakiri kwamba daktari wa mifupa ni mmoja tu aliyepo hospitali ya Mnazi Mmoja.

Je, Mhe. Naibu Spika, huoni kuwa hilo ni tatizo kuwa na daktari mmoja kwa nchi nzima na kama hivyo ndivyo, ni lini kwa kupitia wizara ya afya itaona kwamba kuna haja ya kutafuta daktari mwengine wa mifupa, ili aweze kuhudumia matatizo ya watu wetu wanapopata ajali katika nchi yetu na ni lini watampata daktari huyo?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, anachosema Mhe. Mjumbe ni kweli na sio daktari wa mifupa tu, nilizungumza humu kuwa karibu kila idara ina daktari mmoja bingwa, hao wako Mnazi Mmoja. Madaktari wa aina hiyo wanatakiwa wawepo karibu kila hospitali, sio Mnazi Mmoja tu ambayo ni ya rufaa, mpaka Pemba wanatakiwa wawepo, mpaka Micheweni wanatakiwa wawepo.

Mhe. Naibu Spika, lakini daktari anasoma na kusomeshwa, waliokwisha kusoma na wakarudi ndio hao tulionao na ndio maana tumewaweka kwenye hospitali ya rufaa. Wizara ina mipango ya kuwasomesha madaktari wa fani mbali mbali, wako nje wengi amba wanaosoma, wakirudi tutawapanga katika sehemu husika.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 - Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante, Waheshimiwa Wajumbe tuna mchangiaji mmoja Mhe. Dkt. Sira Ubwa Mamboya, akimaliza yeye tutamwita Mhe. Waziri kwa kufanya majumuisho. Kwa hivyo, Dkt. Sira tunakupa dakika 20.

Mhe. Dkt. Sira Ubwa Mamboya: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa na mimi fursa hii kuchangia katika hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, katika yale ambayo nahisi tunahusika kwa pamoja ili niweze kuyatolea ufafanuzi.

Mhe. Naibu Spika, kwanza napenda nimpongeze Mhe. Waziri, watendaji wake, niwapongeze Wakuu wa Mikoa na wa Wilaya na watendaji wao, niwapongeze Wakurugenzi wa Manispaa na niwapongeze Makamanda wa Vikosi na maaskari wao, wanapaswa kupongezwa hao kwa sababu ya kazi kubwa wanazozifanya.

Mhe. Naibu Spika, kulizungumzwa suala linalohusiana na sheria, ambazo tunahisi kwamba waliozungumza hazijatekelezwa ipasavyo. Tulipitisha sheria hapa ambayo ni ya afya ya jamii na sheria ya mabwana afya. Sheria hizo zinawajibika kufanyiwa kanuni na Wizara ya Afya ndio iliyokuwa na jukumu kwa sababu ndio mdau au muhusika mkubwa wa kanuni hizo na wizara nyengine, kwa sababu afya ya jamii ni suala .....

Mhe. Naibu Spika, napenda niwafahamishe wawakilishi wako kwamba rasimu ya kanuni hiyo imeshakamilika ipo tayari na wadau wote waliohusika walishirikishwa, kwa hivyo kinachosubiriwa ni Baraza kutangaza ili iweze kufanyakazi. Hilo liko nje ya uwezo wa wizara yetu. Lakini kwa upande wetu Wizara ya Afya na hasa kwa Mjini Magharibi, katika ugawaji wa wafanyakazi mwaka jana tulijitahidi kuweka wafanyakazi wa afya kila sehemu Mjini na Magharibi.

Kwa hivyo, tutakuwa na uwezo sheria hiyo itakapoanza kufanyakazi na tutahakikisha kwamba kwa kuanzia angalau Mjini na Magharibi ziweze kufanyakazi, baadaye na sehemu nyengine. Lakini tatizo linalojitokeza Mhe. Naibu Spika, wananchi wetu wa Zanzibar hawapendi kufuata sheria bila ya kushurutishwa. Siku zote tunahimizwa tufuate sheria bila ya shuruti, lakini bado linakuwa ni tatizo.

Kama siku mbili mimi nilikuwa kwenye gari nakuja hapa Barazani, nikasikia tangazo wanatoa asubuhi kwamba wananchi mnatakiwa mumwage taka kuanzia saa 12:00 usiku hadi saa 1:00 asubuhi, ili tuwape nafasi wanaosafisha wasafishe. Mimi wakati nasikia hivyo nikapita njia ya Mpendae, karibu saa 2:30 nikamkuta mtu na doo lake anakwenda kumwaga taka. Nikasema hivi hawa watu hawakusikia taarifa au wanafanya makusudi.

Isitoshe suala la usafi Mhe. Ali Mzee kasema ni la kila mtu, sisi tulipokuwa wadogo asubuhi hatuamki majumbani mwetu tukenda skuli bila ya kufyegia ndani na bila ya kufyagia uwanja wetu. Siku hizi huwezi ukamkuta mtu anafyagia uwanja wake, labda awe kizee wa zaidi ya miaka 70 ndio utamkuta anafanya hivyo. Utaratibu wa watu kusafisha hata majumba yao imekuwa ni shida, seuze kusafisha nyumba.

Pia wenye kukaa katika majumba makubwa wao ndio wanakaa juu wanarusha vipolo chini, wanamwaga taka ovyo, halafu wanasema watu wa Manispaa waje kusafisha. Mimi nafikiri kwa hilo hatuwatendei haki, kila mtu anawajibika kusafisha kwake na kuzichukua taka kuzipeleka pahala panapohusika.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kuzungumzia suala la usafi, sasa napenda nizungumzie suala la vikosi. Suala la vikosi mwaka huu limesemwa vizuri sana sijawahi kuona wala kusikia. Mimi nilitegemea haya yawe pale tulipoanza *GNU*, lakini bado walivisakama vikosi kwamba ni wauwaji, wanavaa ninja, wanapiga watu wakasema waliyosema. Naona hapa kidogo mabadiliko yamekuja, sio mwanzo wa hiki kikao, maana mwanzo wa kikao pia hayakuwa haya. Lakini Mwenyezi Mungu kapitisha rehma yake, wamempata mja aliyekuwa mwema kawafahamisha nafikiri na wamefahamu, maana sasa kila anayeinuka vikosi vyetu hivi, vikosi hivi, hamuwapi hiki, hamuwapi kile.

Mhe. Naibu Spika, jana nilimsikia kiongozi wa UKAWA anasema, jamani msiwasikame CCM, kwenye siasa hakuna adui wa maisha, hakuna rafiki wa maisha. Kwa hivyo, wanaposimama CCM msiwatolee maneno. Nikasema eeh Mwenyezi Mungu afadhali watu wamefahamu, kwa sababu sasa nafikiri tunaelekea kuliko sahihi.

Nawashukuru wajumbe wote mliokuwa zamani mnasakama, lakini safari hii mkatoa pongezi kwa vikosi. Kwa sababu hilo walikuwa wanastahiki tangu huko nyuma, sio jana na leo. Mimi nashangaa zamani kulikuwa kuna usemi, wa ndege mmoja anaitwa kurumbizi. Kurumbizi akiamka asubuhi kichakani anaanza kukinyonyoa kichaka hiki kinanuka mavi, kichaka hiki kinanuka mavi huku anatoka huyo, lakini akirudi jioni anasema, kichaka hiki kinanukia udi, sio udi wa juzi hapana, kinanukia udi, kinanukia mafuta mazuri. Sasa ndio haya yanayofanywa. Majeshi hayo hayo yalikuwa hayafai, lakini leo yanafaa.

Mhe. Naibu Spika, kuna msemaji mmoja hapa alizungumza kitu ambacho nina mashaka nacho kidogo, kusema kwamba tunataka majeshi yetu yajitayarishe kwa sababu tunakokwenda hivi ndivyo vikosi vya Zanzibar hatuna vingine, tunavitegemea itakapokuja serikali Zanzibar ikipata mamlaka kamili, maana yake hivi ndio vitakuwa vikosi vyetu.

Jamani, Zanzibar mamlaka kamili imepata zamani, hivyo bado mpaka leo hamjafahamu. Mamlaka kamili ya Zanzibar yamepatikana tarehe 12 Januari, hayo mamlaka mengine naona kama ni ndoto za alinacha. Maana wenye mamlaka kamili waliopindua wapo na watoto wao tupo, tutahakikisha tunayalinda, tunayaenzi na tunayadumisha, potelea mbali.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa napenda nizungumzie suala la Madiwani. Hapa jana na huko nyuma yalizungumzwa sana kuhusu Madiwani na taratibu ziliopo kwamba hawalipwi kama wanavyolipwa watu wengine.

Mhe. Naibu Spika, yalizungumzwa na wanajua kwamba hili suala ni kuanzia Wawakilishi, Wabunge na Madiwani. Hivi ni vyeo vya kisiasa na inatakiwa serikali iwalipe Madiwani, mimi sikatai nataka Madiwani walipwe, kuwe tu na ule utaratibu wa jinsi gani ya kulipwa. Kwa sababu nikiangalia taratibu ziliopo, serikali siwaoni Madiwani wako wapi, nikiangalia Baraza la Wawakilishi na muhimili mzima huu siwaoni Madiwani wako wapi, nikiangalia kwenye vikosi vingine huko ambako watu wanalipwa siwaoni. Labda utengenezwe utaratibu, lakini walipwe ikiwezekana wanastahiki. Mhe. Naibu Spika, hiyo hoja ya kulipa ndio inayonipa wasi wasi.

Mhe. Naibu Spika, Madiwani wanatakiwa washirikiane na Masheha wafanyenao kazi kwa pamoja na *Alhamdulillah* kuna wanaofanya kazi na Masheha, lakini Masheha hao hao ndio wanaolalamikiwa na kuna Madiwani ambao hawafanyikazi na Masheha, wanafanyakazi ya siasa tu, sasa tuwalipe kwa msingi upi. Diwani ambaye hafanyikazi na Sheha akiwa anafanyakazi ya siasa na kukitumikia chama chake tu, Sheha hana uhusiano naye tutawalipa vipi. Labda tujirekebishe Madiwani wafanyekazi kama wanavyostahiki na ukenda ukenda sehemu nyengine Diwani na Shaha kuliko paka na chui, na kila watu wakiinuka hapa Masheha, Masheha sasa watalipwaje watu hao wakati hizo kazi wanatakiwa wafanyiwe na Masheha mimi nafikiri nalo hilo likarekebishwa kwanza halafu wale wanaofanya kazi na Masheha na wanaotakiwa kufanya kazi na Masheha wafanye ili sasa taratibu za kulipwa kama zipo walipwe.

Mhe. Naibu Spika, nafikiri ujumbe umefika, Ahsanteni. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa fursa ya kuweza kuja tena kwa mara nyingine, kuja kutoa ufafanuzi na kujibu baadhi ya masuali ambayo waheshimiwa wajumbe wameyauliza katika kuchangia bajeti yangu ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa Na Idara Malum za SMZ.

Mhe. Naibu Spika, la pili naomba kuwashukuru na kuwapongeza sana sana waheshimiwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa michango yao na maoni yao na ushauri wao ambao wameutoa kuhusu bajeti hii ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, na Idara maalum za SMZ. Najua kwamba waheshimiwa wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi wamechangia sana maoni mbali mbali na ni Wizara ya mwanzo ambayo imepata wachangiaji wengi katika Baraza lako hili tukufu, lakini ni Wizara ya mwanzo ambayo imechukua siku mbili na nusu kuchangiwa ndani ya Baraza lako hili tukufu.

Mchango huu ambao umetolewa na Waheshimiwa Wajumbe ninauthamini utanisaidia na utaniwezesha kuweza kutekeleza majukumu yangu hasa katika bajeti hii ya mwaka 2014/15, naomba niseme waheshimiwa wajumbe wao ni mashahidi kwamba tokea nimekabidhiwa bajeti hii kama walivyosema wajumbe wengine kwamba hii ndio bajeti yangu ya mwanzo kwa Wizara hii. Nimeteuliwa tarehe 20/8/2013 mwaka jana mpaka ikifika tarehe 20/08/2014 ndio nitakuwa nafikia mwaka mmoja tokea kuwepo katika Wizara hii.

Kwa hivyo naomba waheshimiwa wanielewe kwamba yale yote ambayo watayaona yana mapungufu ni kwa sababu tu pengine ya upya wangu, lakini hata hivyo waheshimiwa ni mashahidi kwamba tokea nimeteuliwa katika Wizara hii sijakaa kitako ofisini. Madhumu ya kutokukaa kitako kwenye deski langu muda wote na kupitia maeneo kwa ajili ya kujifuza maana si aibu mtu kusema anajifunza. Katika kipindi hiki cha mwaka mmoja kasoro na hivi sasa niko tayari kuweza kuyafanyia kazi yale ambayo nimejifunza na hasa kutokana na mchango ambao umetolewa na waheshimiwa wajumbe wa baraza lako tukufu.

Nasema nawapongeza wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi wa vyama vyote vilivyomo humu ndani kwa maoni yao na michango yao ambayo wamenipa. Baada ya utangulizi wa kuwapongeza Wajumbe pia nataka nipongeze kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ambayo nayo imekuwa ni dira katika kunisaidia kuiandaa na kuitayarisha bajeti hii.

Vile vile kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu hivyo nakubaliana na ushauri ambao wamenipa na hasa hasa pale walipoipitia rasimu ya bajeti yangu na wakaweza kunipa ushauri na hii leo nimeweza kuwasilisha bajeti na wajumbe wameweza kuichangia. Kamati hii isingefanya kazi zake vizuri basi nadhani hata wajumbe mngepata tabu sana namna ya kutoa michango yenu.Naomba niwataje wajumbe hao wa kamati;

Mhe. Ussi Jecha Simai	Mwenyekiti
Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Makamu Mwenyekiti
Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Mjumbe
Mhe. Mahamoud Thabit Kombo	Mjumbe
Mhe. Nassor Salum Ali (Jazira)	Mjumbe
Mhe. Suleiman Hemad Khamis	Mjumbe
Mhe. Wanu Hafidha Ameir	Mjumbe

Wajumbe hao walisaidiwa na Makatibu wawili ambao ni;
Nd. Aziza Waziri Kheir
Nd. Khamis Hamad Haji.

Wote kwa pamoja wamesaidia sana katika kunifanya niweze kuiandaa na kuitayarisha bajeti hii.

Mhe. Naibu Spika, kamati imeshauri Ofisi yangu kuweka mazingira mazuri kwa watumishi wa Wizara yangu kama waheshimiwa wajumbe walivyoungana nayo katika kuweka msisitizo kama mtakumbuka. Wajumbe wengi wamezungumzia juu ya masuala ya maslahi kwa wapiganaji wetu wa Vikosi vya SMZ, nasema wajumbe wa pande zote mbili wa vyama viliomo ndani ya Baraza la Wawakilishi. Kamati pia imeshauri kufuatilia kwa vitendo katika mambo mengi tu ambayo nadhani nikiweza kuyataja hapa naweza kuchukua muda mrefu.

Niwashukuru pia wajumbe ambao wamechangia kwa kusema ni bajeti ya mwanzo ambayo tokea tumeanza kwenye bajeti ambayo haijachangiwa kwa maandishi. Wajumbe wote wametamani kusema wenyewe na kusikika wenyewe, kwa nini wamefanya hivi? Wamefanya hivi kwa sababu bajeti hii moja kwa moja imewagusa wananchi na kama inawagusa wananchi isingekuwa vyema wengine kusema kwa maandishi, lakini waheshimiwa wajumbe wote 39 waliochangia wamesema wenyewe na wananchi wamewasikia.

Wajumbe waliochangia kama nilivyosema wa kwanza ni Mhe. Ussi Jecha Simai, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe, Mahamoud Mohammed Mussa, Mhe. Ali Salum Haji, Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa, Mhe. Asha Abdu Haji, Mhe. Salmin Awadh Salmin, Mhe. Salehe Nassor Juma, Mhe. Hassan Hamad Omar, Mhe. Farida Amour Mohammed, Mhe. Abdalla Juma Abdalla, Mhe. Suleiman Hemed Khamis, Mhe. Mohammed Mbwana Hamad, Mhe. Panya Ali Abdalla, Mhe. Hussein Ibarahim Makungu, Mhe. Subeit Khamisa Faki, Mhe. Abdi Mossi Kombo, Mhe. Marina Joel Thomas, Mhe. Asha Bakari Makame, Mhe. Rufai Said Rufai, Mhe, Shadya Mohammed Suleiman, Mhe. Salma Mohammed Ali, Mhe. Mgeni Hassan Juma, Mhe. Omar Ali Shehe, Mhe. Mohammed Abdalla, Mhe. Hija Hassan Hija, Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, Mhe. Salim Abdalla Hamadi, Mhe. Ali Mzee Ali, Mhe. Fatma Mbarouk Said, Mhe. Mohammed Haji Khalid, Mhe. Salma Bilali, Mhe. Raya Suleiman Hamad, Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mhe. Amina Iddi Mabrouk, Mhe. Mussa Ali Hassan na Mhe. Dk. Sira Ubwa Mamboya (*Makofi*)

Wote hawa nawashukuru kwa namna walivyochangia bajeti hii. Nawashukuru sana wajumbe wako hawa wa Baraza lako tukufu kwa kuweza kutekeleza vyema jukumu lao la kuwawakilisha wananchi na kwa vile kila mara wako karibu na wananchi nawapa taarifa nyingi na nitaendelea kuthamini sana michango yao na mafanikiyo tuliyoyapata kwa sehemu kubwa inatokana na maoni na miongozo yao. Mimi Haji Omar Kheir Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, nawaomba tuendelee kushirikiana kujenga taifa letu yaani tukifanikiwa tumefanikiwa sote, na tukiharibikiwa tumeharibikiwa sote.

Mhe. Naibu Spika, natanguliza shukurani zangu za kipekee kwa waheshimiwa wajumbe wote kwa kututhamini na kutambua umuhimu na majukumu mazito ya Ofisi hii ya kulinda amani ya nchi, usalama wa raia na mali zao pamoja na jukumu kubwa la kuhakikisha huduma bora na maendeleo endelevu yanawafikia wananchi katika maeneo waliyopo.

Aidha naungana nao juu ya ukweli kwamba watumishi wetu wa vikosi vya Idara Maalum wana kazi ngumu na nzito na wanafanya kazi katika mazingira magumu kutokana na ufinyu na uchakavu wa majengo yao, lakini pia uhaba wa vitendea kazi. Kwa kuliona hilo Ofisi yangu inajitahidi kuyafanyia kazi kwa kuchukua hatua mbali mbali kukabiliana na changamoto hizo kama inavyoonekana katika hotuba ya Ofisi yangu niliyoiwasilisha.

Mhe. Naibu Spika, michango, maoni ushauri na masuala yote yaliyotolewa na Waheshimiwa Wajumbe ni muhimu katika utekelezaji wa kazi zetu, hivyo tunayapokea na tunaahidi mimi na wenzangu kuyafanyia kazi ipasavyo. Waheshimiwa wengi waliochangia hotuba ya bajeti ya Ofisi yangu walizungumzia sana suala la mazingira ya kazi na maslahi ya watumishi wa vikosi vya Idara Maalum za SMZ.

Utendaji kazi katika Baraza la Manispaa hususan mradi wa *ZUSP,* maslahi ya Madiwani, uvamizi wa maeneo ya wazi na ujenzi katika mabonde ya kilimo, sambamba na hayo baadhi ya wajumbe walitoa ushauri kwa lengo la kuleta ufanisi kiutendaji ndani ya ofisi yangu napenda kuwahakikishia kwamba Ofisi yangu ipo tayari kufuata ushauri wao hasa kwa yale mambo ambayo yamo ndani ya mamlaka ya ofisi yangu, na kwa mengine ambayo yanahusiana na mamlaka nyengine za Serikali, natumai kwamba taasisi hizo wameyasikia nasi tuko tayari kushirikiana nao katika kuyatekeleza na kuyapatia ufumbuzi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba niende katika kutoa ufafanuzi wa michango ya waheshimiwa wajumbe.

Mhe. Naibu Spika, naomba unipe fursa ya kutoa ufafanuzi kwa makundi ambayo yametoa maoni kwa hivyo sitotoa ufafanuzi kwa mtu mmoja mmoja isipokuwa kwa yale maeneo ambayo mtu atakuwa amechangia yeye peke yake, kwa hivyo naomba kusema juu ya suala zima la elimu ya vitambulisho.

Ofisi hii ya usajili na kadi za Utambulisho imezungumzwa sana na Waheshimiwa Wajumbe wengi kwa maoni tofauti tofauti, wengine wamezungumzia suala la wananchi kupewa taaluma ili waelewe sheria na taratibu za kusajiliwa, napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe ambao wamelizungumza hili. Lilianza kuzungumzwa na Mhe. Ussi Jecha Simai, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria lakini na Wajumbe wengine, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mwenyekiti wa kamati kwamba tumelipokea na kwa sababu yeye ndiye msimamizi wa Wizara yetu tutahakikisha jambo hili tunalifanya, nasema nimemtaja yeye kwa sababu aliligusa na Waheshimiwa wajumbe wengine wamelizungumza.

Ninachotaka kusema kwamba hivi sasa elimu tayari inatolewa katika vyombo vya habari mbali mbali ikiwemo ZBC redio, kuna kipindi kinasikika mara mbili kwa wiki Jumanne na marejeo jumapili, lakini pia tuna kipindi kwenye Zenj FM juu ya kutoa taaluma hii lakini Ofisi yangu inalipokea kwa ujumla wake na kuendeleza au kuzidisha taaluma ili wananchi waweze kuielewa sheria na kuelewa haki yako ya kuweza kujisajili katika Ofisi hii ya Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi.

Kutoanza kutolewa vitambulisho kwa wageni jambo hili limezungumzwa pia na Mheshimiwa Mwenyekiti lakini na waheshimiwa wengine, ni kweli vitambulisho kwa wageni havijaanza kutolewa, kinchosubiriwa ni kukamilika kwa kanuni ambazo zimeshawasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu kwa ushauri wa kisheria, na hatimae zitarudi kwangu na mimi nitazitia saini ili zianze kutumika. Kwa hivyo suala hili la vitambulisho kwa wageni litaanza kutekelezwa tu pale ambapo kanuni nitaanza kuzisaini, na si muda mrefu Mwanasheria Mkuu atamaliza kazi yake ya ushauri wa kisheria na hatimae nitaziweka saini ili ziweze kutumika.

Kukabidhiwa vitambulisho kwa watu wasiohusika hili zaidi lilizungumzwa na Mhe. Rufai na baadhi ya Waheshimiwa wengine, katika hili nitamuomba Mheshimiwa Mjumbe nishirikiane nae lakini ninachoamini mimi ni kwamba hilo haliwezekani hasa ukizingatia kwamba kila juhudi zinachukuliwa za kitaaluma za kitaalm na za kisheria kuhakikisha makosa kama ya kidunia hayatokei, lakini binaadam ni sisi ndio maana nikasema nitashirikiana na Mhe. Rufai ile rekodi aliyoiweka Mhe. Dk. Mwinyi Haji akiwa waziri na kufuatana na Waheshimiwa wajumbe kwenda kufuatilia jambo hili basi kwa hili na mimi nitaiga mwenzangu alichofanya, ili na mimi niende nikagundue tatizo liko wapi. Kwa hivyo Mhe. Rufai nitakuomba kwa wakati wetu tusaidiane katika hili ili niweze kubaini matatizo, nia ya Serikali sio kutesa wananchi wala kunyima haki zao wananchi. Bali kila mmoja apate haki yake kwa mujibu wa sheria, kwa hivyo hili kama lipo nipo tayari kufuatana na wewe kupata ushauri na ushauri nimeupokea na tutalifanyia kazi na tutalivalia njuga ili kama lipo liweze kuondoka.

Upatikanaji wa vitambulisho Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Hassan Hamad, Mhe. Suleiman Hemed na Mhe. Subeit Khamis Faki. Hili wamelizungumza bado narudia pale pale kila mwananchi anayetimiza masharti ya kupata kitambulisho cha Mzanzibari anapewa bila ya tatizo lolote. Suala ni kufuata utaratibu na haya yote yanafanyika kwa mujibu wa sheria. Suala la kunyimwa wananchi vitambulisho mimi ninavyoamini halipo lakini wenzangu mmenambia lipo nalo hili, nataka majibu yangu yawe yale yale, kama lipo basi ni vizuri tukayabaini hayo maeneo ambapo hili tatizo lipo basi tuweze kulipatia ufumbuzi. Kwani tunaamini kwanza suala la kunyimwa wananchi vitambulisho halipo isipokuwa wananchi wengi wanakwepa utaratibu wa kisheria ambao unaanzia kwa masheha hususan wakati wa kuhama na kuhamia katika shehia.

Kuhusu wazee kujisajili kama hawawezi; utaratibu wa kufika kwa Mkuu wa Ofisi kwa Pemba na hata Unguja Ofisi Kuu tunazo *mobile station*. Kwa hivyo *mobile station* hizi tutazitumia kuwatambua hawa ambao hawafiki katika maeneo hayo ama kwa uzee ama kwa ugonjwa ili waweze kupata haki zao. Ikibidi tunao uwezo wa kumsajili popote alipo mtu. Jukumu hili ni letu kama mlivyoshauri. Kwa hivyo tutamsajili mtu pahala popote alipo, alimradi tu awe anatimiza masharti. Nataka niliunganishe na suala lile la cheti cha kuzaliwa.

Kama mnakumbuka Waheshimiwa Wajumbe mwanzo wa uandikishaji wa vitambulisho hivi hakukuwa na haja mtu kuulizwa cheti cha kuzaliwa. Lakini baadae kwa mtu ambaye amezaliwa baada ya mwaka 1964, tunajua kwamba suala hili hawa watakuwa na umri mdogo kwa hiyo ili tumthibitishe lazima tupate cheti cha kuzaliwa. Lakini kwa hao wengine mimi nadhani tutatizama kumbukumbu zetu katika kulitatua tatizo hili, tutatizama kumbukumbu zetu zinasemaje. Tuna *data base* ambazo zilianza kuwandikisha hawa watu, tutatizama tukijua kuwa hawa watu walikuwemo kwenye *data base* yetu lakini kuna mambo, nadhani hilo ni jambo ambalo tunaweza tukalifanyia kazi kwa kushirikiana.

Lazima mbainishe yale maeneo ambayo yana matatizo *specific* twende katika yale maeneo kana kwamba hapa kuna mzee huyu. Kwa mfano kama alivyosema Mhe. Hassan Hamad amesema yeye mkwewe, sasa basi nadhani twende tukapate uhakiki huo halafu mimi nadhani Mkurugenzi wangu wa Idara ya Usajili wa Vitambulisho hana matatizo hata kidogo katika kumpatia mtu haki yake, ambaye ana sifa za kuandikishwa kama ni mzanzibari mkaazi.

Maana hapa tutafautishe kuwa Mzanzibari Mkaazi na Mzanzibari nitakuja kutoa ufafanuzi kwa ushahidi ambao tunao wa tukio jengine ambalo limezungumzwa hapa hapa Barazani. Tunamuona mwenzetu ni Mzanzibari kumbe ana ushahidi mwengine kwamba sio Mzanzibari. Sasa mimi nadhani tukifikia huko tumefikia pahala pazuri. Kwa hivyo niko tayari kushirikiana na Waheshimiwa kwenda huko alimradi tu yule mtu ambaye tunamuona analalamika awe amefuata utaratibu na awe amezungumzwa ndani ya sheria kwamba anastahiki kupata haki hiyo kisheria, ambayo inasisitiza kuwa muhusika mwenyewe anapaswa kujisajili na kuhakikisha kuwa anapata kitambulisho chake.

Utaratibu huu ulishafanyika mara nyingi lakini bado vitambulisho vipo katika maeneo mengi. Na hili tusilibishie kwamba vitambulisho vipo katika maeneo mengi *weather* vilivyoandikishwa katika njia za udanganyifu, huu udanganyifu sisi ndio tunaoukataa.

Sasa tunataka tujiridhishe na hilo ili tuhakikishe kwamba tunawapa haki zao watu kwa mujibu wa sheria. Tatizo la vyeti vya kuzaliwa nadhani nimeshalieleza limezungumzwa na Mhe. Hassan Hamad, vyeti vya kuzaliwa ndio kielelezo kikuu katika usajili ukiambatana na barua ya sheha.

Ni kweli kabisa kuna wimbi kubwa la vyeti vinavyosadikiwa sio halali, vyeti vya kughushi na vinatengenezwa nje ya utaratibu Waziri wa Katiba na Sheria ni shahidi wa hili. Ofisi inajitahidi kufanya kazi kwa karibu na Ofisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo ili kuhakikisha uhalali wa vyeti vya kuzaliwa na kumuwekea muhusika taarifa halali na inapobainika udanganyifu hupelekwa mashauri katika vyombo vya sheria. Kwa hivyo tunatambua kwamba tunaofatilia zaidi vyeti ni wale ambao wenye umri mdogo, wale watu wazima tutakwenda kuthibitisha huko kama nilivyosema.

Suala jengine lililozungumziwa hapa ni juu ya kupatikana kwa kiwanja cha kujenga Ofisi ya Polisi Jamii Kwaalinatu, Mhe. Mshimba nisikilize sana katika hili. Hili jambo lilizungumzwa na Mhe. Mshimba lakini ieleweke kwamba Baraza la Manispaa kazi yetu ni kutunza viwanja vilivyo wazi, lakini hatuna mamlaka ya kummilikisha mtu au taasisi yoyote ile kiwanja. Wenye mamlaka hii ni Idara ya Ardhi na Usajili ambayo iko chini ya Wizara ya

Ardhi, kazi yetu sisi ni kutoa kibali cha ujenzi pale ambapo Wizara ya Ardhi imeridhiwa hilo eneo la wazi liweze kutumika.

Sasa sisi si kazi yetu kutoa *open space* na hili baada ya kuingia katika Wizara hii jambo la kwanza nililowaasa wenzangu kwa maana ya watumishi kutoa vibali vya matumizi ya ardhi maeneo ya wazi. Niliwaasa na nitaendelea kuwaasa kazi yetu sisi kuidhinisha ujenzi pale Idara ya Ardhi inapokuwa tayari imetoa hati ya matumizi ya ardhi. Sasa nitamuomba Mhe. Mshimba kwamba hili jambo hapo pahala nimesha patembelea jana nimepaona panazungumzika lakini katika mazungumzo hayo lazima tufuate taratibu na sheria za nchi. Watu wa mipango miji na watu wa ardhi waridhie matumizi ya eneo hilo, wakesharidhia sisi UDCA pamoja na Baraza la Manispaa kazi yetu itakuwa ni kutoa hati ya ujenzi kwa madhumuni hayo ambayo yamekusudiwa. Sasa Mhe. Mshimba nadhani anaweza baadae mimi unanijua si mbishi katika mambo haya yanayowahusu wananchi ukitaka nikushauri zaidi mimi na maofisa wangu tutakushauri, tushirikiane na Wizara husika, jambo la Polisi Jamii ni jambo muhimu wanasaidia sana wananchi katika kuimarisha ulinzi wa wananchi wetu.

Kwa hivyo mimi nakubaliana nao kwamba wanahitaji kuwa na pahala pa kuweza kufanyia kazi zao na wewe ulishawahi kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi taratibu hizi unazijua. Kwa hivyo nitakushauri tushirikiane mimi, wewe, Waziri wa Ardhi tuone kwamba hilo jambo linayumkinika, basi nadhani sisi hatuna tatizo katika kulifanyia kazi jambo hili.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine ambalo limezungumziwa ni suala la ukosefu wa Ofisi ya Wilaya ya Mjini ambayo hivi sasa wanatumia hoteli ya Bwawani kama ni wapangaji wa ofisi ile na jambo hili limezungumzwa na Mheshimiwa mmoja Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa. Nataka niseme tunajua ugumu na tatizo la Ofisi ya Wilaya ya Mjini kufanyakazi pale. Na walihamia pale baada ya jengo walilokuwa wakitumia lilikuwa ni jengo linalomilikiwa na Wizara ya Viwanda na biashara ambayo Wizara ya Viwanda na Biashara waliamua kulichukua jengo lile na kulifanyia matengenezo, kwani hata wao walikuwa na watumishi wao ambao hawana pa kuwaweka. Kwa hivyo jengo lile sasa hivi liko chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara na haliko bure wameiingizwa watumishi wa Wizara ile baadhi yao.

Sasa ni kweli Ofisi ya Wilaya ya Mjini imekodiwa pale Hoteli ya Bwawani, tunajua si pahala muafaka sana panaweza pakawa hapana *status* ya kuwepo Ofisi hiyo, lakini kwa sababu hatuna pengine kwa muda huu tupo pale. Hata hivyo Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi imo katika jitihada za kulitafutia ufumbuzi wa kudumu suala la kuipatia ofisi hiyo majengo ya kutolea huduma kwa wananchi wa Wilaya hiyo. Miongoni mwa jitihada hizo kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ukurasa wa 29 hadi 30 kwamba tuko katika hatua za mwisho za mazungumzo na wawekezaji kwa njia ya PPP kwa lengo la kuanza ujenzi wa jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Magharibi kule Amani. Jengo la kisasa litakalojengwa kule Amani ili utakapokamilika ujenzi wa Ofisi hiyo itapelekea Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mjini kuhamia katika jengo la Mkuu wa Mkoa la sasa ambalo nalo linaendelea na hatua za ukarabati wa hali ya juu ili liendane na hadhi ya Ofisi hiyo.

Nayo kwa sababu ya mpango mzima wa serikali kutafuta maeneo ya kujenga Ofisi za serikali basi nayo itapata ufumbuzi huo. Tunatarajia ujenzi huu uanze mapema mwezi wa Julai mwaka huu, Ofisi ya Mkoa Mjini Magharibi. Kwa hivyo tutakapokamilisha ujenzi huu basi Ofisi ya Wilaya ya Mjini nayo tutaipatia pahala pa kuweza kufanyia kazi.

Ongezeko la vitendo vya kihalifu Mkoa wa Kusini Pemba, hili limezungumzwa sana na Mhe. Saleh Nassor Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Wawi. Ni kweli kabisa tarehe 23/4/2014 Ndugu Mohammed Soud Makame wa Wawi, marehemu huyu alionekana asubuhi ameshafariki dunia katika mazingira ya kutatanisha. Jeshi la Polisi Mkoa wa Kusini Pemba linaendelea na uchunguzi wa tukio hilo na kuwabaini wahalifu waliohusika na tukio hili ili waweze kuchukuliwa hatua za kisheria.

Pili pia Ndugu Farid Abdalla Juma wa Wawi aliingia msikitini na kunajisi mas-hafu, kijana huyu alisemekana ni mgonjwa wa akili kwa hivyo Jeshi la Polisi kwa kushirikinana na Wizara ya Afya na Mahkama inafanya uchunguzi kujua ukweli wa madai hayo na kesi iko mahkamani. Kama hana akili Wizara ya Afya watathibitisha, kama amefanya tu kwa sababu ya vitendo vya kula madawa ya kulevya basi tutathibitishiwa na chochote kitakachotokea basi taratibu za kisheria zitachukuliwa juu ya jambo hili. Kweli sote tunapaswa kulilaani jambo hili la kunajisi mas-hafu kitabu kitukufu cha Mwenyezi Mungu iwapo huyu mtu atakuwa ana akili yeke timamu.

Aidha, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa Kusini Pemba inasimamia ulinzi wa watu na mali zao kwa kushirikiana na wananchi kupitia Vikosi vya Ulinzi na Polisi Jamii kama nilivyoelezea katika hotuba ya bajeti ukurasa wa 51 mpaka namba 121. Kwa hivyo Mhe. Saleh naomba tuendelee kushirikiana na sisi kama serikali tutaendelea kushirikiana na Polisi Jamii ili kuweza kuwasaidia pale inapohitajika kama nilivyosema katika lile jambo la Mhe. Makame Mshimba, na hivi vikundi vyengine ambapo kwa Mkoa wa Kusini Pemba, ninaambiwa kwamba pamoja na lile suala la Mhe. Mohammed Mbwana wa Chambani ninaambiwa kwamba vikundi hivi tayari Jeshi la Polisi limeshawasaidia karibu *packet* 100 za saruji kwa ajili ya kuwasaidia shughuli zao. Kwa hivyo pale kikundi kinapoanzishwa basi nayo inaingiza mkono wake kupitia taasisi zinazohusika.

Ongezeko la baa na kumbi za starehe nalo hili lilizungumzwa sana na Mhe. Saleh Nassor Juma. Mabaa yanayoonekana katika vikosi vya ulinzi tu kama sheria ya vileo inavyoeleza *cap no*. 154 ya mwaka 2008. Kwa upande wa baa za kienyeji Polisi inashirikiana na Polisi Jamii kuhakikisha zinaondolewa, mfano wa baa ya kienyeji iliyoondolewa Minazini Tibirinzi, Machomane, Shungi na Mkungu Malofa. Kwa hivyo baa nyengine zote za kienyeji zilizoko katika maeneo ambayo yanaleta kero kwa wananchi, Serikali ya Mkoa imechukua hatua. Ama kuhusu baa ya *Mortuary Fedel Castro* ambayo Mheshimiwa ameizungumza. Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa iliifunga baa hiyo. Na Polisi Jamii wa eneo hilo iliwakamata wahusika na kuwafikisha Mahkamani na hatua za kisheria zilichukuliwa dhidi yao.

Kwa hii bar ya *Mortuary* ilichukuliwa hatua. Sasa kama imerudi basi nadhani Mhe. Mkuu wa Mkoa na Kamati yake ya Ulinzi na Usalama amesikia ataendelea kuchukua hatua kama alivyochukua hatua hapo mwanzo. Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa kushirikiana na wananchi itaendelea kuyaondoa mabaa yote ya kienyeji yatakayojitokeza ndani ya Mkoa wa Kusini Pemba, hiyo ndio *commitment* yetu.

Hata hivyo hapa kuna tafauti ya baa ambazo zimo ndani ya majeshi; baa zilizomo ndani ya majeshi kuna mambo mengine hapa nadhani tumezungumzia sana suala la maslahi ya vikosi, zana na mambo mengine. Sasa starehe hizi nyengine katika majeshi ni sehemu ya *ration* kwa hivyo anachotakiwa raia asiende pale wabakie wenyewe askari. Sasa niombe wananchi wetu kwamba tukiwaingilia wanajeshi , tukitaka kuingilia mambo yao wanajeshi leo mmekuja mmenishauri kwamba maslahi ya wapiganaji yaongezwe, kesho mtakuja kunishauri maana na hili ni jambo la kiulimwengu. Ili wasiendelee kwenda kufanya uhuni nje wadhibitiwe katika maeneo yao.

Sasa hili nitaomba na kutoa wito kwa wananchi kwamba wasiende kwenye mesi za askari ambazo hawakukusudiwa kwenda wao, na wabakie askari wenyewe ili wasipate nafasi ya kutoka nje huku wakaja wakafanya mambo mengine ambayo hayastahiki kufanywa na askari au walinzi.

Mhe. Naibu Spika, juhudi zichukuliwe na Mkoa wa Kaskazini Pemba kuimarisha Bandari ya Wete. Hili limezungumzwa na Mhe. Farida Amour Mohammed; nakubaliana naye Mhe. Farida kwamba mkoa ufanye kazi hii na tayari umeshafanya vikao na wadau mbali mbali kuzungumzia suala la bandari ya Wete, na kuiomba Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano iweze kuwashajihisha wafanyabiashara wa vyombo vya baharini waweze kwenda katika bandari ya Wete.

Sasa na sisi kwa upande wetu madhali Mhe. Farida hili jambo umelizungumza kwenye wizara yangu, basi nitashirikiana na Mkoa na Waheshimiwa Wabunge na Wawakilishi wa Wilaya ya Wete ili kuwashajihisha wafanyabiashara wa vyombo vya baharini waweze kupeleka vyombo vyao katika bandari ya Wete.

Kutekelezwa kwa agizo la Mhe. Waziri la kuvunjwa ukuta wa hoteli ya *Cristal Resort;* Paje. Jambo hili limezungumzwa na Mhe. Hamza Hassan Juma na jambo hili limeendelea kuzungumzwa na Mhe. Hamza mara nyingi. Nakubali kwamba si utaratibu wa kawaida na wala haupendezi na wala mimi sipendi.

Kilichonizuia mimi kupeleka *bulldozer* kwamba hili jambo limepelekwa Mahakamani. Lakini hata hivyo kama nilivyofanya utafiti juu ya kiwanja cha stendi ya Wete ambao nitatoa ufafanuzi wake na hili nalo nitaendelea kufanya utafiti ili nibaini njia ambazo zinaweza zikatupa mamlaka kwenda kuchukua hatua. Hatuwezi kuwa na mwekezaji jeuri.

Mimi nataka nikuhakikishie Mhe. Hamza mimi hawezi kuniweka mfukoni humu sina ninachohitaji kwake, basi kama hivyo ndivyo wale pale mnaowaona wote wale watendaji wangu wamejaa kule, hakuna anayeweza kunishawishi kufanya mambo ya kuwadhalilisha wananchi. (*Makofi*)

Tutashirikiana na Wizara ya Ardhi, tutashirikiana na Idara ya Uhamiaji, tutashirikiana na *ZIPA* na wenzangu wanielewe itakapoonekana kwamba miongoni mwa taasisi zetu zimehusika pa kukimbilia ninapo, aliyetuteua sisi anaitwa Dk. Ali Mohamed Shein, hakuna mtumishi yeyote yule anayeweza akawa jeuri, hakuna Waziri yeyote anayeweza akawa jeuri mbele yake.

Mhe. Hamza naomba tushirikiane, nitafanya utafiti na uchunguzi hii ni mbinu ya kuwahi Mahakamani ambayo inatumiwa na watu wengi. Sasa ukiujua huu na mwenzako anaujua huu. Mhe. Naibu Spika, hatuwezi kuchezewa ndani ya nchi yetu, tunakubali wawekezaji lakini wawekezaji wenye heshima hatuwezi kubaki na wawekezaji ambao hawana heshima ndani ya nchi hii. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wajumbe naomba mnielewe, mimi niko hivyo na nitajitahidi kusimamia ushauri huu ili tuone kwa kushirikiana na Waziri wa Ardhi tuone tunalifanyaje jambo hili.

Jambo jengine ambalo limezungumzwa katika michango ni Halmashauri ya Kusini haijafikia malengo katika bajeti yake ya mwaka wa fedha 2013/2014 limezungumzwa na Mhe. Asha Abdu; kwanza Mhe. Asha nakupongeza sana kwa kuona Halmashauri yako haikufikia lengo. Wewe unasema umeona choyo lakini choyo cha maana, siyo choyo cha hasadi kwamba unataka na Halmashauri yako iweze kufikia lengo na iweze kuwatumikia wananchi. Taarifa ya makusanyo iliyowasilishwa katika Baraza la Wawakilishi ni kwa kipindi cha robo tatu za miezi tisa na siyo ya mwaka mzima. Hata hivyo bado Halmashauri kwa miezi mitatu iliyobakia inaendelea na makusanyo yake ambapo inategemea kufikia malengo yake iliyowekewa, kwa sasa Halmashauri ya Kusini imeshakusanya jumla ya Tsh. 91,278,000/=.

Sambamba na hili na kipi kilichosababisha kila Halmashauri kuvuka lengo kinachoonekana je ilikuwa ni kukisia kiwango kidogo ili wafikie wavuke kile walichokikisia na halafu ionekane wamevuka lengo. Hili toka niko kwenye Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kama Mwenyekiti nikilisema na nilipofika wizarani nilianza na hili.

Pale mlipoona kwamba Halmashauri ilipanga kukusanya milioni 40, kwa kuelewa hili nilipofika niliwaambia nataka mkusanye milioni 100 kwa kuelewa kwamba zipo. Kwamba yale yaliyozungumzwa na baadhi ya Waheshimiwa hapa yalikuwa yana ukweli ndani yake, na ndiyo maana mimi nilikwenda na *gear* ile ya kuwaambia wewe umepanga kukusanya milioni 1000, ndiyo basi kusanya milioni 150, wewe umepanga kukusanya milioni 80, ndiyo basi wewe kusanya milioni 150 kwa kuelewa kwamba pesa zipo za kuweza kukusanywa na wakaweza kufanya shughuli za maendeleo kwa ajili ya wananchi. Kwa hiyo, ni imani yangu Mhe. Asha, Katibu wa Halmashauri amekusikia, Madiwani wamekusikia na watendaji wa Halmashauri wamekusikia.

Halmashauri za Unguja kufikia malengo ya makusanyo kwa mwaka Mhe. Abdalla Juma Abdalla kwa nini nyengine hazikufikia malengo na amezipongeza sana na yeye ni Mjumbe wa Kamati anaelewa. Nasema kwa upande wa Wilaya ya Kaskazini “A” si vibaya mtu kujipeleka polisi mwenyewe. Niligundua *management* haikuwa nzuri kwa hiyo cha mwanzo nilipofika nilifanya *reshuffle* ya *management*. Kwa hiyo, nampongeza Katibu wa Halmashauri wa sasa na Waheshimiwa Madiwani kwa kuongeza kasi ya makusanyo; kwani vianzio katika Wilaya ya Kaskazini “A” ni vingi zaidi kuliko Halmashauri nyengine yoyote ile. Kwa hiyo, muono wako ni muono wa mbali, nakushukuru umeliona hili.

Kwa upande Pemba nako ongezeko lile limetokana na maagizo niliyoyatoa na baada ya kuelewa kwamba vipo vianzio na yapo makusanyo ambayo hayakusanywi, na kama yalikuwa yanakusanywa yalikuwa yanakwenda wapi? Sasa nikawaambia lazima mkusanye hiki, na hili nataka nilizungumze katika suala zima kwamba wamekusanya zaidi wamevuka lengo, lakini wametumia zaidi wamevuka lengo, si utaratibu wa kawaida.

Na hili nataka nilikemee kwa nguvu zangu zote, na sijaja kulikemea hapa tu kwa sababu Wajumbe mmechangia. Waheshimiwa hao watendaji walipokusanya wakapeleka kwenye Baraza la Madiwani; *of course* Waheshimiwa Madiwani kwa sababu wamepelekewa wameidhinisha, lakini hii ni sawa na *supplementary* au saa nyengine *reallocation* kwa kule wizarani. Walichokosea kwamba walisahau kuwa lazima Waziri kwa sababu ni kitu cha ziada lazima aidhinishe, na maombi yote ambayo wameyaleta nimeyakataa. Nimeyakataa kwa sababu ya kukosa msingi wa utaratibu, sikukataa maamuzi ya madiwani aah! Madiwani wameidhinisha lakini wameidhinisha kitu ambacho hawakukipanga kama alivyokuwa ananukuu Mhe. Salmin Awadh Salmin hapa. Madiwani lazima wapange, sasa walikuwa na *right* madiwani kuidhinisha, lakini ilibidi mimi lazima niruhusu kwa mujibu wa taratibu na sheria ilivyo.

Sasa naomba niwahakikishie Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba hili watendaji walikosea, na kukosea kwao tutachukua hatua za kinidhamu kwa mujibu wa sheria ya utumishi wa umma waelewe kwamba hili walilolifanya siyo sahihi. Maana mtu akikosea halafu ukawa hujamwambia mimi nadhani ataendelea kukosea na kukosea. Lakini Mhe. Abdalla alisema pia kupitia na kufanyia marekebisho ya viwango vya ada. Hilo tunalipokea na tutalifanyia kazi.

Kuanzisha vyanzo vipya vya mapato, kutoa elimu kwa wananchi juu ya ulipaji ada, kuwajengea uwezo watendaji na madiwani katika utekelezaji wa majukumu yao, kusimamia na kufuatilia sheria na kanuni ndogo ndogo za Halmashauri. Mheshimiwa ushauri wako tunaupokea kama unavyotushauri siku zote kwenye Kamati basi tutaendelea kulifanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, mji wa Chake Chake hauna maegesho na vituo vya daladala Mhe. Saleh Nassor na Waheshimiwa wengine wamelizungumza hili jambo. Hili jambo ni kweli Mji wa Chake Chake kwa hivi sasa maegesho yaliyokuwepo yalikuwa pale Marikiti ya zamani ya Chake Chake. Sote tunaelewa kwamba eneo lile sasa ni finyu mno, lakini mipango ya utafutaji wa eneo la ujenzi wa stendi kwa upande wa gari zinazotoka upande wa Mkoa wa Kaskazini Pemba umekamilika. Utafutaji wa eneo umekamilika eneo la Michakaeni hilo ambalo tumeambiwa kwamba lina mabonde, ni kweli kwa sababu ya *nature* ya Pemba hatuwezi kupata pahala palipokuwa tambarare lazima tupate eneo lilokuwa tupu; halina migogoro, ili tuweze kutumia fedha kulirekebisha na kuligeuza kuwa ni stendi.

Na kwamba upande wa gari zinazotoka Kusini limepatikana eneo la Chanjaani katika bajeti ya mwaka huu ya Baraza la Mji Chake Chake wametenga fedha kwa ajili ya kuliweka sawa na kuliweka kifusi, ili eneo lile liwe ni eneo la maegesho ya magari kwa upande wa Pemba. Taratibu za umiliki zinaendelea na hatua za mwanzo za usafishaji wa eneo zinatarajiwa kuanza katika bajeti inayofuata ya mwaka 2014/2015.

Utayarishaji wa maeneo ya maegesho (*parking*) umeshaanza kwa kulitengeneza eneo la maegesho liliopo pembezoni mwa soko liliopo Qatar. Naomba ieleweke kwamba serikali si kama haijataka kutengeneza stendi ya magari, tatizo ilichangiwa na hali ya maumbile iliyopo Chake Chake. Kwa hiyo, sisi kama serikali kwa kushirikiana na Baraza la Mji tunafanya juhudi hizo ili eneo la maegesho liweze kupatikana.

Ni kweli kuegesha magari barabarani kama walivyosema Wajumbe wengi ni tatizo, na hili linatokana na kasoro ambazo sisi kama serikali inabidi tuzirekebishe. Miji hii ilipangwa zamani, na ilipopangwa idadi ya watu ilikuwa ni kidogo, na ndiyo maana kwa Chake Chake stendi ile ya ndani ya soko kule Chake Chake ilikuwa inatosha kwa wakati ule. Lakini lazima tukubali kwamba nchi imepanuka kwa maana ya idadi ya wapewa huduma na watoa huduma. Kwa hiyo, kwa vyovyote vile tatizo hili litaendelea kuwepo, lakini tutashirikiana na taasisi husika ili kuona tunamaliza mipango miji ili kuona sasa tunajipanga katika kuhakikisha huduma zote zinazohitajika ndani ya miji zinapatikana.

Eneo la Qatar kutokuwa na vyoo. Mhe. Saleh Nassor alisema pia hivyo, vyoo vya kutosha vimejengwa ubavuni mwa soko la Qatar labda Mhe. Saleh mtakapokwenda Pemba keshokutwa tukifuata niende nikaone hayo maeneo ambayo yamejengwa hizo huduma za vyoo. Imetenganisha sehemu ya wanawake na wanaume, vile vile maji ya kutosha yanapatikana kupitia katika hodhi lililojengwa na Baraza.

Mhe. Naibu Spika, sasa huduma hizi zipo soko la Qatar kuwa chafu, mashimo na tope eneo la barabarani, hili lilizungumzwa na Mhe. Saleh lakini hata Mhe. Salma aliligusia jambo hili. Mashimo na tope zilizopo barabarani zimesababishwa na mradi wa maji mjini kuchimbua misingi pembezoni mwa barabara katika msimu wa mvua na donge hilo kuingia barabarani.

Sasa tusingekuwa na namna ya kuzuia hili jambo, kwa sababu kuna mradi wa maendeleo unachimba dongo na dongo lile nadhani walishindwa kuweka utaratibu wa kuliondosha na kuliweka pahala pengine likakaa barabarani. Sasa tunakiri kuwepo kwa jambo hilo.
Usafi na matengenezo ya barabara hiyo utafinyika kwa mujibu wa uwezo wa Baraza kwa kutia kifusi eneo hilo baada ya mvua kubwa kumalizika.

Hatua ya ukarabati ya njia hizo kwa kiwango cha lami unategemewa kutekelezwa na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kupitia mfuko wa barabara, ambapo makisio tayari yameshafanyika.

Napenda niliarifu pia Baraza lako tukufu kwa mara ya kwanza mfuko wa barabara unatushirikisha sasa rasmi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum ili kuzitambua njia zinazohitaji matengenezo katika Mikoa, Wilaya na kwenye Halmashauri. Na bajeti ipo tayari imeshatengwa, kilichobakia ni kujua tu ile *ceiling* kwa ajili ya kazi hii. Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wengi ambao wamechangia jambo hili akiwemo Mhe. Hamza Hassan Juma kuhusu barabara yake ya Shaurimoyo/Mboriborini na wengi wengineo.

Mhe. Omar Ali Shehe barabara yake ya Msingini, ile barabara tayari sisi Baraza la Manispaa tumetengeneza misingi ya maji ya mvua, lakini kwenye bajeti hii ya Mfuko wa Barabara nayo barabara ile itajengwa kwa kiwango cha lami. Usafi na matengenezo ya barabara hiyo utafanyika kwa mujibu wa uwezo kama nilivyosema, na hatua za ukarabati zitafanyika.

Huduma za usafi zimekuwa zikifanyika kila siku na taka zinaondoshwa. Soko hilo linatarajiwa kuimarishwa kupitia mradi wa *MIVARF*. Uko mradi ambao unasimamiwa na Wizara ya Kilimo na Maliasili, miongoni mwa kazi ambazo zitafanya mradi huu ni ujenzi wa barabara ziendazo katika maeneo ya kilimo na ujenzi wa masoko. Sasa soko hili limo katika mpango wa kulijenga liwe ni soko la kisasa liweze kutoa huduma nzuri.

Lile ombi ambalo amelitoa Mhe. Salma la daladala kuzungukia eneo la hospitali ili wagonjwa na watu wasiojiweza waweze kufika kwa haraka. Wizara yangu itashirikiana na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na Idara ya Leseni na Jumuiya za wenye Daladala na wenye magari ili kuzungumza nao jambo hilo liweze kutekelezeka.

Kuhusu taa za barabarani kutokuwaka miji ya Pemba; Chake Chake, Wete na Mkoani. Mhe. Hassan Hamad Omar serikali imeshafanya mazungumzo na Serikali ya China na kuahidiwa mradi huo kutekelezwa katika awamu ya pili ya mradi wa taa za *solar* mijini kupitia kampuni ya *ZTD*. Hata hivyo, kupitia njia mbadala, Baraza la Mji Chake Chake likisubiria mradi huo limeanza kuweka taa za barabarani kwa baadhi ya maeneo ya Mji wa Chake Chake.

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe tatizo la giza na umuhimu wa kuwepo mwanga kwa ajili ya usalama wa wananchi wetu na mali zao, serikali inatambua. Lakini kama mnavyojua kinachotukwaza ni unyonge, unyonge wa hizi Halmashauri kwa sababu tutambue kwamba gharama hizi hazibebwi na Shirika la Umeme, gharama hizi ni za kwetu sisi wenyewe kama Mabaraza ya Miji na Halmashauri za wilaya. Kwa hivyo, tukiona tunahangaika kutafuta wahisani basi ni pale ambapo sisi wenyewe hatuna uwezo. Hata hivyo, taarifa hii nadhani itosheleze kuweza kuwapa ahadi Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Naibu Spika, sasa niingie katika kiwanja nambari 226 kilichopo Wete, Pemba. Mhe Farida Amour Mohammed na Mhe. Asha Bakari Makame na wengine ambao wamechangia. Nataka niseme kwamba yako mambo ambayo yalifanyika na Uongozi wa zamani, bahati mbaya sijui niseme mbaya au nzuri, bahati nzuri wote wameshatangulia mbele ya haki, kidini lazima niseme hivyo siwezi kusema bahati mbaya ni bahati nzuri. Lakini nini kilichotokea, kilichotokea ni kwamba kiwanja hiki kina umiliki wa Baraza la Mji la Wete na tunayo hati. Lakini kingine kilichofanyika kuna hati ambayo tuna mashaka nayo na ambayo imetolewa tena na Taasisi hii ya Ardhi kwa huyu mtu, hati hii kwanza tuna mashaka nayo, sio utaratibu wa kawaida kiwanja kimoja kuwa na hati mbili, kwa hiyo la kwanza ni hilo; tutashirikiana na Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwanza kubaini ukweli.

Katika kufanya ujanja hakulishitaki Baraza la Mji aliwashitaki wafanyabiashara walioruhusiwa kujenga maeneo ya biashara kwa ombi la Mhe. Dr. Omar Ali Juma, (marehemu) na wafanyabiashara hao wanapata riziki kupitia maeneo yale, akaenda akawashitaki wao kwa kuvamia kiwanja anachokidai chake. Hakutushitaki sisi Baraza la Mji, kwa sababu angetushitaki na sisi tungekwenda na vielelezo vyetu. Sasa jambo hili limekwenda Mahkamani na kwa sababu wale wafanyabiashara hawana hati wao walipewa hati za muda za kujenga vibanda vya biashara tu, inaonekana Mahakama ilimpa haki huyu na mambo mengine ambayo Waheshimiwa Wajumbe wameniarifu.

Mhe. Naibu Spika, lakini sisi hatua ya mwanzo ambayo tutaifanya kwanza ni hilo la kukaa na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kujua uhalali wa umiliki wa eneo lile, wizara itatuthibitishia.

Jengine ambalo tutalifanya pindi Mkuu wa Mkoa na Wajumbe wa Baraza la Mji watakaporudi hatukumpa kibali cha uzungushaji wa uzio katika eneo lile, tutavunja hapo ndio pa kuanzia. Uzio ule tutauvunja kwa sababu sisi hatukutoa kibali cha kuzungusha uzio ule, kwa sababu hata kama una hati ya matumizi ya ardhi unatakiwa uombe kibali sasa

cha ujenzi, sisi Baraza la Mji hatujatoa kibali. Kwa hiyo, kujenga uzio amevunja sheria, na kama amevunja sheria hatuna haja ya sisi kwenda Mahakamani, sisi tutavunja kwa sababu yeye ndio amevunja sheria. Baya zaidi kwa ushahidi tulionao, nalo hili tutawasiliana na wenzetu wa Wizara ya Mambo ya Ndani, maana ametuchokoza sasa na sisi tutamtafuta.

Permit ya kuishi Zanzibar mara ya mwisho amepewa mwaka 2006. Kwa hivyo, tuna mashaka na utaratibu aliotumia wa kumilikishwa matumizi ya ardhi, ametutafuta, ametuchokoza sasa na sisi tutamtafuta, hawezi kuja mtu ndani ya nchi yetu akawanyanyasa wananchi tukavumilia.

Mhe. Naibu Spika, sisi hatuna mamlaka ya kuondosha amri ya Mahakama, lakini na sisi tuna taratibu zetu za nchi. Kwa hiyo, hili nalo nataka niishie hapo kulizungumza hivyo, hivyo ndivyo muono wetu, na sisi tumeanza kulifuatilia na wananchi wasiwe na wasiwasi kama kuna haki yao haki hii wataipata.

Mhe. Naibu Spika, suala la mapato yanayokusanywa na Halmashauri nishalieleza. Nadhani kwa kuokoa muda naomba hili niliache. Waheshimiwa waridhike na yale majibu ambayo nimeyatoa mwanzo.

Baraza la Manispaa na Mradi wa *ZUSP*. Mradi huu nataka nikubaliane na Waheshimiwa Wajumbe kwamba ni wa muda mrefu; huu mradi unaratibiwa na Wizara ya Fedha. Kwa hiyo, tulichoamua sisi serikalini kupitia wizara yangu kwamba tukae na Wizara ya Fedha, viongozi wa serikali na viongozi wa Wizara ya Fedha na Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ tukae pamoja, maana masuala makubwa naulizwa mimi haulizwi Waziri wa Fedha.

Sasa nataka niwahakikishie; mazungumzo kati ya wizara hizi mbili kujua hatima ya mradi huu yatafanyika kabla ya tarehe 13 mwezi huu. Pahala yatakapofanyika sikwambiini, lakini yatafanyika na yatasimamiwa na Mkuu wetu sote ili kupata uelewa mpana zaidi, lakini mradi ulipofikia ni pazuri sana na wala hakuna mradi uliofutwa katika kujengwa, mradi wa Mhe. Salmin Awadh Salmin mnadhimu wangu upo, mradi wa Mhe. Hamza Hassan Juma upo, mradi wa Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa upo, mradi wa Mhe. Ismail Jussa Ladhu wa kuwatetea wananchi wa Mji Mkongwe upo na Waheshimiwa wengine. Hii inahusu zaidi mradi huu wa michirizi ya maji machafu.

Nataka niwahakikishie Wajumbe, sisi Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha tutafuta makosa ya zamani kuwapata wakandarasi wasio na uwezo kujenga michirizi.

Mhe. Naibu Spika, liko suala moja la Mhe. Jaku Hashim Ayoub amenambia mimi ni rafiki yake, kweli ni rafiki yake, ndugu yake hasa, lakini atakuwa mgumu kwenye msingi wa Gongoni. Tatizo lilioko pale ni kumuajiri mkandarasi mbovu ambaye amejenga chini ya kiwango ambacho kinasababisha yale matatizo aliyoyasema Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Sasa niache hapo nirudi kwenye *ZUSP*.

Kwa hiyo, nataka niwahakikishie kwamba mradi huu wa mitaro ya maji machafu utajengwa. Tunatarajia hivi punde tutapata *no objection* kutoka *World Bank* ili sasa tuweze kutangaza *tender* za ujenzi kwa ajili ya ujenzi wa hii michirizi. Mnaweza kusema ah, kweli pesa tumekopa sisi lakini kwa nini *World Bank*? Nasema yako mengine ndio hayo tunayotaka tukazungumze kwa pamoja ili kubaini undani wa masuala haya ili tuweze kutatua. Lakini mradi huu una maeneo mengi kama walivyosema Waheshimiwa Wajumbe, kuna *component* hiyo ya ujenzi wa michirizi, *capacity building* ya watumishi wa Baraza la Manispaa, ukarabati wa Ofisi ya Baraza la Manispaa, ununuzi wa vifaa na zana za Baraza la Manispaa kwa ajili ya usafishaji pamoja na ujenzi huu na mambo mengine.

Kwa nini mji mchafu wakati magari yapo na vikapu vipo? Katika ununuzi wa vifaa vyote vile kulitokea *delay* na *LC* ika-*expire*, sisemi hili kwa sababu namrushia mwenzangu paka wa uso, sisi sio tunaotoa hizo zabuni, tulichelewa kubaini kwamba kuna tatizo hilo.

Sisi kazi yetu ni kupokea tu, ikafika pahala *LC* ya ununuzi wa magari matano ya kunyanyulia vikapu na gari moja la kunyonyea maji machafu, jumla magari sita ika-*expire* ikabidi ufanyike utaratibu mwengine wa kumpata *supplier* ili aweze kuleta magari hayo, magari hayo tunatarajia kuyapokea mwezi wa Julai na Agosti magari sita yaliyobakia.

Vile vile nataka nijibu suala la Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwa nini vikapu vimebiruliwa? Kwa sababu gari liliopo la kunyanyulia vikapu ni moja tena bovu, kwa hivyo taka zinaweza zikakaa wiki nzima hazijaja kuchukuliwa.

Tuliamua vikapu vile tuvibirue ili kila siku tuhakikishe taka tunazizoa kwa njia ya *manual* badala ya kunyanyua kwa gari lile. Kwa hiyo, ni njia ya *temporary;* tumeamua tufanye vile kwa sababu wafanyakazi waliopo katika majaa yale hawawezi kulinyanyua na kulipakia kwenye gari, kwa hiyo tuliamua tufunike.

Vile vile kwa wakati huu wa mvua tuliona likiwa juu na taka wananchi watakwenda kutia litajaa maji na taka, sasa hata wale wafanyakazi wa Baraza la Manispaa, na kwa kuwa tuna ukosefu wa vifaa vya kuwapa wafanyakazi wa Baraza la Manispaa kutokana na uwezo wetu, hivyo tukaona ile ni njia itakayoturahisishia kuziondosha taka kwa njia nyepesi.

Kwa hivyo, sababu zilizopelekea harakati za usafi zisite ni kukosekana kwa gari la kunyanyulia vikapu. Ziko na sababu nyengine ambazo nikizizungumza hapa nadhani zitachukua muda mrefu zaidi.

Wafanyakazi wazee wasioweza kufanya kazi lakini wafanyakazi pia wanaofanya kazi kwa mazowea. Hilo nalo lina utaratibu wake, tumeshaandaa utaratibu wa kuweza kulisawazisha ili tuweze kukabiliana na tatizo hilo. Sasa mara tu baada ya gari za kunyanyulia vikapu zitakapofika, basi nadhani Waheshimiwa Wajumbe pamoja na ule ushauri uliotolewa na Waheshimiwa wengine tuwahimize wananchi wetu, na sisi sote tuwe na tabia ya kuwa wasafi. Hapa nataka nimpongeze sana Mhe. Ali Mzee Ali kwa kuweka mazingira ya nyumba yake safi. Kama sote tungekuwa kama Mhe. Ali Mzee Ali nadhani lisingetupa tabu.

Jengine kama mnakumbuka Mji Mkongwe matoroli yale yalikuwa yanapita chini ya milango kuchukua taka na utaratibu ule sasa haupo, kwa nini haupo? Kuna taka za aina nyingi; taka unatakiwa uzitenganishe taka za maji maji mbali, taka nyengine za maganda mbali na taka za chupachupa mbali, lakini taka zote tunazichanganya pamoja. Kwa sababu utamaduni ule wa mtu kuchukua taka zake akaziweka kwenye *dust bin* haupo, ambao tunaahidi tunataka tuurejeshe, watu wote sasa wanakwenda kutupa taka katika majaa, wanapotupa taka katika majaa tatizo linakuwa kubwa zaidi.

Sasa nataka niseme kwa sababu ya hayo maboresho ya Baraza la Mji, tutahakikisha mambo haya tunayasimamia kwa ukamilifu wake ili kuondokana na tatizo hili. Mimi sitaki niseme kwamba mji ni msafi, mimi nataka nikiri kwamba mji ni mchafu, lakini kama mji mchafu nataka niungane na wale waliosema si Baraza la Mji peke yao, na sisi wananchi pia tubadilike. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, tunaoishi Michenzani tuangalie ngazi zile, kule nako pia tunataka Baraza la Mji. Tunaoishi kwenye majumba makubwa, majumba makubwa ya Mji Mkongwe. Zamani nyumba moja yenye chumba kimoja na ukumbi mkubwa anakaa mtu na watoto wake wawili, siku hizi sehemu kama hiyo wanakaa watu 10. Taka zinaongezeka, uzalishaji wa taka umeongezeka ndani ya mji wetu, tunakotupa taka mbali.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa bado dakika 10 nakuongeza hizo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, nitakuomba uje unilinde na mabuti maana mengine nisipoyasema watakuja kuniuliza. Kwamba mimi majibu yote ninayo, lakini kama bado dakika 10 sitaweza kuyajibu yale yote ambayo nimeulizwa na Waheshimiwa Wajumbe. Kwa hiyo waelewe Waheshimiwa Wajumbe kwamba ninayo majibu mengi.

Mhe. Hamza Hassan Juma nadhani maeneo yako mengi nimeyajibu. Kuna suala limezungumzwa na Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Ismail Jussa Ladhu na Mhe. Panya Ali Abdalla kuhusu suala la bustani ndani ya mji wetu.

Ni kweli uongozi uliopita ulianza hii kazi lakini Kamati Teule ilitushauri, na baadhi ya mambo yale ambayo yamo ndani ya Kamati Teule tusingependa kuyarejea. Kwa hiyo katika bajeti hii ya mwaka huu tuna azma ya kuimarisha zile bustani ambazo wenzetu wamezianzisha, na hivi sasa tumempeleka mtaalamu wetu mmoja Moshi kwa ajili ya kuchukua mafunzo kwenye ngazi ya diploma ili aje atusaidie katika shughuli hizi za bustani. Na hatusemi kwamba mpaka arudi ndio tuanze, tutaendeleza pale ambapo wenzetu walianza kwa kutumia bajeti yetu, kwani kama tunavyojua bajeti ya sasa ni ndogo mno katika eneo hili, lakini tutashughulika pia pamoja na kukemea vitendo vya wale wanaozivuruga bustani.

Taa za usalama barabarani kutofanya kazi kwa kipindi kirefu amezungumzia Mhe. Hamza Hassan Juma. Mhe. Naibu Spika, taa za zamani za kuongozea magari *(traffic lights)* hivi sasa zimeondoshwa kupitisha uwekaji wa taa

mpya. Tuna mpango wa kuweka taa mpya za *traffic lights* katika maeneo tofauti, na ndio maana mtaona hivi sasa kunachimbwa chimbwa mashimo. Kwa kushirikiana na wenzetu wa Miundombinu na Mawasiliano taa hizi zitarejeshwa.

Hali ya barabara za mji kuwa na mchanga mwingi yaani michafu. Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Ali Salum Haji, Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa, Mhe. Abdalla Juma Abdalla na Mhe. Mgeni Hassan Juma; wote walichangia eneo hili. Tunachosema ni kwamba kama nilivyosema wafanyakazi hawa wengi utawaona hoi bin taaban. Tunataka kufanya marekebisho ya kuwaondoa wale wasioweza kazi. Tutafuata taratibu za kisheria tuwa- *phase out* ili tuwaajiri vijana wenye uwezo wa kuweza kufanya kazi hiyo.

Sasa Waheshimiwa Wajumbe mnielewe tutakapoanza kutekeleza jambo hili, msije tena mkanambia nina mtu wangu muache, kwa sababu hawa wengi wao wameshindwa kazi. Nikikupeni *list* ya wafanyakazi waliomo kwa idadi basi mtathibitisha kwamba hawa wengi wao hawana uwezo wa kufanya kazi; wamechoka. Tunafuata taratibu za kisheria ili tuone tunawa-*phase out* vipi na kuajiri watu wapya watakaoweza kufanya kazi hii. Vyenginevyo kila bajeti hapa mtakuja kunikaa na roho, kama mimi Waziri ningekuwa naruhusika kwenda kuzoa hiyo michanga basi ningekwenda mwenyewe, lakini *protocol* hainiruhusu isipokuwa kwa *operation* maalum. Sasa tatizo tulilonalo ni hilo, lakini nakiri pia kwamba na *supervision* nayo ina matatizo yake, inataka kurekebishwa. Tabia yangu mimi maji huita maji, siwezi kuita soda.

Jengine ambalo limezungumzwa na Mhe. Hamza Hassan Juma jengo la Amani linalotumiwa na Baraza la Manispaa. Mnakumbuka kwamba katika programu ya mradi huu wa *ZUSP* ni pamoja na ukarabati wa jengo la Baraza la Manispaa.

Hapo mwanzo Baraza la Manispaa lilikuwa limedhamiria likihama pale liende *Victoria Garden* waende wakafanyie kazi pale kwa muda, lakini yakaja maamuzi ya Serikali kwa ufinyu wa ofisi za Serikali watu wetu wa taasisi ya Mamlaka ya Rushwa hawakuwa na ofisi, ikabidi Serikali ifanye maamuzi ya kuwapeleka watu wa Rushwa pale *Victoria Garden*. Na kama lilivyozungumziwa lile suala la maslahi ya vikosi na Mhe. Hamza sijui Mheshimiwa gani, na hili nataka nikiri ni mimi mwenyewe niliyekuwa nikiwahimiza Manispaa watukabidhi ufunguo, wakati ule mimi ni Waziri wa Utumishi na Utawala Bora.

Sasa bahati nzuri wanakabidhi Utumishi na mabadiliko ya Wizara yamefanyika, jambo la kwanza ninalikuta kwenye deski langu ni matatizo ya ofisi ya Baraza la Manispaa. Tukaanza kuomba Serikalini, Serikalini tukashindwa hakuna. Tukaanza kwenda kwenye majengo mbali mbali ya watu binafsi bei wanataka kwa *square meter*, kukodi tukashindwa.

Sasa ni kweli jambo hili halikuwepo katika mpango toka mwanzo ambao mpango huo ungeweza kupitishwa na Madiwani kwa sababu hatukuwa na mpango wa kukodi jengo. Lakini baada ya mazingira hayo ikalazimika ifanye jambo la dharura, jambo la dharura hili lilipofanywa ikabidi taarifa ipelekwe kwenye Baraza la Madiwani kwamba hali imefikia hivi. Ikabidi Manispaa wakodi jengo kwa mkataba ambao pia umezingatia masharti ya Kamati Teule. Wamekodi jengo, amesaini Mkurugenzi na amesaini Mstahiki Meya wa Baraza la Manispaa. Na kwa sababu muda wa kuwakabidhi *World Bank* jengo lile la Manispaa ulikuwa umeshafika, ilibidi ufanyike utaratibu ule kulipata hili jengo ili Manispaa waweze kuhamia. Sasa inawezekana kukawa kuna mambo mengine yakawa hayakukaa sawa, lakini hayo yametokana na udharura wa lile jambo lenyewe lilivyokuwa.

Malipo ya wafanyakazi na mishahara yao. Ni kweli wafanyakazi wa Manispaa bado hawalipwi kiwango cha chini cha wafanyakazi wa Serikali, nakiri. Na hili kwa ufupi niseme Serikali ilishatoa maelekezo. Tutashirikiana na wenzetu wa Wizara ya Fedha waweze kutusaidia hili jambo liweze kulipika. Ikifika mwezi wa Julai kutakuwa na malimbikizo ya watumishi yasiyopungua milioni 200 na zaidi kupewa *arrears* zao, ili waweze kupata sawa na wenzao wa Serikalini.

Na hii inatokana na ule mfumo kwamba Serikali inatupa *100 million* kwa ajili ya ruzuku ya mishahara, lakini na kinachokusanywa Baraza la Mji kinachangia milioni 65, kinachobaki kidogo ndio kinafanyia kazi za *OC*.

Sasa hili Serikali imeshaliamua naomba niwahakikishie Waheshimiwa, wafanyakazi wa Baraza la Manispaa kwamba haki zao watazipata. Na *inshaallah* kuanzia mwezi wa Julai wafanyakazi hawa Serikali imekubali waingie

kwenye *payroll* ya Serikali, na kile kinachokusanywa na Baraza la Manispaa chote kifanye kazi ya kuuhudumia mji. Mji uwe safi, magari yatengenezwe na huduma nyengine za wananchi ziweze kupatikana.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa dakika 10 zimekwisha ungemalizia. Mengine utajibu Waheshimiwa kama hawakuridhika.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, la mwisho naomba nilijibu kwa umuhimu wake linalohusu kituo cha daladala kilichopo Kisiwandui. Hili jambo limezungumzwa karibu na Waheshimiwa wengi, lakini kama nilivyojibu swali la nyongeza juzi kwamba kituo kile hakikuidhinishwa. Na sisi kama sekta husika tulikaa na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ambao wao ndio wanatoa leseni za madereva, na wao ndio wanaopanga zamu za magari haya ya abiria. Tukakaa na Kamati ya Usalama Barabarani, tukakaa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, tukakaa na Kamati ya Ulinzi na Usalama.

Na yalipangwa maeneo maalum ya magari haya, yanaposhusha kabla zamu yake ya kuzunguka mjini haijafika aende akakae, lakini baadhi ya madereva hawa wanakaidi jambo hili. Narejea tena kusema kwamba kituo kile ni sawasawa na vituo vyengine; washushe wapakie na gari iondoke.

Na katika mji huu yapo maeneo mengi kama hayo gari zinapita zinachukua, wanapakia, wanashusha lakini hapaonekani msongamano huo. Na bahati mbaya jambo hili kuna baadhi ya mambo mengine tumeyazungumza Serikalini, *traffic* saa nyengine wanapochukua hatua ya madereva wanapofika Mahkamani kesi hazipokelewi. Lakini hili tumeshakaa na Wizara husika tumelizungumza. Wala hatukukurupuka, lazima niseme kweli. Kituo cha kudumu hakijawekwa na hiyo inatokana na kwamba tunasubiri mipango miji ituelekeze tukiweke wapi. Lakini vituo vya muda tuliviweka katika maeneo mbali mbali.

Hata hivyo, Ofisi ya Mkoa wa Mjini Magharibi kwa kupitia Bodi ya Usalama Barabarani kwa kushirikiana na sisi tumeshakaa kuona nini cha kufanya. Lakini na Wizara yangu kupitia Baraza la Manispaa kuanzia kesho kituo kile wanapoegesha magari, yaani watu wanaoendesha magari kinyume na utaratibu tutafanya jitihada zote tukiondoshe ili tuondoshe usumbufu kwa wananchi wetu.

Maelezo ambayo yameelezwa na Waheshimiwa Wajumbe wengine wamekaribia kulia najua. Mhe. Ismail Jussa Ladhu yeye anapata tabu zaidi pale kwa sababu ya ghasia zilizopo. Lakini nataka nimhakikishie Mhe. Jussa kwamba kile kituo kesho asubuhi ukiamka utakikuta hasimami mtu pale. Ni kwamba tunasikia, na hili nitalifanyia kazi kwa nguvu zote.

Limetoka wazo kwa nini tusizipeleke zile gari Mnazi Mmoja. Sisi kazi yetu maeneo haya ya wazi, tutawasiliana na wenzetu pia kama tulivyowasiliana nao mwanzo watu wa Ardhi tuone kama kuna *possibility* ya kuweza kulitumia eneo lile.

Limekuja suala kwa nini eneo la Darajani sasa limekuwa *parking* na tumeondosha *stand.* Ni Baraza hili hili wakati wa kuniuliza maswali na majibu tulipata kushauriwa kwamba kwa nini badala ya lile eneo kukaa bure lisitengenezwe *parking* kwa watu wanaokuja sokoni. Na Baraza lika-*act* ushauri wa Baraza la Wawakilishi. Sasa mimi nadhani lililofanya tuondoshe stendi ya Darajani ndilo lile lile litakalotufanya tuondoshe wanaoegesha magari kinyume na utaratibu Kisiwandui kesho.

Mhe. Naibu Spika, mengine ambayo yamezungumzwa kama ulivyokwisha kunisihi naomba nisiyatolee ufafanuzi kwa sababu ni mengi mno.

Mwisho kabisa nataka niendelee kuna suala limezungumzwa na nitakuwa mkosefu wa fadhila kama sikuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa maoni yao ya kuwatakia mema askari wetu wa Vikosi vya SMZ. Hili limezungumzwa na Waheshimiwa wote wa pande zote, na mimi ni imani yangu wote wana nia ya kuona kwamba kama wakati huo walikuwa wakiwazungumza vibaya pengine kulikuwa na mambo ambayo walikuwa wanayaona kwa maoni yao si mazuri, lakini kwa sasa wanaona kwamba hawa watu wanafanya kazi vizuri.

Kwa hiyo mimi nataka nikushukuruni nyote, nia ile ambayo nilianza nayo, maana mimi mwenyewe nimepita kambi, hadi kituo, hakuna sehemu ya kikosi ambayo sijenda na hakuna askari ambaye sijaonana nae.

Kwa hiyo nyinyi kama Wawakilishi wa wananchi mmeelezwa, nashukuru mmeelezwa yale niliyoelezwa mimi. Na ndio maana kwenye bajeti hii tunayokwenda nayo Serikali iliamua kuwaongezea *increment* 10 askari wanaomaliza mafunzo leo tofauti na wafanyakazi wengine wa kawaida. Lakini na kuwaongezea posho ya *ration allowance* kwa *100%* ya posho ambalo walikuwa wanalipata pale. Mambo ya *risk allowance*, pamoja na maslahi mengine ya makaazi.

Mhe. Rais juzi alipokuwa anatoa kamisheni kwa maafisa aliahidi pale Kama kwamba atahakikisha anawajengea maslahi mazuri askari wa vikosi vyetu vya SMZ. Sasa nadhani jambo akisha kulisema Rais mimi sitakiwi nilitie mikono, tusubiri ahadi ya Rais aitekeleze na matokeo yake mtayaona.

Nakiri kwamba wana makaazi duni. Wizara yangu imeanza juhudi ya kuzungumza na makampuni yanayotaka kuingia mkataba na Serikali kwa njia hiyo hiyo ya *PPP* au *BOT* ili tuweze kuwajengea makaazi bora. Sio makaazi tu ya kuishi na familia zao, lakini hata yale mabweni wanayoishi katika kambi zao, nataka nikiri kwamba yana mapungufu. Suala la zana tumeanza tulivyokuwa kabla ya Agosti sivyo tulivyo sasa.

Na mimi hata lile alilolisema Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, nataka nikuarifu kwamba kwenda kuwatembelea askari kwa malalamiko madogo madogo kama ya chakula, hiyo kazi nimekwishaifanya. Askari wenyewe wamepangwa sasa kujiundia uongozi wa kupanga *menu* ya chakula ambacho watakula makambini mule mwahala walipo, hasa Kikosi cha Valantia ambapo amekisema.

Valantia sasa hivi wapo kambini, na kwa sababu utaratibu wa Valantia ni sawa sawa na utaratibu wa jeshi. Katika kipindi cha miaka miwili lazima wawepo kambini kwa ajili ya kingo. Sasa utaratibu wao wale wakiwa kambini wanalishwa kupitia zile pesa za *ration allowance* ambazo wanalipwa. Jeshi wanafanya hivyo na wao wanafanya hivyo, na huu ni utaratibu wa kimataifa. Pale serikali inapokuwa na uwezo mkubwa sana basi mazingira haya yanazingatiwa. (*Makofi*).

Suala la uongozi Mhe. Mshimba, Kamanda alikuwa Mkuu wa Utawala. Rais ameamua kumpandisha cheo. Mchakato unaendelea wa kumtafuta mkuu wa utawala mwengine, hivi karibuni tutamtangaza mkuu wa utawala na kule wanakokaimu watatangazwa wengine ili uongozi katika vikosi uweze kufanya kazi vizuri.

Suala la Mhasibu nilipotembelea tumekubaliana kwamba wale vijana ambao...

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa malizia.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Ahsante sana ninamalizia hili.

Wale vijana ambao wamepata ujuzi wa kufanya kazi za uhasibu wafanyakazi katika vikosi vyao, na wale walioazimwa warudi kwenye vikosi ambavyo wameazimwa.

Mwisho kabisa Mhe. Naibu Spika, baada ya kwisha kusema hayo, naomba niseme kwamba yale ambayo sikupata kuyajibu kutokana na muda, rundo hili ni kubwa ningeweza kuyajibu yote lakini muda hautoshi. Naomba kutoa hoja.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri kwa majumuisho yako. Waheshimiwa hoja iamuliwe. Kwa hivyo sasa niwahoji. Wale waliokubali hotuba ya Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2014/2015 wanyooshe mikono, waliokataa. Waliokubali wameshinda. (*Makofi*).

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya wizara yangu, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya wizara yangu. Naomba kutoa hoja.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU 17 - JESHI LA KUJENGA UCHUMI

Kifungu 0201 Utawala Unguja	Shs.25,000,000.00
Jumla ya Fungu	**Shs.25,000,000.00**

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 18 - CHUO CHA MAFUNZO

Kifungu 0201 Idara ya Vituo vya Mafunzo	Shs.41,000,000.00
Jumla ya Fungu	**Shs.41,000,000.00**

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 29 - KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO

Kifungu 0201 Idara ya Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo	Shs.15,830,000.00
Jumla ya Fungu	**Shs.15,830,000.00**

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 32 - KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI

Kifungu 0201 Utawala Unguja	Shs.10,000,000.00
Jumla ya Fungu	**Shs.10,000,000.00**

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 34 - KIKOSI CHA VALANTIA

Kifungu 0201 Kikosi cha Valantia	Shs.7,000,000.00
Jumla ya Fungu	**Shs.7,000,000.00**

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 37 - MKOA WA MJINI/MAGHARIBI

Kifungu 0401 Mkoa wa Mjini/Magharibi	Shs.20,000,000.00
Jumla ya Fungu	**Shs.20,000,000.00**

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 43 - OFISI YA USAJILI NA KADI ZA UTAMBULISHO

Kifungu 0201 Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho	Shs.1, 500,000.00
Kifungu 0301 Ofisi Kuu Pemba	Shs.1,000,000.00
Jumla ya Fungu	**Shs.2,500,000.00**

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 09 TAWALA ZA MIKOA NA IDARA MAALUM ZA SMZ

Kifungu 0201 Idara ya Utawala na Raslimali Watu Shs.1, 135,796,000.00
Kifungu 0301 Ofisi Kuu Pemba

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake ya kina ambayo ameyatoa kwenye michangio ya Wajumbe wengi sana ingawa hakunifika mimi, lakini ninaamini angenijibu nikaridhika.

Mhe. Mwenyekiti, na kwa sababu hiyo nilipohoji kwenye Ofisi Kuu Pemba, nilihoji maamuzi ya Afisa Mdhamini kuamua kuwapeleka watendaji wa Halmashauri za Pemba Tanga, wakati bajeti za Halmashauri hazikuelekeza hivyo. Kwa nini hawakuamua maamuzi ya Mabaraza ya Halmashauri Pemba hayakuwa na bajeti ya ziara ya Tanga lakini Afisa Mdhamini akawachukua watendaji kwenda Tanga, na walitumia zaidi ya milioni nane hadi kumi. Naomba maelezo hayo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nikubaliane na ndugu yangu Mhe. Hija Hassan Hija kwamba sikumfika katika kutoa maelezo yanayohusu masuala ambayo ameniuliza, nayo yanahusu juu ya suala la Afisa Mdhamini kuwapangia watendaji wa Halmashauri na Mabaraza Pemba kwenda katika ziara kikazi Tanga. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka niseme kwamba Mabaraza ya Miji na Halmashauri wanacho kifungu cha safari za kikazi, iwe Dar es Salaam iwe Tanga, iwe Ulaya au iwe pahala pengine.

Afisa Mdhamini alichokifanya ni kuratibu ile ziara yenyewe, kwa sababu inaonekana ni ziara ambayo huwa inafanyika kila mwaka. Halmashauri zote inacho kifungu hicho. Inawezekana kwamba kifungu hicho kikawa kimetumika kama yale maelezo ambayo niliyatoa pale, kwamba baada ya kwishakuona makusanyo yamefanyika yakatumika kabla ya kufuata utaratibu.

Afisa Mdhamini kaenda Tanga kwa kutumia kifungu chake cha ofisi yake na wala sio cha Mabaraza wala cha Halmashauri. Sasa mimi ningeomba tu Mhe. Hija Hassan Hija akubali tu kwamba kifungu cha safari za kikazi kilikuwepo. Sasa suala la kupanga ni kuchagua. Mimi ninaelewa kwamba *concern* yake kwamba pengine pesa hizi ambazo wamezitumia wangeweza kuzitumia kwenye shughuli nyengine za maendeleo kama alivyosema, lakini kifungu kilikuwepo.

Sasa naomba Mhe. Mwenyekiti, akubali kwamba kifungu cha safari za kikazi kilikuwepo na walikitumia kifungu hicho kwa ajili ya kwenda kwenye ziara ya kujifunza jinsi gani wenzetu wanavyotekeleza miradi ya wananchi ile ambayo inachangiwa na Halmashauri. Ndio safari ambayo ilifanyika huko Tanga.

Ahsante sana.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nimejaribu kuangalia bajeti ya Ofisi Kuu Pemba. Mwaka jana hakuna safari za kifungu cha safari za nje, kuna safari za ndani milioni 15, mwaka huu milioni 20. Lakini kama katumia fungu hilo, hoja yangu ni kwamba fedha zilizotumika ni fedha za Ofisi za Halmashauri za Pemba ambapo ili fedha zitumike Mabaraza ya Halmashauri hizo lazima yaidhinishe.

Mimi nimefanya utafiti Pemba wote hakuna idhini ya Mabaraza yote na Miji ya Pemba kwamba Afisa Mdhamini aondoke na watendaji kwenda Tanga. Sasa aniambie kwa nini asitumie fungu la milioni 15 ofisi yake na akaagiza Mabaraza yagharamie safari wakati hakuna maamuzi ya Mabaraza, hakuna bajeti iliyotengwa. Fedha alipata wapi ndio hoja yangu.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa kaeleza labda kama hukuridhika arejee tena. Mheshimiwa muongezee majibu ya ziada.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, ninachotaka kusema kwamba Afisa Mdhamini yeye hastahiki kutumia fedha za Mabaraza na Halmashauri, ametumia vifungu vya ofisi yake kwenda hiyo safari kufuatana na Makatibu wa Halmashauri.

Afisi za Halmashauri zina vifungu vya safari za kikazi kwenye vifungu vyao vya Halmashauri. Na bajeti hiyo itakuwa imepitishwa na Baraza mwanzoni mwa mwaka. Suala hapa linaloonekana, kwa sababu sisi hapa tukishapitisha bajeti na ndio maana kuna kamati za ufuatiliaji kwamba vile mulivyotupitishia ndivyo tulivyotumia?

Mimi ninadhani nikishapitishiwa fungu hapa, siji tena Baraza la Wawakilishi nikasema naomba muniruhusu niende safari fulani, ni utaratibu wa kawaida. Kwa hivyo kama Baraza halikuidhinisha, Mabaraza haya hayakuidhinisha, hili ni jambo ambalo linahitaji kufuatiliwa. Naomba nifuatane mimi na yeye, twende tukaangalie nini kilichofanyika. (*Makofi*).

Kama itakuwa hawakuidhinisha bado tunarudi kule kule kama nilivyosema mwanzo kwamba utaratibu utakuwa haukufuatwa. Sasa kama utaratibu haukufuatwa, sasa wa kuchukuliwa hatua za kinidhamu ni hao waliokuwa hawakufuata utaratibu utafanyika na taratibu zipo. Kwa hivyo mimi ninamuomba Ndugu yangu Mhe. Hija Hassan Hija kama hawakushirikishwa Madiwani, hawakuidhinisha hilo siwezi kuliona hapa, ila tutalithibitisha baada ya kwenda kuona.

Lakini ninavyojua mimi matumizi ya mwaka yanaidhinishwa na Baraza la Madiwani. Sasa kama hawakushirikishwa, jambo hilo tutakwenda kuliona pamoja na utafiti alioufanya yeye, ninakubaliana naye kafanya utafiti. Maana asingekuja kusema tu lakini na mimi namuomba anipe muda, huo utafiti twende tukaendelee kuufanya pamoja mimi na yeye.(*Makofi*).

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, anaendelea kunijibu vizuri sana na mimi hiyo ndio hoja yangu kwamba ikiwa Mabaraza hayakuidhinisha, maana yake fedha zile zimetumika nje ya utaratibu wa kisheria. Sasa ninafurahi kwamba Mhe. Waziri kwamba yupo tayari kwenda kufanya utafiti huo pamoja. Naomba anipangie siku twende Pemba mbele ya watendaji wote; Mabaraza manne na miji ya Pemba ili tuone hiyo ruhusa aliipata wapi kwa idhini ya bajeti hii. Mhe. Waziri naomba unipangie siku gani twende.

Mhe. Mwenyekiti: Haya tunaendelea.

Mhe. Hija Hassan Hija: Naomba nijue ni siku gani.

Mhe. Mwenyekiti: Kasema mufuatane mwende.

Mhe. Hija Hassan Hija: Hapana aniambie ni siku gani mbele ya Baraza ili tupate kuripoti.

Mhe. Mwenyekiti: Mbona simfahamu. Mbona sikufahamu?

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, yeye Mhe. Hija Hassan Hija anajua *commitment* ya Mawaziri hapa Barazani. Asubiri tupitishe bajeti, halafu tufanye hayo mambo mengine.

Maana hata sasa hivi hiyo bajeti ya mimi kunipeleka Pemba haipo kama bajeti hii haijapita. (Makofi).

Mhe. Mwenyekiti: Baada ya bajeti.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, mimi ninamuelewa sana Mhe. Waziri lakini jamani hili ni Baraza, *hansard* ikae sawa kwa manufaa ya Wazanzibari. Mawaziri wengi hapa hutwambia keshokutwa halafu anaingia mitini. Sitaki kuhukumu kwa makosa ya Mawaziri wengine lakini angalau angeniambia mwisho wa mwezi huu twende, mimi ningemkumbusha. Lakini ukiniambia tu tusubiri tu bajeti imalizike, kwa kweli ninapata tabu.

Mhe. Mwenyekiti: Nadhani tuendelee, Mheshimiwa kajitahidi.

Mhe. Hija Hassan Hija: Naam!

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa kajitahidi tuendelee.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, sijafahamu.

Mhe. Mwenyekiti: Eeh! baada ya bajeti.

Mhe. Hija Hassan Hija: Baada ya bajeti?

Mhe. Mwenyekiti: Ndio. Baada ya bajeti Mhe. Waziri kakwambia mutakwenda Pemba mukafanye huo utafiti.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, nimesema lugha ya Kiswahili inaeleweka. Mimi kama Waziri inatakiwa *commitment* katika kipindi hichi niwepo Barazani, tukimaliza bajeti nzima mimi nitaondoka tutafuatana tutakwenda. Sio bajeti hii tu, bajeti hii yote tunayopitisha, maana wizara hapa Wajumbe wote wanatuhimiza tufanye kazi kwa pamoja kama serikali. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hija Hassan karidhika tuendelee.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, nilipochangia nilimuuliza Mhe. Waziri kama kule Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni, kuna Kaimu ambaye anamkaimu Katibu wa Halmashauri ya Wilaya, na wakati huo nikamwambia kwamba na yule kijana aliyekwenda kusoma aliyekuwa Katibu wa Halmashauri amesharudi na ameshakuwa na *degree* yupo tu. Sasa kwa bahati mbaya Mhe. Waziri hajanijibu hata neno moja, na nilimuuliza huu ukaimu utaendelea mpaka lini na huyu kijana atakuwa vipi, anakwenda Chake Chake akirudi tu? Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri anipe majibu.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, nakubali kuwa sikuweza kumjibu swali lake, lakini nadhani hao watu wawili wote anaowazungumza kuna nafasi kama mbili za kukaimu. Baada ya kumaliza bajeti yangu kwa sababu jukumu hilo ni la Waziri, nitafanya uteuzi wa kuwateua, sisemi kama waliopo au waliokuwa hawapo, kwa mujibu wa taratibu za kiutumishi nitamtafuta mtu ambaye ana uwezo wa kuweza kufanya kazi za Ukatibu wa Halmashauri. Nitateua kwa mujibu wa mamlaka niliyonayo.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, namsikia sana Mhe. Waziri, lakini namuomba sana na busara zitumike. Maana anasema anaweza akamteua aliyepo au akamteua mwengine. Namuomba sana kama amefanya kazi vizuri asije akasema anateua mwengine, akaja kuwaacha wale ambao wameshafanya kazi na kuchukua watu wengine nje ya wale. Namuomba sana busara zitumike, ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 0301	Ofisi Kuu Pemba	521,061,000

Kifungu 0401

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa ya kuweza kupata ufafanuzi wa maswali kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mhe. Waziri kwa namna alivyokuwa ametujibu hoja zetu pamoja na maswali yetu na pia nashukuru sana suala la *ZUSP;* kwamba limefikia pahala serikali kuu itaingilia kati na tarehe 13 tutaweza kuelewa muelekeo na mustakabali wa suala hili baada ya taasisi husika kukaa kitako na kuweza kulitafutia ufumbuzi suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu ni katika suala zima la daladala ambazo ziko pale Kisiwandui, kama alivyosema Mhe. Waziri, katika majibu ya nyongeza wakati wa maswali na majibu; kwamba lile sio eneo ambalo wametakiwa waweke magari yao kama ni maeneo ya kutulia. Sasa kama sheria ya serikali iko hivyo, kwa nini hadi leo hii magari yanaachwa kuendelea na msongamano katika eneo lile na ikawa bado zile kadhia zinaendelea katika eneo husika.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mhe. Mahmoud na Waheshimiwa wengine nadhani watakuwa wamenielewa; kwamba pale hakuna mtu ambaye ameruhusiwa kisheria, na juhudi ambazo tunazichukua nimeshamwambia. Changamoto ambazo tunapambana nazo nimeshazieleza, kwa sababu hili jambo sio la Manispaa peke yake kama hivyo linavyofikiriwa, linakusanya taasisi nyingi.

Kwa hivyo, ninachowaahidi mimi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba kituo kile kesho asubuhi, na ninawaambia wasikie, mbinu gani nitatumia kuwaondosha nazijua mimi. Nitakiondosha kituo kile kesho asubuhi au nitayaondosha magari yale kesho asubuhi kama nilivyosema pale kwenye hoja.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, majibu ya Mhe. Waziri ni katika lengo la kujenga Zanzibar yetu na kuwasaidia watu ambao wana maumbile maalum ambayo Mwenyezi Mungu amewajaalia. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, hoja hii wamesimama watu wengi. Kwa hivyo, katika *group* hili nimechagua watu watatu, wengine baadaye wataingia kwenye hoja nyengine. Mhe. Ismail Jussa Ladhu na baadaye Mhe. Hamza Hassan Juma, waliobakia tungoje hoja nyengine.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nitakuwa sitendi haki kama sikuanza kwanza kwa kumshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake ya kina na ufafanuzi wake mzuri. Kikawaida ningeridhika, na kwa sababu ni hoja nyingi, lakini kwa sababu ya nafasi finyu, naomba nijikite na hii moja ambayo imeshaanzwa lakini mimi kidogo nimepata wasi wasi na ndio maana nataka ufafanuzi wa Mhe. Waziri.

Hatuwezi kutatua matatizo Mhe. Mwenyekiti, kwa kutumia nguvu. Suala tunalolizungumzia ni hili ambalo liko katika kituo kilichopo maeneo ya Michenzani na mimi nilikizungumzia, lakini katika majibu yake Mhe. Waziri, kwanza kakiri kwamba bado hawajajipanga kuwa kituo cha kudumu cha magari, vilivyokuwepo ni vile ambavyo vinapaswa kupita kuchukua abiria.

Mhe. Mwenyekiti, katika hali ambayo kunakuwa na *vacuum*, wananchi wanafanya kama ambacho kimeonekana pale. Kwa sababu huwezi kuwa na mji wowote duniani Mhe. Mwenyekiti, ukawa hauna kituo kikuu cha magari, sijapata kuona kutembea kwangu kote duniani, kwamba magari yapite tu yachukue abiria; haiwezekani. Kwa hivyo, hata akitumia ubabe akienda kuwahamisha kesho pale, itapelekea usumbufu mwengine, patatokezea zahma pale na itakuwa Baraza la Wawakilishi inayotumika sasa kuhalalisha kwamba tumetoa agizo lile.

Mhe. Mwenyekiti, suala ni kwamba lazima kwanza serikali ijipange, ndio tukasema mmekurupuka. Ni kwamba hicho kituo kikuu kipatikane, kama hakipo hicho Mhe. Mwenyekiti, hii hamisha hamisha kila siku itakuwa inaendelea, tutaendelea kulitia ubaya jina la serikali yetu mbele ya wananchi; kwa sababu kama ilivyotokezea kulaumiwa kwa Darajani, tutalaumiwa sisi kwa pale.

Kwa hivyo, nilikuwa nadhani jawabu la kusema tu kwamba kesho kituo kiondoke hapana, ni kwamba tupate jawabu kuwa kituo kikuu na mipango itakuwa vipi Mhe. Mwenyekiti. Naogopa tusijekuwa tunafanya maamuzi hapa tukaonekana kuwa tumeamua kama ilivyoamuliwa Darajani; kwamba limeondoka. Lakini utaratibu wa wananchi utapatikana vipi, kwa sababu kile kituo cha kupita na kuondoka Mhe. Mwenyekiti, ndio kinachopelekea usumbufu kwa wananchi, wanafunzi kukimbilia daladala, kwa sababu hakuna kituo maalum cha kusimama pale, daladala ikifika wanafunzi wanakimbilia kutaka kuwahi kuingia kabla haijasimama vizuri.

Serikali itujibu jibu la makini kwamba utaratibu wa kupata kituo cha kudumu uko wapi. Mimi sishauri pamoja na kwamba nakaa eneo lile, sishauri kwamba kiondoshwe kabla ya kupatikana ufumbuzi huu. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti kama ni hivyo tutakuwa tunatatua tatizo moja halafu tunakwenda kutayarisha matatizo mengine. Tupate jawabu la kina juu ya suala hili Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kama alivyosema Mhe. Ismail Jussa apate jibu la makini. Jawabu la makini ni kwamba ili tupate kituo cha kudumu ndani ya mji wetu ni lazima tusubiri *master plan* mpya ya Mji wa Zanzibar. Hiyo ndiyo itakayotupa ufumbuzi wa kupata kituo cha kudumu cha stendi ya magari yanayoingia ndani ya mji huu. Kwa hivi sasa serikali ilichoamua ni kuweka vituo vya muda vya kuegesha magari ambayo yanaingia ndani ya mji huu. Vituo hivyo kimoja kipo Kibandamaiti, kingine kipo Kwabinti Amrani, Kinazini na maeneo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, maeneo hayo serikali iliyafanya kwa kukaa na taasisi zote zinazohusika. Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa maana ya Idara ya Leseni, Jumuiya ya wenye daladala, na wamiliki wa magari, Kamati ya usalama barabarani na watu wa mipango miji.

Tukakubaliana kwamba kwa sababu kuna mpango mzima wa *master plan* mpya ya mji wa Zanzibar, tuweke vituo vya kuegesha magari katika maeneo tofauti na humu ndani ya mji zije gari zishushe watu na wala hakuna gari iliyotakiwa izungushe pale Ofisi Kuu ya CCM, hakuna gari iliyoruhusiwa kuzungusha pale Baraza la Wawakilishi la zamani, hakuna gari iliyotakiwa izungushe pale Darajani, hakuna gari iliyotakiwa izungushe Michenzani. Gari zote zinatakiwa zifuate mzunguko wa kawaida kuja mjini kutoa huduma kushusha abiria na kupakia abiria. Kwa ile gari ambayo haiko kwenye zamu ya wakati ule iende ikaegeshe katika vituo vya muda vilivyopangwa, ikifika zamu yake iingie mjini.

Mhe. Mwenyekiti, kinachofanyika madereva hawa hawataki kufuata utaratibu, sasa kama hawataki kufuata utaratibu ndio maana nimeeleza hapa *traffic* nao wanachukua hatua kwa wanaofanya makosa wanawapeleka Mahakamani, na wakifika mahakamani wanadaiwa sare, wakati najua mimi Mahakama zinahukumu kwa mujibu wa sheria.

Ndio nikasema kuna changamoto ambazo unaweza ukahisi kwamba sisi peke yetu kama Baraza la Manispaa tuna wajibu wa kufanya hivyo. Tumekaa serikalini; Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria nilimwambia hili jambo, kwamba tulifanyie utaratibu yeye aliulizie, kwanza lina ukweli gani hayo wanayotuambia polisi, kwa maana ya usalama barabarani au na wao wanafanya hivi kwa sababu gani tujue. Lakini suala hili tulikubaliana na hatukukurupuka, na kama mtu hataki kufuata utaratibu wa sheria, umeshafanya juhudi zote za kumuelimisha kinachobakia serikali ni kuona kwamba wanaoishi katika mazingira yale, pamoja na wale wanafunzi ambao wana mahitaji maalum, ni lazima na wao wapate haki yao ya kimsingi.

Kwa hivyo, Mhe. Ismail Jussa rafiki yangu kama alivyoniambia atuelewe kuwa serikali kwanza hatukukurupuka tu, isipokuwa ni kweli kabisa hakuna kituo kati ya mji na hili tumelifanya kwa kukumbuka utaratibu uliokuwepo zamani; kwamba gari zote zinazotoka Mkoa wa Kaskazini na njia ya Kaskazini stendi yao ilikuwa pale Kinazini, kwa hivyo imetoka Kinazini tumesema zikakae Saateni, gari zote zinazotoka njia ya Chwaka zikae pale Kibandamaiti na nyengine zinakaa Mwembeladu, gari zote zinazotoka huku Fumba na kwengineko zikakae kwa Bintihamrani. Na utaratibu huo unafanyika kwa kuwatumia watu wanaitwa Mabaguani wanaosimamia *route;* na ule mzunguko wa wafanyabiashara wa daladala, wanajua kwamba nani mwenye zamu ya kufanya kazi ya kwenda kuchukua abiria na yupi anatakiwa akae, ni hivyo hivyo na tulikaa nao tukakubaliana nao.

Kwa hivyo, kama mkiniambia nisichukue hatua, maana ni nyinyi hapa mlioniambia kwamba wanaudhi, kuna hali isiyokuwa ya salama. Sasa mtu anapotakiwa afuate utaratibu hataki basi tutatumia mbinu nyengine ili kuhakikisha anafuata utaratibu huo. Wala sisi hatwendi kutumia mabavu kama hivyo inavyofikiriwa, lakini tutatumia utaratibu mwengine wa kiserikali ili kuhakikisha kwamba kituo kile msisitizo ni kuondoka.

Mhe. Mwenyekiti, nilisema na tulishauriwa kuwa badala ya hawa kuegesha hapa kama wanaona kwenda huko ni mbali, basi tufikirie uwezekano wa kuwapeleka pale Mnazi Mmoja. Kwa hivi sasa serikali kama hatujamaliza kupata *master plan* mpya ya mji, basi tutashindwa kusema kituo cha kudumu ni kipi ndani ya mji wetu, ahsante sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kama ulivyoniona namsikiliza kwa makini sana Mhe. Waziri, majibu yake yanaonesha changamoto ambazo zipo. Mhe. Mwenyekiti, hoja tunayoisimamia ni kwamba kama hujatatua tatizo la kuwa na kituo kwenye eneo la mji; kwa sababu watu wanafuata huduma katika mji, na bahati mbaya sana kwa nchi yetu, pamoja na mji kutanuka sana, lakini bado huduma za msingi; ofisi nyingi za serikali, hospitali kubwa, soko kubwa, maeneo ya kibiashara takriban huduma nyingi bado zimejikita katika eneo la Mji Mkongwe na katika eneo linalozunguka viunga vyake; Darajani, Vikokotoni na maeneo yake.

Kwa hivyo, binadamu kwa kawaida Mhe. Mwenyekiti, hata ukimpangia vipi, kama hajafuata mfumo ambao unamfikisha pale akapata huduma zake, ikiwa ni hospitali, ikiwa ni biashara, ikiwa ni taasisi za serikali na ikiwa ni soko bado atatafuta mbinu yake. Kama ilivyojitokeza Darajani kwamba kimehamishwa wametafuta njia nyengine.

Kwa hivyo, mimi nataka kumshauri Mhe. Haji Omar Kheri ni kwa nia njema na serikali kwa jumla; kwamba maamuzi haya kwa sababu tumesema ionekane imetekeleza ndio anasema kesho kitaondoka, basi maamuzi yatakuwa ni yale yale. Mimi ningeshauri serikali ingelichukua hili na haya yaliyotolewa na Wajumbe, kumetolewa rai hapa. Mimi siwezi kusema kwamba kikahamie Mnazi Mmoja, na kawaida yangu sipendi kuingilia mamlaka yaliyokuwa sio yangu, lakini nasema wao wenyewe wakae na waangalie katika maeneo yaliyo karibu kwenye kupata hizi huduma Mhe. Mwenyekiti, watu wanatoka Bandarini.

Mhe. Asha Bakari alisema humu ndani kwamba wananchi wa Pemba wakisafiri wanakwenda na twika na wakirudi twika, twika zile anajitwika mpaka wapi Mhe. Mwenyekiti. Huwezi kumwambia akapande daladala katika maeneo uliyompangia. Kwa hivyo, nasema na wale wanafunzi wanaotoka skuli jioni, ukimwambia mwenye daladala moja iliyokuwa zamu ipakie abiria basi wanafunzi wanatoka kwa maelfu kwa pamoja skuli, hilo bado ni tatizo.

Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri katika hili asije akajijengea sifa, na sio yake yeye tu inakwenda mpaka kwa serikali anayoiwakilisha, kwamba inatumia nguvu na ubabe kwa hayo maamuzi ya kukurupuka kwamba kesho nitaondosha. Serikali ilichukuwe hili wakakae kwa makini watafute ni wapi kituo cha kudumu kiwe bila ya kuwasumbua wananchi, wananchi hawa hawa mwakani tunahitaji watupigie kura. Wasije wakafikiria wanahudumiwa wananchi wa Mji Mkongwe tu, wanahudumiwa wananchi wa kila kona ya mji wetu kwa mapana yake wanafuata huduma pale. Sasa kama Mhe. Haji Omar Kheri na chama chake hawawataki mwakani atatwambia, lakini mimi namshauri sana kwamba atafakari na alichukuwe, sio maamuzi ya leo kwa kesho, hapana. Atafakari afikiri vipi tupate kituo cha maana cha kuwahudumia wananchi, kuwafikisha katika huduma zao, lakini pia kupanga mji wetu vizuri. Hata kama ni cha muda mpaka hapo mipango ya miji itakapokaa sawa. Hilo ndio ninaloiomba serikali Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa nadhani Mhe. Waziri suala ulichukuwe na serikali, halafu baadaye kutatolewa maelezo au wataona wenyewe wananchi. Mhe. Nassor Salim Ali utaratibu.

UTARATIBU

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Mwenyekiti, huwa tuna utaratibu kila wakati wa kupitia vifungu, watendaji huwa wanaingia ndani ili kuweza kumsaidia majibu Mhe. Waziri, lakini leo tunashangaa kwamba kwa nini wamezuiwa hawakuingia ndani kuja kumsaidia Mhe. Waziri. Naomba muongozo wako Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Utaratibu hebu angalia na viti vyetu 12 tu angalia kule juu, wizara ni kubwa hawawezi kuja wote. Kwa hivyo, tumeona ni bora tuwaache kule kule. Bado una hoja.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Mwenyekiti, wa kuingia humu ni Makatibu Wakuu na Wakurugenzi, sio lazima waingie wote, lakini wale ambao ni wahusika wakuu kama Katibu Mkuu na Wakurugenzi waingie ndani.

Mhe. Mwenyekiti: Nitamwambia Waziri atafute wale muhimu watashuka. Waziri atawataja wale muhimu watateremka watamsaidia. Mhe. Waziri hebu chagua wale muhimu wanaokufaa waje kukusaidia, uchague maafisa ambao wanaweza kuingia hapa ndani wakakusaidia, laa umeridhika tuendelee, maana umeombewa wewe.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, nijibu hili au.

Mhe. Mwenyekiti: Hilo la Mhe. Nassor Salim Ali umelifahamu?

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: la Mhe. Nassor Salim Ali?

Mhe. Mwenyekiti: Eeeh.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mimi nahisi haya masuala bado nina uwezo nayo Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hivyo, mwenyewe ana uwezo nayo. Tunaendelea. Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nilitoa mapendekezo kwa serikali, lakini sijapata majibu. Kwa hivyo, tukiiacha hivi hivi hoja yangu itakuwa inaning'inia bado, natoa hoja yangu, bado naomba majibu ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi nilitegemea imeshachukuliwa.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwanza chama changu kinawajali sana wananchi na wala hata siku moja hatuwezi kuwa sisi hatuwapendi, hatuwataki na hatuwatakii mema wananchi na ndio maana tulikuja na ilani ya uchaguzi na tunaendelea kuisimamia ilani hiyo. Serikali inatakiwa isimamie hilo. Kwa hivyo, hili la kwamba Chama changu hakiwajali, hili naona Mhe. Ismail Jussa Ladhu, nadhani amekwenda mbali zaidi, mimi sitaki kusema ameteleza wala nini, lakini amekwenda mbali zaidi, chama changu kinawajali sana wananchi wa nchi hii ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, lakini jengine ni kwamba ushauri ambao amenipa Mhe. Ismail Jussa Ladhu, mimi naupokea na ndio maana tokea pale mwanzo nimesema jambo hili kutokana na changamoto zake, Serikali imeamua kukaa kulitafakari upya, lakini sasa tuliona labda ameshalielewa. Kwa hivyo, ushauri wake tunauchukua na tutaufanyia kazi, lakini na suala la kufanya jitihada za kuwaondosha wanaovunja sheria hili nalo nafikiri hatutolitumia nguvu, asiwe na hofu, hizo hizo taratibu za kukaa tutakazo za njia gani mbadala ya kuwaondosha, ahsante sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi hii nikaongeza ufahamu na uelewa kidogo kutoka kwa Mhe. Waziri, kwanza Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, nakushukuru sana kwa majibu yako na nitaomba tu kama alivyoutoa ushauri Mhe. Ali Mzee Ali jana kama utauchukua ushauri wa Mhe. Ali Mzee Ali kwa sababu Wizara yako ni ngumu tusisubiriane hapa, tufanye kazi bega kwa bega, naamini tutakwenda vizuri. Sasa katika mashirikiano hayo hayo bado nilikuwa narudia hili suala la wananchi walionileta hapa wa Jimbo la kwa Mtipura hasa katika ujenzi wa mitaro umetoa ufafanuzi mzuri, lakini mimi nilikuwa na wasi wasi na jambo moja kwa sababu niliwahi kupata majibu mazuri sana kutoka kwa Mhe. Waziri aliyekuwa katika Wizara hii na yeye alitupa mpaka muda wa kuanza kutoa tenda kwa wakandarasi, lakini katika kitabu chako safari hii nilipokuja kuiona ndio kwanza umetafuta mshauri mwelekezi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa mimi niliwahi kusema sana huko nyuma kwamba kwa nini mradi huu ukawa unasimamiwa na Wizara ya Fedha, usisimamiwe na wenyewe Baraza la Manispaa na hapa inaonyesha hapa ndio kidogo kwenye kukwama kwa huu mradi, kwa sababu Baraza la Manispaa mitaro ikijaa maji watu wakizama, sisi tunawasakama wao, tunajiuliza kwa nini wanashindwa kuiboresha mitaro hii inaonyesha hapa kuna *gap* kubwa baina ya Baraza la Manispaa na Wizara ya Fedha, sasa pamoja na kwamba Mhe. Waziri ameniambia tarehe ya kukaa na Waziri wa fedha nafikiri tarehe 13.

Mhe. Mwenyekiti, naomba labda huu ushauri wangu katika hicho kikao chao, haoni iko haja hivi sasa ule mradi ukahama Wizara ya Fedha ukahamia Baraza la Manispaa kupitia Wizarani kwake ili kuhakikisha huu mradi unakwenda na hoja yangu na hofu yangu mradi huu kama nilivyosema sasa hivi unafika karibu miaka mitano, bajeti ya mtaro wa Kwamtipura mpaka Shaurimoyo, bajeti yake nakumbuka kama ilikuwa bilioni moja na milioni mia mbili kwa wakati ule.

Je, sasa hivi mradi ule utakuwa umeshafikia fedha kiasi gani? Je, fedha zile kama hazikuja kutosha, tutawaambia nini wananchi wa Jimbo la Kwamtipura pamoja na wananchi wa Amani, Magomeni na sehemu nyengine? Labda nilikuwa nataka hizo rai zangu mbili aweze kunisaidia.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, mimi nimemfahamu sana Mhe. Hamza Hassan Juma, kwanza nataka nitumie nafasi hii tena kwa mara nyengine tena kumpongeza mzee wetu Profesa Ali Mzee Ali, kwa ushauri ambao ametupa na ushauri kwa Mhe. Ali Mzee Ali kwangu haukuanzia Barazani. Kwa hivyo, nitaendelea kufuata ushauri ambao wametupa na ule anaotupa sote serikalini, lakini nataka kukushukuru pia Mhe. Hamza Hassan Juma kwa kuelewa changamoto zinazoukabili mradi huu na ndio maana nimesema baada ya kupata changamoto hizi, ndio maana serikali tumeamua tukutane kati ya Wziara ya Fedha na Wizara yetu kuzungumzia namna ya mustakabali wa kuendesha mradi huu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani kwa *stage* iliyofika, si vizuri kusema tuutoe Wizara ya Fedha, lakini nafikiri kuwe na ukaribu zaidi wa ufuatiliaji kati ya Wizara yangu na Wizara ya Fedha, utaratibu uliopo sasa, sisi ni watu ambao tunafaidika na huo mradi kama Manispaa Wizara ya fedha, ndio wanaosimamia utekelezaji, lakini kuna na timu nyengine ya nje ya taasisi za serikali ndio kama *coordinator* wa huu mradi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, sisi huku serikalini tunachoweza kufanya hasa katika maeneo ya *Procurement* na maeneo mengine kukawa na timu yenye mchanganyiko kati ya Wizara ya Fedha na Wizara ya Nchi Afisi ya Rais,

Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ ili kuwe na ukaribu zaidi wa kuweza kufuatilia, kwa sababu ni kweli masuala zaidi tunaulizwa sisi, kuliko kuulizwa Wizara ya Fedha.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, ushauri wake hiki kikao ambacho nimekisema sio tarehe 15 au 13, ni kabla ya tarehe 13, mkutano huu nataka nimhakikishie Mhe. Hamza Hassan Juma, utafanyika na huu ushauri ambao ametupa tutauweka mezani ili tuone tutakavyokubaliana, kama hakuna ulazima kwamba lazima tusimamie, lakini tuwe karibu zaidi katika kufuatilia mradi huu badala ya kuwaachilia Wizara ya Fedha peke yao, hilo nina hakika Mhe. Hamza tutalifanya na matokeo yataanza kubadilika baada ya mashirikiano hayo kati ya Wizara yangu na Wizara ya Fedha, ahsante sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri kwa kiasi fulani ameukubali ushauri wangu, lakini vile vile, amejaribu kuniambia kwamba kwa kuwa Wizara ya fedha wao ndio *coordinator,* ni busara basi na wao waendelee kushirikiana, unajua hofu yangu mradi wa *E-government,* tuliupigia kelele sana kwa sababu hivyo hivyo hauna bwana mmoja na mradi ukiwa hauna bwana mmoja, kila mmoja anahisi afanye shughuli zake zilizokuwa za msingi ile nyengine inakuwa ya baadae, lakini mradi huu kama ungekuwa moja kwa moja chini ya Wizara hii ya Afisi ya Rais inayoshughulikia Tawala za Mikoa, mradi huu naamini tungekuwa tumeshafikia pahala, Wizara ya Fedha kila kitu wana Wizara ya fedha, miradi yote fedha, Wizara ya Fedha watafutaji fedha ni Wizara ya Fedha, wasimamiaji wa miradi ni Wizara ya Fedha, tuwapunguzie mzigo Wizara ya Fedha, watutafutie pesa, hizi Wizara ambazo zenye miradi waachiwe.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu hoja yetu itakuja hapa, mradi leo umekwenda vizuri sawa, mradi unakuja kufeli tunamkamata nani, tunataka tumkamate Waziri mwenye sekta. Kwa hivyo, mimi bado nashauri na naamini Mhe. Haji Omar Kheri mimi ni mwalimu wangu, mimi kabla ya kugombea jimbo nilikuwa naangalia harakati zake jimboni namna gani alivyokuwa anapeleka maendeleo Tumbatu na mimi ndio nikaiga, sasa asije akaniharibu huku.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi palipobakia padogo, Watumbatu na Washaurimoyo mradi huu kama haukufanyika watakuja kuniua, sasa nilikuwa namuomba sana kwanza akubaliane na huo ushauri wangu hoja atakayokwenda nayo kwa Wizara ya fedha nipeni mradi wangu kwa ushauri wa Baraza la Wawakilishi, akishakabidhiwa yeye naamini mradi utakwenda. Sasa kabla sijakaa nitamuomba Mhe. Haji Omar Kheir, kama alivyomuahidi Mhe. Hija Hassan Hija, basi mimi kwa kuwa Mwenyekiti wa Wenyeviti sitokubali Mjumbe wangu akaondolewa wakati tupo katika *section* ya baraza, Makamu wa pili wa Rais yeye ndio kiongozi wa Shughuli za serikali *backbencher*.

Mhe.Mwenyekiti,mimi mwenyewe ingawa Kanuni haijatungwa, lakini taratibu zipo, naomba tukishamaliza hili baraza, basi tuandae siku tuende kule Jimboni na sheha wa Shaurimoyo ananisikia tukakae Jimboni na wale Watumbatu wote wanaozama wakati wa masika tukakae na Waziri ili ile ahadi niliyoitoa mimi kwamba mtaro ule ungelijengwa Julai, 2013, sasa aje atwambie tarehe nyengine ikiwa yeye ndio Waziri wa Tawala za Mikoa, ikiwa *time* hiyo mradi ameshakabidhiwa na Wizara ya Fedha, naomba jawabu.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe.Mwenyekiti, mimi mwalimu wake Mhe. Hamza, sitaharibika upevuni, nataka nimhakikishie kwamba niliyomfundisha bado nayakumbuka na mengine aliyoyafanya chini ya mafunzo hayo pia nitayaendeleza, lakini Watumbatu walipo Shaurimoyo *Ishaallah* haitatokea siku wazame kwa mafuriko, kwanza namuahidi nitakwenda kuwahakikisha wananchi wa Shaurimoyo na Kwamtipura kwa sababu mimi nina *programme* nzima hapa ya utekelezaji wa huo mradi wenyewe, lakini sina muda wa kuweza kuisoma, naomba uridhike na hilo, lakini ushauri wake tunaupokea na kama nilivyosema, ndio madhumuni ya kukaa serikali.

Mhe.Mwenyekiti, kwa hivyo, naomba atuamini kwamba tutakaa na ushauri wake, nitaufikisha ukikubalika itakuwa *well and good,* lakini kama haukukubalika angalau lile la kuwa na ukaribu zaidi kati yetu na wao kufanya kwa pamoja, basi hilo linaweza kufanyika ushauri wake tunaupokea.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kama katika ushauri watashindwa basi iko timu yetu ambayo Wizara ya Fedha tunataka wapunguziwe majukumu, tutakwenda kumsaidia. Kwa hivyo, naomba tuendelee.

Kifungu 0401 Idara ya Mipango Sera na Utafiti- 337,472,000
Kifungu 0801Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa-

Mhe. Jaku Hassan Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ahsante, kwanza nitakuwa sio mwingi wa fadhila kama sikumshukuru Mhe. Waziri Haji Omar Kheri kwa kupangua hoja baada ya hoja kwa ufundi wa hali ya juu, nakushukuru sana Mhe. Waziri, hoja zangu hapa zilikuwa mbili, moja inafanana na Mhe. Ismail Jussa Ladhu, nitakwenda na hii kubwa ambayo inahusu wananchi kwa nguvu kubwa sana ya Hospitali ya Mnazi Mmoja, Mhe. Waziri nikuombe sana kwa unyenyekevu sana kabisa wajawazito wamekuwa wakipata shida kwenye kujifungua Hospitali pale na chombo hiki au uheshimiwa wetu huu unatokana na wananchi kutuchagua sisi ili tuje tuwasemee hapa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, mimi nimuombe kabisa Mhe. Waziri tena kwa unyenyekevu wa hali ya juu ukaziruhusu baadhi ya daladala kwenda kule Hospitali ya Mnazi Mmoja, hivi sasa wananchi wanateseka, madaktari hawapiti kwa wakati, manesi hawafiki kwa wakati na vyengine, hata hivi vi-*notes* tumeletewa, sasa hivi si muda mrefu hapa, naomba nikione.

Mhe. Mwenyekiti, muombe Mhe. Waziri *Stands* za Unguja lazima gari zifike Hospitali kwa sababu za kuwasaidia wagonjwa na wajawazito, gari hazifiki, hii hapa. Kwa hivyo, nikuombe sana kwa unyenyekevu wa hali ya juu kabisa na kwa lugha nyepesi na laini ufanye haraka pale gari ziende ni hayo tu.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mhe. Jaku kwa unyenyekevu mkubwa kwa kunieleza hoja yake na ningemshangaa sana angeniuliza kwa munkari, kwa sababu mimi na yeye tunatokea mbali, hatukukutana hapa.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Jaku, kwanza hakuna daladala yoyote iliyokuwa haikupewa ruti ya Mjini na kufika Hospitali, kinachofanyika bado ni ubishi wa waendesha daladala kwa kutaka mapato ya haraka haraka kwa kugeuza katikati ya njia, bila ya kugeuza na bila ya kufika huko kwenye vituo. Kwa hivyo, idara ya leseni ya barabara inayohusika na jambo hili, ruti ya mjini kwa daladala yoyote ile ni lazima kituo chake cha mwisho iwe Hospitali.

Mhe. Mwenyekiti, ninachoweza kumhakikishia Mhe. Jaku, mimi kwa kushirikiana na Wizara husika tutasimamia jambo hili ili kuhakikisha vituo au gari hizi za daladala zinafika kwenye kituo cha mwisho kilichowekwa kwa mujibu wa sheria na yule ambaye atafanya ubishi wa kufuata taratibu hizo, basi tutatumia sheria ya usalama barabarani ili kuweza kumdhibiti na kuweza kumchukulia hatua za kisheria. Kwa hivyo, Mhe. Jaku usiwe na wasi wasi tutalisimamia hilo ili liweze kufanya kazi.

Mhe. Jaku Hassan Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini nahofia anaweza kusimama kwa muda mrefu bila ya kukaa kitako, sasa aniambie atasimamia lini nimuombe hivyo tu ili kukuonea huruma ili wananchi wetu wasije wakateseka.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, hivi ninavyokwambia Ofisi ya Mkoa wa Mjini Magharibi chini ya usimamizi wangu na Kamati ya usalama barabarani wameshapanga tarehe ya kuweza kukutana kuzungumzia kadhiya hii. Kwa hivyo, asiwe na wasi wasi.

Mhe. Jaku Hassan Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, uungwana ni vitendo, tuendelee.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, nimesimama hapa si kwa sababu ya kumzuia rafiki yangu fungu, hapana, ninachotaka anihakikishie kurekebisha hii hali akiwa ndio msimamizi wa Manispaa ya Zanzibar, wakati nikichangia nilizungumzia juu ya namna ya taratibu za utendaji katika Baraza na ambapo wakati ule tulipokuwa na Kamati teule ya Baraza la Wawakilishi tuligundua kasoro nyingi hasa katika masuala Katibu na masuala ya utendaji. Sasa mwanzo baada ya kuja Mkurugenzi mpya alianza vizuri na tukamsifia, lakini baada ya muda mfupi, sasa ameanza kutuharibikia na kumekuwa na malalamiko.

Mhe. Mwenyekiti, sasa ni kwamba sheria hii tuliyopitisha namba tatu ya mwaka 1995 inazungumzia juu ya utendaji wa Mkurugenzi wa Manispaa kwamba atawajibika katika Baraza la Manispaa, lakini kinyume chake sasa Mkurugenzi amekuwa akichukua maelekezo Wizarani jambo ambalo linakwamisha shughuli za utendaji na kuhamisha nguvu za utendaji wa taasisi ile.

Mhe. Mwenyekiti, kitabu chake Mhe. Waziri, kina maelezo hapa, naomba nimnukuu ameyasema mwenyewe kwenye hotuba yake, nanukuu sehemu tu. Ukurasa wa 23 inasema; "Marekebisho hayo yamefanyika kufuatia

kukamilika kwa sera za Serikali za Mitaa, mabadiliko hayo ya sheria yatasaidia utekelezaji wa sera kwa uhalisi, aidha sasa nakuja hapo idara inayoratibu vikao mbali mbali vya kupeyana miongozo ya utendaji kazi kwa waheshimiwa madiwani ambao ndio waamuzi wakuu wa shughuli za Serikali za Mitaa"

Mhe. Mwenyekiti, sasa kama Mhe. Waziri, anakiri kwamba Madiwani kupitia *Council* yao ndio waamuzi wakuu, leo inakuwaje Mkurugenzi anakwenda kuchukua maelekezo Wizarani badala ya kufuata sheria. Kwa hivyo, utendaji wake unaonekana unakwenda kinyume na sheria, sasa mimi ushauri wangu Mhe. Waziri, arekebishe hii hali kwa sababu kitendo hiki ndio kilichosababisha kuwe na malalamiko mengi mji mchafu, hapa pako hivi kwa sababu wale waliopewa mamlaka hawapewi fursa ya kuamua juu ya mustakbali wa taasisi ile baadae tukawapa nafasi ya kuwalaumu wao, sasa nimuombe Mhe. Waziri, hapa ajikubalishe juu ya kuirejesha hiyo hali na kumtaka Mkurugenzi sasa afate sheria. Mkurugenzi hatakiwi kufanya kazi na Wizara. Mimi *concern* yangu ndio hiyo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi nataka nimshukuru sahibu yangu Mhe. Salmin Awadh Salmin mrithi wangu wa nafasi ya Unadhim wa CCM ndani ya Baraza hili la Wawakilishi na Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Magomeni.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nikubaliane nae na nukuu yake ya kifungu cha sheria na ndio maana mimi nikaamua kukiweka kwenye bajeti yangu kwa kuelewa hilo. Natambua kwamba Mheshimiwa alikuwa Diwani pale, lakini napenda kuliarifu Baraza hili pia na mimi nilikuwa Afisa mmoja mkubwa sana pale ndani ya Baraza lile. Nilikuwa *Public Relation Officer* katika Baraza lile. Kwa hivyo, natambua kwa kiasi fulani na siwezi kuzipuuza hizo sheria. La kwanza ushauri wake ninaupokea, la pili, kutokuonekana kwangu kwenye *field* ni kwa sababu tu kuna kipindi nilikuwa likizo, lakini kuna kipindi tulikuwa kwenye Bunge la Katiba na inawezekana kipindi kile nilikuwa naonekana kwenye *TV*, sasa hivi ninakwenda bila ya *TV*. Kwa hivyo, bado nakwenda na nimeshakaa na Waheshimiwa Madiwani na Mkurugenzi wa Manispaa kuyazungumza haya, sina tatizo na hali. Kwa hivyo, ushauri naupokea.

Mhe. Mwenyekiti, lakini suala hili tulieleze vizuri, kwa nini Mkurugenzi anakuja Wizarani. Mimi Waziri na *Minister* maana yake sio mtu mmoja, *Minister* maana yake pamoja na watendaji wake. Kwa hivyo, mimi saa nyengine ninapotaka kuzungumza na Mkurugenzi nitamuagiza Katibu Mkuu, hebu zungumza na Mkurugenzi kuhusu jambo hili na hatuzungumzi na Mkurugenzi *against* na maamuzi ya Wajumbe wa Baraza la Mji kwa maana ya Madiwani hapana. Kwa sababu hii taasisi bado ni taasisi ya serikali na mimi napokea maelekezo kutoka serikalini na maelekezo hayo ni pamoja na ripoti ya Kamati Teule ambayo Mhe. Salmin ameiongoza.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimuhakikishie ripoti ile ndio *reference* yangu ya kuendelea kulirekebisha Baraza la Manispaa. Anapoitwa Mkurugenzi katika Wizara iwe nimemwita mimi kwa sababu karibu katika kipindi hiki chote hizi shughuli zote zinazofanyika za *operation* hasa za usafi, mimi huwa ninamuuliza mshakaa na Madiwani kuzungumzia hali ya uchafu? Mimi ninamuhimiza hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, ninakubali ushauri wake, kwanza nataka nimthibitishie kwamba sheria mimi nitaisimamia na kuifata kikamilifu, wala Madiwani hawataingiliwa, wala hawatapuuzwa maamuzi yao na Mkurugenzi ili afanye kazi vizuri lazima afate ushuri wa Madiwani, lakini sisi kama binaadamu tuelewe kwamba wengine tuna matatizo. Kwa sababu miongoni mwa mazonge ambayo yapo Baraza la Mji mengine yanasababishwa na Madiwani.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nitoe mfano mmoja juzi kuna Diwani mmoja katoa ruhusa ya kujenga pahala pasiporuhusiwa. Sasa Diwani kama huyu ambaye sidhani kama ndie anayemzungumzia, lakini wapo Madiwani ambao nao inabidi lazima tuwarekebishe na tuzungumze nao, tuwashauri kwa kupitia Mstahiki Meya. Mstahiki Meya mwenyewe anapokuwa jambo anakuja Wizarani na anaarifiwa kila kitu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, Mhe. Salmin nimemuelewa, la kwanza nataka nikubali ushauri wake tutafuata sheria, tutaheshimu maamuzi ya Madiwani, lakini kuna maelekezo ya kiutendaji, saa nyengine ya kisera lazima nayo hayo yatoke kutoka kwa Kamisaa wa Wizara hii. Kwa sababu saa nyengine nisipotoa maelekezo nisipoita nikajua kinachoendelea haya masuala mnayoniuliza hapa, wala sitapata kuyajibu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, naomba Mhe. Salmin anielewe mimi ni muumini wa jambo hilo na ushauri wake tunaupokea.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, ahsante, nimemsikiliza kwa makini sana Mhe. Waziri na maelezo aliyoyatoa yanaweza kuwa ni sahihi, lakini ninataka kumkumbusha Mhe. Waziri, kwamba taasisi hii inaongozwa na wanasiasa, Madiwani ambao wamechaguliwa na yeye ndie mwanasiasa wa Wizara.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, ni vyema mara nyingi kunapotokea matatizo, basi mtu wake wa karibu ni Mstahiki Meya pamoja na Naibu Meya, ndio kiungo kikubwa. Kama kuna Madiwani wamefanya matatizo ama wamefanya hivi na ndio maana sheria hii namba 3 ya mwaka 1995 imemtaja zaidi yeye Waziri kusimamia taasisi ile, kwa sababu ni ya wanasiasa na wao wanasiasa ndio wasimamizi wa sera kuhakikisha zile sera ambazo zipo, basi zinatekelezwa ipasavyo, yanaweza kuwa matatizo yapo kati ya Madiwani hayakosi, lakini ni vyema tukaiangalia zaidi sheria na ile dhamana ambayo Mhe. Waziri amepewa juu ya taasisi hii.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kama utakuwa unawatumia watendaji wako wa chini, Wakurugenzi wako matokeo yake mambo haya yatakwenda kombo. Ni vyema ukatumia muda wako Mhe. Waziri, ukahakikisha unamtumia zaidi Mstahiki Meya katika taasisi ile, kwa sababu hata sheria imesema humu kwamba Baraza la Manispaa ni *Board Corporate*, ni Taasisi inayojitegemea na Waziri umeunganishwa pale kama mwanasiasa. Kwa hivyo, Taasisi zote hata binafsi ziko chini ya Mawaziri. Kwa hivyo, tuwape nafasi hawa Waheshimiwa Madiwani ili tuje tupate nafasi kuwalaumu inapotokea hitilafu.

Mhe. Mwenyekiti, juzi katika suala hili ambalo Mhe. Waziri ameeleza la uhamaji kutoka pale kwenda eneo jengine. Waheshimiwa Madiwani walikuwa hawana taarifa juu ya hali ile Kamati zinazohusika hazina taarifa, Madiwani hawana taarifa, lakini kibaya kilichofanyika katika jengo lile ambalo wametoka huku, basi hata uchochoro mmoja kuweka viti Madiwani wanapokwenda pale kufanya shughuli zao hawajatengewa na badala yake Madiwani wanapofika pale wanakaa chini ya miembe.

Mhe. Mwenyekiti, sasa mimi nashangaa kwamba mtu punda wake anakwenda kumkalia mkiani. Tunaposema Baraza la Manispaa maana yake ni Madiwani, leo Madiwani wanapokwenda katika Ofisi yao wanakaa chini, miembe ikinyesha mvua wanajibanza banza pembeni, huu sio utaratibu. Kwa hivyo, ninamuomba sana alisimamie hili, tuone kwamba hii sheria inafatwa na mambo mengine yanakwenda vizuri.

Mhe. Naibu Spika, tuendelee.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwa kuwa muda wetu wa kawaida unakaribia kumalizika na kazi yetu haijesha, ninamuomba Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais atoe hoja ya kuongeza muda ili tumalize shughuli yetu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais: Kwa kuwa muda wetu kama ulivyosema unamalizia na kwa kuwa kazi iliyo mbele yetu bado inahitaji muda zaidi. Kwa hivyo, ninaliomba Baraza lako tukufu liridhie kuongeza muda ili tuweze kumaliza kazi iliyo mbele yetu. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, niwahoji wale wanaokubaliana na hoja hiyo ya Mhe. Waziri, wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

KAMATI YA MATUMIZI

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi jana nilipokuwa nikichangia katika kifungu hiki cha Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, nilitaka kujua ni kitu gani kilichokwamisha soko la Kangani

kutokumalizwa kujengwa hadi hii leo wakati watu wanauza samaki chini? Nilimuomba Mhe. Waziri, anipe maelezo juu ya soko hili. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, haya ni katika yale ambayo nilishindwa kuyajibu kutokana na muda, lakini jawabu lake lipo, kilichokwamisha ilikuwa ni uchache wa fedha na kwa sababu tayari Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani imekusanya mapato mengi zaidi, nataka nimuhakikishie Mhe.Mwanajuma Faki Mdachi, kwamba soko hilo litaingia katika mpango huu wa mwaka huu kulimalizia ili liweze kufanya kazi zake na ndio maana zile fedha nilizizuia nikasema tupate kianzio. Kwa hivyo, astahmili kidogo ili tuweze kupitisha bajeti yetu, tunacho kianzio, pesa zile tutazielekeza katika miradi ya maendeleo kama hiyo ya Soko la Kangani. Ahsante sana.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee.

Kifungu 0801 Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa- 1,200,000,000

Kifungu 0802 Baraza la Manispaa-

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, ahsante, nishukuru kwa majibu ya Mhe. Waziri namna alivyokuwa akichambua majibu yake.Wakati nikichangia nilichangia zaidi suala la Baraza la Manispaa katika masuala mazima ya taka na nikatoa mfano mpaka wa baadhi ya majaa na zaidi nikatumia katika jimbo langu ambayo yako katikati ya eneo na Mhe. Waziri wakati akifanya majibu yake alielezea changamoto zinazoikabili Baraza la Manispaa jinsi ya suala zima la ukosefu wa magari na akataja mpaka tarehe za magari kuwasili *by July to August,* lakini mimi nataka nimsidie Mhe. Waziri, nataka nimsaidie kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati nzuri mimi nina uzoefu wa Baraza la Manispaa na katika uzoefu wangu wa miaka 10 ndani ya Baraza la Manispaa miaka yote 10, nilikuwa *chairman* pia nilikuwa *chairman* wa huduma za jamii ndani ya Baraza la Manispaa. Sasa nataka nimueleze tu kwamba pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, hatuwezi tukasubiri Julai, Agosti wakati hatuna uhakika wakati wananchi ndani ya maeneo wanateketea katika suala zima la usafi wa Mazingira na kuna tatizo nataka unisaidie, mimi ninakushukuru kila majibu yako unasema kwamba utasimamia na utafatilia na hapa nataka bado ufatilie. Pamoja na kwamba tuna matatizo ya magari, lakini bado kuna matatizo ya *Management* ndani ya Baraza la Manispaa. Tatizo gani ambalo lipo ninataka nimueleze Mhe. Waziri na atakuja kunieleza labda kama karidhika nalo au haridhiki.

Mhe. Mwenyekiti, hata hapo nyuma pia tulikuwa tuna ukosefu wa magari na hatukuwa na magari ya *pick up*, tulikuwa tunatumia magari ya *G.F* na tukatumia gari la tata katika ukusanyaji wa taka na katika zoezi hilo hilo sasa hivi magari hayo ya wazi tunayo yale ambayo ya *ZUSP* ambayo yameshawasili yale meupe, lakini tatizo linaloonekana hiki kitengo sasa hivi kina upungufu wa wafanyakazi na upungufu wafanyakazi wanao katika suala la kufariki ama kustaafu na kwa muda mrefu wafanyakazi katika kitengo hiki hawajaajiriwa, ukiachilia mbali hao wazee ambao yeye kawazungumzia wakati wa kujibu maswali yake.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimwambie Mheshimiwa nina ushahidi wa wafanyakazi wazoa taka ambao wameondoshwa katika taasisi ya kuzoa taka, sasa hivi wamepelekwa baada ya kuanzishwa kitengo kipya cha *Parking*, nina ushahidi wa majina, kwamba watu wameondoshwa kwenye taka wamepelekwa kwenye *Parking*, wengine wamepelekwa katika maeneo ya kusafisha njia za barabarani.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nataka nimwambie Mhe. Waziri ajaribu kulifatilia hili sababu za msingi za kuondosha watu kwenye taka, hapa inaonekana pana upungufu kwa sababu tulichokizoea kipindi cha nyuma kila jaa lilikuwa na watu maalum wa kusafisha taka ambapo wanafika alfajiri katika yale majaa. Sasa hivi inaonekana kwamba wafanyakazi wengi katika vituo hawapo na wafanyakazi waliokuwa wanachukuliwa kutoka kituo kwenda kituo na hili ni moja ya sababu.

Mhe. Mwenyekiti, anielezee tu ni namna gani atavyolifanyia ukarabati suala la kurejesha watu katika vituo ili kuondosha hili tatizo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, nataka nimshukuru ndugu yangu Mhe. Ali Salum Haji, shemeji yangu huyu kama alivyosema maelezo ambayo ameyatoa ni

kweli yeye aliwahi kuwa Diwani wa Baraza la Manispaa na aliwaji kukamata nafasi za uongozi katika chombo chetu hiki cha Baraza la Manispaa.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli lipo tatizo la kwamba hatujafanya *replacement* ya watumishi ambao wanafariki maeneo haya na vile vile, ni kweli kabisa kuna baadhi ya wafanyakazi ambao wametoka katika maeneo ya usafishaji na kupelekwa katika maeneo mengine, kwa sababu nayo hatujafanya uajiri kwa ajili ya maeneo mapya yaliyoanzishwa ya ukusanyaji wa mapato.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kwa jumla kwenye eneo la wazoa taka tunao 76 kama nilivyosema na hawa wengi wao wameshakuwa wazee na jitihada ni zile nilizozisema wakati ule kwamba tunachofanya sasa ni kuangalia upungufu uko wapi ili tutakapoweza kuajiri tuajiri katika maeneo hayo. Kwa hivyo, ninamuomba Mhe. Ali Salum astahmili kidogo mara tu baada ya bajeti hii tutafanya masawazisho hayo ili kuhakikisha tunaajiri wafanyakazi wa kutosha na kujaza zile nafasi za mapengo ambazo zipo kwa kuomba kibali kutoka Wizara ya Kazi na Utumishi wa Umma. Kwa hivyo, tatizo hili litamalizika ili tuweze kujaza wafanyakazi waweze kufanyakazi zao.

Mhe. Mwenyekiti, lakini vile vile, nakubaliana, ndio maana nilisema kwamba ukiacha *Management* ya Ofisi Kuu Baraza Manispaa, lakini kuna *supervisor*, *supervision* sio nzuri, nilikiri hapa kusema nayo, hiyo tuna haja tuweze kuisimamia ili tuweze kuondosha kasoro ambazo zipo. Ahsante sana.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, nimemsikia Mhe. Waziri na sitaki kuwa mbishi juu yake sana, lakini nataka tusaidiane mawazo. Nimekubaliana na mawazo yake kwamba baada ya bajeti wataajiri watu wengine kwa ajili ya ku-*cover* hizo nafasi. Nataka nimsaidie Mhe. Waziri, lakini bado kuna haja ya kuisimamia hii Wizara. Kwa sababu pamoja na ajira ambazo tunazoziajiri, lakini na kitendo ambacho kinafanyika katika Baraza la Manispaa pia hakiridhishi na kwamba mtu kaajiriwa katika suala la taka hana uzoefu wa kukusanya kodi, lakini anachukuliwa kwenye masuala ya taka, yanapelekwa katika masuala ya kodi, pia kuna athari ya kupunguza mapato ya Baraza la Manispaa.

Mhe. Mwenyekiti, sasa katika usimamizi wako na hili pia uliangalie. Nasema nina majina ya watu ambao wametoka kwenye taka hawana *experience* ya kukusanya kodi, sasa hivi wamepelekwa katika masuala ya kodi. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, sina dhamira ya kuzuia, lakini katika mchanganuo Mhe. Waziri, nilipochangia nilisema ile sura ya *Airport* haipendezi, sasa nafikiri kutokana na wakati Mhe. Waziri, hakuweza kunijibu. Kwa hiyo, naomba anipe taswira ya sura ya *Airport* itafanyika fanyika vipi angalau wale watu pale pajengwe vizuri ili ile sura ya *Airport* ionekane nzuri pamoja na Benki ya *CRDB* jinsi magari ambavyo yanavyosheni hata kupita hupati. Kwa hiyo, naomba anipatie ufafanuzi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana Mhe. Asha Bakari Makame, ni kweli sikupata kutoa uchanganuzi huo, lakini suala la *Airport* bado vile vile mamlaka ya kuweka ile sura kamili pale, mimi kama Halmashauri maana pale siyo Baraza la Manispaa, pale ni Halmashauri ya Wilaya Magharibi nayo ipo kwangu imekuwa vizuri hili suala umeliuliza hapa.

Mhe. Mwenyekiti, nitashirikiana na taasisi husika ili tuone tatizo ni nini ili tuweze kurekebisha mandhari iliyopo pale kweli hairidhishi na tuone tunafanyaje kuweza kuyashughulikia na eneo la *CRDB* Mkunazini kwenye *junction* au kule ndani nayo vile vile, tutaichukua na tunachukua ushauri wake ili tuende tukaufanyie kazi ili tujue tatizo ni nini ili tuweze kurekebisha hiyo hali.

Mhe. Asha Bakari Makame: Tuendelee.

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, wakati nilipochangia upande wa Manispaa nilitaka Mhe. Waziri, anieleze ile nia ya serikali ya kuondosha msongamano wa wafanyabiashara wadogo na waegesha magari kwa kujenga majengo ya kisasa eneo la Darajani amefikia wapi? Kwani katika majibu naona sikumsikia. Naomba anieleze kidogo Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Shadya aliuliza hoja hiyo na kweli sikupata kumjibu wala kutoa ufafanuzi na wameuliza watu kama wawili juu ya hoja hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, serikali kupitia Baraza la Manispaa tunao mpango wa kuliendeleza eneo la Darajani, ukanda wa Darajani kwa maana ya kutoka Malindi mpaka Mnazimmoja kwenye viwanja vya mpira, lile lote tunaita ni eneo la ukanda wa Darajani na kwa nini serikali imefanya hivyo, imefanya hivyo, Waheshimiwa wengi wamesema hapa anapokuja mgeni Zanzibar hasa Mjini Unguja hawezi kujua akikwambia nitembeze Mjini, hawezi kujua wapi mjini na wapi Ng'ambu. Hilo la kwanza.

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba serikali tumelitambua hilo na ndiyo maana tukaanza huu mpango wa kuuendeleza ukanda wa Darajani. Awamu ya tano ya serikali hii, walitaka kulifanya kama ni eneo la *Green belt* katika ukanda ule wote wa Darajani, lakini sisi tu tukajiuliza *Green belt* peke yake italeta manufaa gani kwa wananchi wa Zanzibar. Kwa hiyo, awamu ya saba tumedhamiria kuuendeleza ukanda ule kwa kujenga majengo ya kisasa yatakayofanana na mandhari ya Mji Mkongwe, tutaanza na lile la *Chawal Building* ambalo liko upande wa pili na Marikiti.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema juzi wakati wa kujibu hoja ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwamba nalo soko kuu tutalifanyia ukarabati mkubwa ili liweze kufanana na hadhi ya mji wa Zanzibar, lakini upande wa pili wa barabara tutakuwa na *shopping mall* moja na *shopping talk* moja. *Shopping talk* wale walioulizia wafanyabiashara wadogo wadogo watakwenda wapi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu sote tunapotembea ndani ya miji ya wenzetu tunaona kuna *shopping mall* ambao watu wenye *standard* ya kwenda kufanya *shopping* huko, wanakwenda na wale wa *shopping talk* wale wafanyabiashara wadogo wadogo na wao wanakuwa katika jengo lao ambalo unaweza kwenda ukafanya *shopping* kwa mujibu wa hali yako, lakini tutakuwa na jengo la *take away*, tutakuwa na jengo la *parking*, halafu tutakuwa na bustani.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo, tayari wataalamu wa Baraza la Manispaa na wataalamu wa mipango miji wameshakamilisha michoro na hivi karibu inatarajia kuwasilisha waraka Baraza la Mapinduzi ili serikali ituruhusu tuweze kulitangaza eneo lile kwa ajili ya kulifanyia kazi. Kwa hiyo, Mhe. Shadya aelewe kwamba hiyo ndiyo mipango ya serikali kupitia Baraza la Manispaa na lengo la kuendeleza lile eneo la Darajani. Ahsante sana.

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri, naomba tuendelee.

Kifungu 0802 Baraza la Manispaa - 1,200,000,000

Kifungu 0901

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, sina haja ya kutaka kuona buti hili, nina malengo maalum kwanza nilikuwa nataka nijiridhishe kwa hicho kizaazaa kilichonipata, maana yake nilikuwa kile kifungu nilichokusudia kukizuia sikukiona, kwa kizaazaa kilichonipata, lakini nikaona nimalizie hapa. Mhe. Waziri nakushukuru sana kwa kunijibu vizuri lile suala la KVZ, lakini ninachotaka kukwambia Mhe. Waziri, nataka nikwambie jana kwa jicho langu mwenyewe nimeona kitoweo walichopewa dagaa dogo na *juice* hata ile tungule hakuna, nimeona mwenyewe sikutaka ushahidi tosha.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hiyo Tume naomba sana hiyo *menu* yao waliyokusudia kwa jana wameteleza, maana yake ile jana ilikuwa *is too much*. Kwa hiyo, nakuomba sana ikazanie hiyo *menu* kwa kweli inasikitisha, mimi nataka niulize ile ni *juice* au mchuzi, nilishindwa kupata jibu, lakini nafikiri mtaalamu Mheshimiwa wangu Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi atanisaidia kunitafsiria kama ni *juice* au mchuzi. Kwa hiyo, rangi ilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, nakuomba sana na nakushukuru sana endelea na jitihada zako za ziara, naweka *Hansard* vizuri, sipigi fungu na fungu lako nimeliachia, naunga mkono asilimia mia kwa mia. Ahsante sana.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, kabla sijaeleza hii *concern* yangu hapa, naomba tu Baraza lielewe kwamba sayansi ya siasa inatamka rasmi kwamba hakuna adui wa kudumu, wala rafiki wa kudumu kwenye siasa. Kwa mnasaba huu, mimi nilikuwa sivipendi vikosi vile, lakini sasa nitavipenda na nitaendelea kuvipenda siku zote.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu ipo hapa juzi wakati nachangia kwa heshima kubwa sana na kwa masikitiko makubwa nilieleza kazi wanazozifanya hawa ndugu zetu wa vikosi na maslahi yao wanayoyapata kwamba ni duni mno. Pamoja na maslahi ambayo nimeyatetea juzi ni pamoja na mishahara pamoja na maposho mengine, ikiwemo kwamba hawa wanalinda sawa sawa na Jeshi la Polisi wakiwepo hapo kwenye doria wanakuwemo Jeshi la Polisi.

Mhe. Mwenyekiti, Jeshi la Polisi wanapokwenda doria usiku wanapewa kitu kinaitwa "mbu *allowance"*, lakini wenzetu hawa wa vikosi vyengine hawapewi. Ni lini namuuliza Mhe. Waziri hawa vijana wetu wapiganaji wa vikosi wanaolinda doria usiku na wao watapewa hiyo "mbu *allowance"* pamoja na "baridi *allowance"*. Hilo ni (a)

Mhe. Mwenyekiti, hawa vikosi walikuwa hawapati…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Saleh, hoja moja tuliyobakia usiseme (a) na (b) sema (a) umalize na umeshaisema (a) mbili ishasemwa na wenzeo.Kwa hiyo, subiri jibu ya hoja (a), kuhusu askari usiku wanapewa posho nao kama polisi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakubaliana naye kwamba katika siasa hakuna adui wa kudumu, wala rafiki wa kudumu, lakini mimi ndiye waziri na mimi ni ushahidi kwamba niliposimama pale nimewashukuru Waheshimiwa wote, lakini tatizo Mhe. Mjumbe wako hakuwepo ndani wakati natoa majibu yake, kwanza hilo akiri. Sasa sisemi shemegi yangu kwamba hanitendei haki, lakini hakuwemo humu ndani na nimelijibu vizuri suala hili. Nimemtizama sana kote sikumuona na kila aliyekuwepo mimi nilimuona.

Mhe. Mwenyekiti, kimsingi sisi hatuna *formula* hiyo, kama wanayo wenzetu wa Jeshi la Polisi, lakini tuna *ration allowance*, kwa baadhi ya vikosi tuna *risk allowance*, tuna *hard risk allowance*. Tunakiri baadhi ya *allowance* hatujaanza kuzitoa, ndiyo maana serikali kwa tangazo alilolitoa Mhe. Rais atahakikisha kwamba anazingatia maslahi ya wapiganaji.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nadhani niliwaomba Wajumbe tuishie hapo kwa sababu akishasema Mhe. Rais, maana yake sisi wengine kazi yetu ni kufuatilia. Tunawajali na haya wanayoyapata sasa Mhe. Saleh, hawakuwa nayo kama nilivyosema katika majibu yangu. Kwa hiyo, na mimi nawapenda na nawajali wapiganaji wote wa vikosi vyetu, kama tunavyowapenda ndani ya Baraza hili, sasa tusubiri tuone serikali itafanya nini katika kutengeneza hizo posho nyengine Mhe. Saleh. Nakuomba sana tustahamili.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, imepita hiyo na habari ya likizo vile vile nao wapewe kila mtu anataka likizo.

Kifungu 0901 Idara ya Uratibu wa Idara Maalum- 78,128,000

Kifungu 018

Mhe. Panya Ali Abdallah: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi nilipokuwa nikichangia nilichangia katika Tume hii ya Utumishi Idara Maalum ili kumshauri Mhe. Waziri, wakati haya yako chini ya ungalizi wake kuwa makini wakati wa kuajiri vijana ambao tayari wameshatumikia katika ujenzi wa Taifa pale na kuacha kuajiri wale wapya ambao hawajaajiriwa. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri anisaidie juu ya hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru Mhe. Panya mpiga kura wangu kwa maelezo ambayo ameyasema. Nataka nimuhakikishie kupitia Tume ya Utumishi ya Idara ya Maalum ya Vikosi vya SMZ katika kuajiri itazingatia sheria ya Tume ya Utumishi Idara Maalum, lakini pia, sheria ya utumishi wa umma ya mwaka 2011.

Mhe. Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kweli sikupata kumjibu, lakini katika hotuba yangu nilisema vijana ambao tunawachukua ndani ya JKU, tunawaandaa kuwafundisha kazi mbali mbali ili waweze kujiajiri wenyewe,

lakini halikadhalika tunawaandaa ili waweze kuajirika. Kwa hiyo, kwa zile nafasi za Idara Maalum kwa yule ambaye ameandaliwa na anaajirika, maana anaweza akawa amekwenda JKU, lakini akawa ana matatizo mengine ambayo kwa mujibu wa sifa za kijeshi akawa hana. Huyo hata kama amekwenda kwenye kambi za vijana, basi tutashindwa kuweza kumuajiri, lakini sifa si ya kwenda kwenye kikosi tu kujenga Taifa, lakini kuna na sifa nyengine za ziada. Kwa hiyo, tutazingatia sifa zote ambazo zinaelezwa kwa mujibu wa sheria ili tuweze kuwaajiri vijana wetu. Ahsante sana.

Mhe. Panya Ali Abdallah: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, mimi nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. Waziri, kwa sababu tunaelewa kama waziri msikivu, Mhe. Waziri, mfatiliaji na tuna matumaini makubwa ya mafanikio, *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atamsaidia atamuwezesha, lakini tu nimuombe kwa wale ambao watathibitika sifa za kuajiriwa kama serikalini hawana. Kwa hiyo, serikali iweze kuwazingatia kuwawezesha ili vijana hawa wasirudi vijiweni na waweze kujiajiri wenyewe. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo, tuendelee.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, ahsante, nilipokuwa nikichangia mbali ya kuzungumza kwa ujumla kuhusu masuala ya maslahi ya vikosi vya SMZ na niungane na Mhe. Waziri, kama hapa tulipofikia ni pazuri kwa sababu unapofika pahala vikosi vya ulinzi katika nchi vikawa vinathaminiwa na wote ndiyo kielelezo kikuu cha kufikia mafanikio ya kikosi hivi, ndivyo ilivyo dunia nzima.

Mhe. Mwenyekiti, mimi katika michango yangu nimezungumzia masuali mengi, lakini nilikuwa nataka maelezo juu ya suala moja *specifically* ambalo tumelizungumzia wengi humu ndani suala la miundo ya utumishi na ndiyo maana nimesimama hapa. Sababu hii ilikuwa amefikia mwisho kule na alipokuwa akijibu hakuwahi kutoa ufafanuzi wa kina.

Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia tumesema kwamba taarifa zilizokuwepo ni kwamba miundo, tunaambiwa imekamilika, lakini miaka mingi tunaambiwa hivyo hasa miaka iliyopita utekelezaji wake, nilikuwa nataka kujua kwamba umefikia wapi, kwa sababu vijana wengi wetu waliokuwa katika vikosi hivyo wanalalamikia hilo kwamba mfumo wao na taratibu zao, mishahara yao, upandishaji vyeo vyao, mambo ya *increment* saa nyengine yanakuwa hayako wazi kwao kiasi ambacho inaleta picha si nzuri, saa nyengine kama inaleta tofauti baina yao na wakuu wao kwa kuamini kwamba labda hawawatendei haki.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba Mhe. Waziri, atupe maelezo suala la miundo ya utumishi ambayo imeshapitishwa imefikia wapi utekelezaji wake. Ahsante

.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru tena Mhe. Ismail Jussa Ladhu, kwa suala ambalo ameliuliza, ni kweli kabisa miundo ya utumishi ya Idara Maalum kwa wapiganaji wetu iko tayari na kila mkuu wa kikosi ameshakabidhiwa muundo na kinachofanyika sasa nikuwapanga wapiganaji katika daraja zao kwa mujibu wa *Scheme of service*.

Mhe. Mwenyekiti, hii *Scheme of service* kwa wapiganaji ina maana sana hata yale malalamiko yaliyotokea hapa ya upandishwaji vyeo yatazingatia pia namna gani watumishi hawa hao wapinagaji hawa watakavyoweza kupanda daraja na kupata vyeo. Kwa hiyo, ni imani yangu kwamba moja kati ya jambo ambalo hivi sasa napita ku-*monitor* nani ameweza kufanya na nani hajaweza kufanya, ni pamoja na kuhakikisha kwamba vikosi vyote vinawapanga watumishi katika daraja zao kwa mujibu *Scheme of service* zao.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo Mhe. Ismail, namuomba asiwe na wasi wasi aendelee kunipa marando kwa maana muda niendelee kufuatilia ili nihakikishe kwamba askari wote tayari wameshakuwa *fitting* katika nafasi na daraja zao kwa kupitia ile miundo ya utumishi za wapiganaji. Ahsante sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu fasaha na mazuri ya Mhe. Waziri, sitaki nimnyanyue tena nimuombe tu kwamba kama alivyokumbuka mwenyewe kama mwaka jana nilisimama hapa nikaja na ushahidi wa malalamiko ya askari katika masuala ya upandishaji vyeo. Kwa hiyo, madhali alikumbuka nimuombe tu kwamba alisimamie vyema kwa uadilifu na kuhakikisha kwamba vijana wetu hawa wanatendewa haki.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia, akazungumza habari ya kuwapanga kwa dhamana na vyeo tofauti na nimuombe pia katika hilo hilo ahakikishe kwa sababu kumekuwa na malalamiko ya wengine unaweza ukapangwa dhamana, lakini mishahara ikawa haiendi vile na haya yako malalamiko hata katika kada nyengine huku kwa watumishi wa kawaida wa serikali mbali ya vikosi. Kwa hiyo, nilikuwa nimuombe tu kwamba ayazingatie yote hayo tuhakikishe kwamba hakuna malalamiko na nidhamu itapatikana na vikosi vyetu kuwa hakuna malalamiko au hakuna mtu kuhisi kwamba kuna upendeleo fulani. Kwa hiyo, nimuombe asimamie vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, na baada ya hapo, nasema tuendelee. Ahsante sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakushukuru sana kunipa nafasi hii nikajaribu kuzungumzia kuhusu Kamisheni ya Utumishi au Tume ya Utumishi ya Idara Maalum. Nadhani hata juzi nilipokuwa nikizungumza bajeti ya Mwalimu wangu Waziri wa Nchi (OR), Kazi na Utumishi wa Umma, nilizungumzia sana kwamba sijaridhika pamoja na Wajumbe wenzangu namna ya maslahi ya askari wetu wa Vikosi vya SMZ.

Mhe. Mwenyekiti, sisi kama Baraza la Wawakilishi madhumuni yetu hasa kwa hivi vikosi vyetu tulikuwa tunataka virudi katika ile hadhi ya aliyewajenga majeshi Marehemu Mzee Abeid Amani Karume, hata unapokwenda kuowa ukisema tu mimi jeshi, basi watu hawaulizi mara mbili, naamini Mhe. Waziri na yeye nia yake hiyo hiyo. Sasa mimi kwa ninavyojua Tume hii ya Utumishi ya Idara Maalum ilikwishakufanya kazi kubwa sana, ilikwenda ikarudi, imekwenda ikarudi, mpaka imefika pahala tunamshukuru Mwenyezi Mungu angalau ule muundo sasa hivi tayari umekubaliwa.

Mhe. Mwenyekiti, swahibu wangu kaondoka hapa Waziri wa Nchi (OR), Kazi na Utumishi wa Umma, lakini hili pia nilikuwa nataka nilizungumze na yeye alikuwa alisikie, kwamba Tume hizi zilitiwa mpaka kwenye Katiba kutokana na umuhimu na uzito wake. Narejea tena kauli ya Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria haki kuicheleweshe, basi ni sawasawa na haki kuikosesha. Tunaomba askari wetu tumeshawasemea sana tunashukuru, nidhamu wanayotupa, wewe mwenyewe unaona haya ile nidhamu wanayotupa, basi mwenyewe unaona haya kuipokea.

Mhe. Mwenyekiti, sasa na sisi tusifike pahala tukawaangusha, naomba pamoja na kwamba kuna utaratibu umewekwa hawa, wakati wameshakamilisha, maana mimi naamini miundo walipeleka pamoja na stahiki. Sasa kama hizi stahiki zilichelewa kidogo, hili naomba sana Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi, basi waliharakishe ili tuhakikishe kwamba kabla hatujaingia katika awamu nyengine, yaani tunakusudia bajeti hii tunayokwenda nayo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu kule katika kipindi cha bajeti ya Wizara ya Fedha katika Mfuko Mkuu wa Serikali tuliweka hakiba, kwamba kuna hii miundo itakayokuwa tayari imeweza kurekebishwa ndani ya kipindi hiki, basi tuweze kunyooka kule kidogo na tuweze kuzingatia haya maslahi, tusilazimishe lazima katika bajeti inayokuja. Ndio maana mimi nikawa napenda sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais tunapozungumza haya mambo yetu hapa Barazani Waziri wa Fedha awepo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu hawa mawaziri tunawatetea wao, lakini mkoba anao mtu mwengine na anakuwa hayupo. Naomba sana hili, Mhe. Waziri ameshalitolea ufafanuzi sana, lakini vile vile, nilikuwa namuomba sana na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, najua kila tunachokizungumza anaandika na anapokuja kusoma hotuba yake, naamini atarejea yale niliyoshauri, kwamba vikosi vyetu tuvirejeshee hadhi yake kama alivyokusudia Muasisi wetu wa Mapinduzi ya Zanzibar, Marehemu Mzee Amani Abeid Karume.

Mhe. Mwenyekiti, hata kama Mhe. Waziri hakunipa jawabu, naamini maneno yangu ameyasikia, lakini hata kuyatia baraka si vibaya. Nakushukuru.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Hamza Hassan Juma, tunazungumza lugha moja na yeye ni Mtumbatu wa juu, mimi ni Mtumbatu wa kisiwani. Kwa hiyo, yeye ananifahamu na mimi namfahamu. Serikali hii ina azma ya kuendelea kufuata nyayo za muasisi na Baba wa Taifa hili la Zanzibar, Marehemu Mzee Abeid Amani Karume katika kuvipa hadhi vikosi hivi vya SMZ na ndio maana tunakuja na maboresho mengi au marekebisho mengi yanayohusiana na maslahi ya vikosi vyetu.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nikubaliane na ushauri huo, lakini nataka na mimi aniamini juu ya yale niliyoyasema, akiona pahala ameingia mkuu wa nchi, hakuna mwengine tena ambaye anaweza akaweka *commitment* zaidi yake yeye na hili amesema. Sasa nadhani itoshe kwamba sisi tunavithamini, lakini mimi kama alivyo yeye na kama

nilivyosema nimekwenda kila pahala hakuna askari ambaye sikumsikiliza. Baada ya kujua uzito wa majukumu na matatizo waliyonayo, ndio maana tukaipeleka hoja hii serikalini na hatua zilizochukuliwa kwenye mwezi wa 10 wa mwaka uliopita zimetokana na hayo ambayo tumekwenda kuyaona mazingira ya vikosi vyetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, vikosi vyetu tutaendelea kuvipa hadhi mambo mengine sitaki niyasema hapa, lakini tutaendelea kuvipa hadhi na maslahi yao kama nilivyosema, tutaendelea kuyaimarisha kadiri serikali itakapoendelea kupata uwezo na hadhi ya Kikatiba bado ipo kwa Tume hii ya Idara Maalum, ndio maana sheria yao haikufutwa, kimefutwa kifungu tu kwenye sheria ile kwa maana ya kuzidisha kubaki na hadhi yake ile ile. Kwa hiyo, naomba aridhike na hilo na sisi serikali na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kama alivyosema amelisikia na mimi kama msimamizi wa jambo hili, basi nitaendelea kulisimamia vizuri.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru tuendelee.

Kifungu 1802 Tume ya Utumishi Idara Maalum-	68,500,000
Jumla ya Fungu-	**4,360,400,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 17 - JESHI LA KUJENGA UCHUMI

Kifungu 0201 Utawala Unguja-	9,482,600,000
Jumla ya Fungu-	**9,482,600,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 18 - CHUO CHA MAFUNZO

Kifungu 0201 Idara ya

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nimeona nisimame kabisa hapa ili tumalizane na Mhe. Waziri. Katika mchango wangu nimehoji katika hotuba yake ya maandishi Mhe. Waziri, ilikuwa na suala la ujenzi wa Chuo kipya cha Mafunzo katika eneo la Hanyegwa Mchana, lakini alipokuwa anasoma akatwambia sentensi ile tuifute. Sasa katika mchango wangu nilihoji kwamba maelezo kama hatukuyapata kwa nini mradi umefutwa? Sasa kama nilivyosema mradi ule umefikia pahala Mhe. Rais mwenyewe alikwenda kutembezwa akatoa kauli ya kuahidi kwamba aina mpya ya vyuo vya mafunzo tunavyovihitaji tumevipata. Nilikuwa naomba Mhe. Waziri ningeweza kusimama katika miradi ya maendeleo, lakini nimeona nisimame hapa tumalizane kabisa, atupe maelezo kwa nini mradi ule ambao umeshafika hatua ya kum-*commit* Mhe. Rais umefutwa ghafla.

Mhe Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru tena Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwa hoja hii. Ni kweli katika maelezo yangu ya kitabu cha mradi huu nimeamua niutoe kwenye mradi wa maendeleo wa mwaka huu wa bajeti, lakini umeondolewa, haina maana kwamba Gereza au Chuo cha Mafunzo cha Hanyegwa Mchana hakitojengwa na wala serikali haitofanya utaratibu wa kuweza kukijenga chuo hiki, kwani chuo hiki kikijengwa kitaondosha zile kasoro nyingi ambazo zipo katika vyuo vyetu vya mafunzo.

Mhe. Mwenyekiti, sababu iliyopelekea tuutoe kwenye bajeti ya serikali mradi huu unatarajia kwa gharama za sasa kutumia shilingi 21 bilioni pesa za Kitanzania, ukiangalia *Trend* ya bajeti ambayo ilikuwa inatengwa na serikali kwenye *developed* si zaidi ya shilingi milioni 300. Kwa hivyo, tunahisi kama ni kuchezacheza tu. Sasa serikali imeamua mradi huu uchukuliwe kama ni *component* nyengine itakayojumuishwa katika miradi ambayo tutaiombea ama mkopo au ufadhili katika maeneo mbali mbali duniani, kilichobakishwa kile cha shilingi 100 milioni kirudi katika *re-current* ili tuweze kuzitumia pesa zile kwa ajili ya kuendelea kulihifadhi lile eneo, lakini mradi huu kwa umuhimu wake kwa bajeti ile ya shilingi 300 milioni tusingeweza hata siku moja kuweza kuutekeleza.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka niwahakikishie Wajumbe wako wa Baraza hili tukufu kwamba mradu huu serikali umeuchukua kama ni *component* mbali ya kuweza kuutafutia *source* ili tuweze kupata hizi fedha na kuweza

kujenga na Gereza lile linajengwa tafauti na Magereza haya mengine ambayo tumeyazowea. Gereza lile nataka niwatanabahishie Wajumbe kwamba yale mahitaji yote ambayo yamependekezwa na taasisi za haki za binaadamu duniani zimo, yale ambayo Waheshimiwa Wajumbe tumeyapendekeza yamo na haya ni lazima tufanye hivi, kwa sababu kuna hadithi huwa anaitoa sana Mhe. Ali Mzee Ali, ya waziri mmoja wa fedha na waziri mwengine wa Tawala za Mikoa Afrika Magharibi.

Mhe. Mwenyeniti, kwa hiyo, na sisi lazima kwenye Gereza lile tujenge maeneo ya kukaa Waheshimiwa, wala tusilishangae hilo na kwa kuona umuhimu huo, lazima tutafute fedha za kujenga Gereza ambalo litakuwa na vigezo vyote, kuweka watoto, kuweka wanawake, kuweka wafungwa wengine wa makosa ya kihalifu na kuweka maeneo, siku nyengine tukiteleza na sisi twende.

Mhe. Mwenyeniti, kwa hiyo, kwa umuhimu huo Gereza hili linahitaji kupata fedha nyingi na sio shilingi 300 milioni, linahitaji kupata shilingi 21 bilioni na serikali inachokifanya ni kuhakikisha tunahangaika tunapata fedha hizi kupitia wahisani na mabenki kama kwa kukopeshwa, lakini tupate Gereza ambalo litakuwa na hadhi ya Kimataifa ili tusifanye kule Gerezani kama ni sehemu ya kwenda kuadhibu watu peke yake, lakini turejee ile kauli ya Muasisi wetu kwenda kuwafunza tabia njema wanaopelekwa kule.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mhe. Waziri kwa maelezo yake na kama alivyosema ni kweli wanaweza wakenda wowote, upande huu niliokuweko mimi, tuna uzoefu mkubwa sana wa kwenda sehemu kama hizo, *Inshaallah* maelezo yake yatasaidia upande mwengine, wajue kwamba kule hakuna mmoja anaweza kwenda mtu yeyote.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa naomba anisaidie kitu kimoja tu sasa, kwa maelezo yake ni kwamba fedha ambayo ilikuwa imetengwa na pengine ningesubiri huko, lakini nimesema nilimalize kabisa lisije likasemwa tena mara ya pili. Sasa nikitizama katika fedha za maendeleo za Chuo cha Mafunzo kumetengwa shilingi 200 milioni na katika vitabu ambavyo tunavyo hivi imo hiyo, iko katika ukurasa wa 251.

Mhe. Mwenyekiti, sasa labda angetwambia kwa sababu tukiacha baadae tukipitisha wizara hapa itakuwa tumepitisha na hizi, atwambie kwamba hizi shilingi 200 milioni ambazo zimeingizwa kule japo kuwa halijafika hilo suala nilimalize kabisa nikiondoka nimeondoka tu, kwamba hizi ambazo zipo katika ukurasa wa 251 wa kitabu hiki cha kwanza zitakwenda wapi ikiwa mradi huu kaamua kuuondoa. Kwa sababu yeye kataja shilingi 100 milioni, lakini hapa zimetajwa shilingi 200 milioni, hebu atuwekee sawa.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, fedha hizi ziko shilingi 100 milioni kuna masawazisho hapa yamefanyika, nitawaomba radhi Wajumbe zitabakia shilingi 100 milioni kwa ajili ya kuendeleza ukuta wa Chuo cha Mafunzo. Fedha hizi zimebakishwa katika wizara yetu, kuna taasisi ambazo zilikuwa na fedha kidogo zimepewa, lakini shilingi 100 milioni itabakia kwa ajili ya kuendeleza ule uzio wa kujihifadhi wakati serikali tunatafuta mambo mengine. Kwa hiyo, sahihi ni shilingi 100 milioni.

Kifungu 0201 Idara ya Vituo vya Mafunzo-	7,491,300,000
Jumla ya Fungu-	**7,491,300,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 29 - KIKOSI MAALUM CHA KUZUWIA MAGENDO

Kifungu 0201 Utawala-	11,766,800,000
Jumla ya Fungu-	**11,766,800,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 32 - KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI

Kifungu 0201 Utawala Unguja-	3,787,500,000
Jumla ya Fungu-	**3,787,500,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 34 - KIKOSI CHA VALANTIA

Kifungu 0201 Utawala Unguja-	4,660,400,000
Jumla ya Fungu-	**4,660,400,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 37 - MKOA WA MJINI MAGHARIBI

Kifungu 0401

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwa niko peke yangu katika hoja hii ya Mkoa wa Mjini. Kwa hivyo, hoja zangu mbili nitazitumia hapa hapa.

Mhe. Mwenyekiti, ninachokizungumza hapa kiko katika Mkoa wa Mjini ni soko la Darajani la wauza samaki na soko la mbogamboga.

Mhe. Mwenyekiti: Soko limezungumzwa kwenye Manispaa tumeshapita hiyo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, lipo katika Mkoa wa Mjini hili. Mkuu wa Mkoa tumeshuhudia akisimamia taasisi chungu nzima hapa.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, kila jambo lina utaratibu. Soko limezungumzwa kwenye Manispaa, ndio wanaohusika na limechangiwa na hoja zimetolewa. Sasa katika Mkuu wa Mkoa unaleta soko. Lete hoja nyengine kama unayo sio ya soko.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ninachokizungumza kipo katika Mkoa wa Mjini na hili soko lipo mjini na Mkuu wa Mkoa tumemwona akisimamia mambo chungu nzima hapa mjini. Imesemwa kuhusu barabara, kuendesha bandari zipo katika mkoa wake. Kwa hiyo, hoja yangu ni hapa hapa Mhe. Mwenyekiti, vyengine vyovyote utakuwa hujanifanyia haki.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, naendelea kusema kwa mara nyengine tena katika suala zima la Mkoa wa Mjini Magharibi. Kutokana na muda Ofisi yako siku hizi imetupunguzia muda kuna maeneo mengine sikupata kuyasema, lakini nilimpelekea Mhe. Waziri kwa maandishi. Kila siku tumekuwa tunapata ahadi ya Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi kujenga jengo lake jipya akahama pale alipo. Sasa hadithi hii kila siku inakuja. Sasa na safari hii, Serikali imefanya jambo zuri sana kutuletea hii programu *PBBB*, hii randama.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kwa kuwa randama hii inaeleza, Mkuu wa Mkoa wa Mjini atahama pale atajenga jengo lake. Utekelezaji wake kama haukuwezekana Mhe. Waziri tuje tumfanye nini hapa Barazani.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza Hassan Juma, lugha si nzuri.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa na Idara za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru Mhe. Hamza Hassan Juma, ni kweli sikupata muda. Nadhani utaratibu wa kawaida unajulikana Mhe. Waziri asipotekeleza kikaangoni, hapa tunauliza maswali. Sasa siwezi kuja na *commitment* nyengine zaidi ya utaratibu wa kawaida ambao upo kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na hoja ya Mhe. Waziri, lakini tatizo letu hapa tukimkaanga Waziri hatumkaangi Waziri, tutakuwa tunajikaanga wenyewe kwa mujibu wa Katiba. Sasa mimi nadhani kila tunachokisema hapa kina faida zake. Sasa mimi nadhani Mhe. Waziri ajitahidi kusimamia kwamba angalau mwaka huu, huu ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi tuuone.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu kama alivyosema yeye mwenyewe tumsubiri hapa. Hapa kama hatujabadilisha Katiba, hapa tutakuwa tunahoji, tunazuia, lakini baadae lazima inapitishwa. Sasa nafikiri kitu ambacho nilichokikusudia hapa kwamba sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi vitabu hivi tunakuwa tunavisoma mara kwa mara. Tulikuwa tunahitaji utekelezaji hasa katika ujenzi wa Ofisi ya Mkoa wa Mjini Magharibi, hayo ndio madhumuni yangu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, katika jambo nisilolipenda kusema nisitende. Kwa hiyo, naomba Mhe. Hamza Hassan Juma, aendelee kunipa imani kwamba hilo nitalisimamia kulifanya.

Kifungu 0401	Mipango na Sera-	663,115,400
Kifungu 0501	Wilaya ya Mjini-	543,394,200
Kifungu 0601	Wilaya ya Magharibi-	551,290,400
Jumla ya Fungu-		**1,757,800,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 38 Mkoa wa Kusini Unguja

Kifungu 0401	Mipango na Sera-	407,231,000
Kifungu 0501	Wilaya ya Kati Unguja-	490,131,000
Kifungu 0601	Wilaya ya Kusini Unguja-	439,238,000
Jumla ya Fungu-		**1,336,600,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 39 Mkoa wa Kaskazini Unguja

Kifungu 0401	Mipango na Sera-	392,757,000
Kifungu 0501	Wilaya ya Kaskazini 'A' -	430,543,000
Kifungu 0601	Wilaya ya Kaskazini 'A' -	421,625,000
Kifungu 0701	Wilaya Ndogo Tumbatu-	117,775,000
Jumla ya Fungu-		**1,362,700,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 40 Mkoa wa Kusini Pemba

Kifungu 0401	Mipango na Sera-	370,000,000
Kifungu 0403	Baraza la Mji Mkoani-	211,000,000

Kifungu 0501	Wilaya ya Chake Chake-	441,269,000
Kifungu 0601	Wilaya ya Mkoani-	426,298,000
Jumla ya Fungu-		**1,916,900,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 41 Mkoa wa Kaskazini Pemba

Kifungu 0401	Mipango na Sera-	439,268,000
Kifungu 0402	Baraza la Mji-	

Mhe. Farida Amour Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia fursa ya kupenya penya tu haikuwa ya uhakika. Naomba nishukuru na kumpongeza kwa dhati kabisa Mhe. Waziri, kwa ufafanuzi wake mzuri kuhusu Baraza la Mji wa Wete, lakini naomba nimwambie kitu kimoja.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu Mhe. Waziri alizungumzia kuhusu hawa wafanyabiashara, ndio walioshtakiwa, hawakushtakiwa Baraza la Mji wa Wete, lakini nataka nimwambie Baraza la Mji wa Wete bado ndio dhamana wa eneo lile la soko.

Mhe. Mwenyekiti, sasa katika hili Baraza la Mji wa Wete wana haki ya kuomba Mahakamani kupitiwa hukumu ile upya na kupeleka vielelezo vyao walivyonavyo ili kuwasaidia wafanyabiashara wale 16 walioambiwa wavunje tarehe 19 au watavunjiwa tarehe 20.

Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo kwa Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nataka nimshukuru Mhe. Farida Amour Mohammed kwa kutaka ufafanuzi wa ziada. Kama nilivyokwisha kusema kwamba hili jambo lipo Mahakamani na Mahakama kuna taratibu zake. Sisi kama nilivyosema tumefanya utafiti kupitia taratibu za kawaida za Kiserikali, tutashauriana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ili kuona na sisi tunapeleka malalamiko yetu Mahakamani. Kwa yale ambayo yamo ndani ya uwezo wetu ambayo na sisi tunahisi tumekoswa, yaani huyu alivyofanya amekosea, yale hatuna haja ya kwenda Mahakamani tutayachukulia hatua. Moja kati ya hilo ni lile la kuzungusha ule uzio.

Mhe. Mwenyekiti, lakini la pili, hili jengine tutawasiliana na vyombo husika ili tuone uwezekano wa kuweza na sisi kudai haki yetu mpaka tuweze kuipata. Kwa hiyo, Mhe. Farida, ningeomba tuvute subra, najua wafanyabiashara waliopo huku wana haki kwa sababu tuliwaruhusu sisi wenyewe na hatuna mtu mwengine anayeweza kuwakataza, lakini kwa sababu ya taratibu zile za Kimahakama na vielelezo vilivyokwenda na kwa sababu huyu alitumia mbinu ya kuwashtaki wafanyabiashara badala ya kutushtaki sisi, ndio maana kukapatikana hiyo *Loophole*. Kwa hiyo, nakuomba univumilie ili tuweze kulifuatilia hili jambo kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, ili tuweze kuirejesha haki hii kwenye chombo cha Baraza la Mji wa Wete.

Mhe. Farida Amour Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, mimi sitomvumilia Mhe. Waziri, kwa sababu pamoja na yote na hao tarehe 19 au 20 wakenda wakivunjiwa itakuwa masuala mengine. Sasa namuomba sana Mhe. Waziri, kwamba alitafakari kuanzia leo kabla ya hiyo tarehe 19 na 20, bila ya kubomolewa. Kwa sababu kwa taarifa waliyopewa wananchi wa pale wamesema kwamba vitabomolewa vile vibanda vyao na baadhi ya nyumba ambazo ziko pale kwenye hili Baraza la Mji la Wete.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi namuomba sana Mhe. Waziri, tunaweza tukasema tunavumilia huku, lakini huku kwengine tukaja tukatota. Sasa namuomba sana Mhe. Waziri, suala hili pamoja na kwamba sasa hivi tunapitisha bajeti hii, lakini alichukulie kwa hatua ya haraka sana ili wananchi wale wasije wakavunjiwa vile ambavyo kwa kweli ndio kula yao, ndio kula ya watoto wao, ndio kusomesha kwao. Namuomba sana Mhe. Waziri, tukimaliza hayo tuendelee, anijibu lakini.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mhe. Asha Bakari Makame kwa kushauriana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu tutalisimamia kwa karibu zaidi jambo hili ili kuona yule mwenye haki aweze kupata haki yake na yule aliyekuwa hana haki aweze kumpisha mwenye haki na kwa vielelezo ambavyo tumevikusanya nina hakika serikali tutarejesha eneo lenu. Ahsante sana.

Kifungu 0402	Baraza la Mji Wete	-	276,700,000
Kifungu 0501	Wilaya ya Wete-		448,245,000
Kifungu 0601	Wilaya ya Micheweni-		405,530,000
Kifungu 0701	Wilaya ya Kojani-		72,257,000
Jumla ya Fungu-			**1,642,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 43 Afisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho

Kifungu 0201 Utawala Unguja-

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nilipokuwa nikichangia katika kifungu hichi nilisema kuna wazee wanaotimiza umri wa miaka 65 mpaka 70, hawa walipiga kura mwaka 2000-2005, lakini kwa dharura zilizowatokezea tu kwa matatizo, kwa vile kule tayari mambo yamekwisha endelea wakakosa haki zao za kimsingi, lakini Mhe. Waziri, alipotoa maelezo hapa alisema kama watu hawa anataka kuwatambua ili wapate haki zao zile za kimsingi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kama Mwakilishi wa Jimbo la Kojani nipo tayari na jimbo langu watu hao kuwaorodhesha na kuwatambua, lakini baada ya kwisha kuwatambua nataka kujua unawafanyia nini kupata haki zao.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikijibu kama mnakumbuka Wajumbe nilirejea mara mbili Mhe. Hassan Hamad Omara, kwa kumfanya anisikilize mimi ninachokisema, lakini akawa yupo *busy* sana, sijui alibabaishwa na Mhe. Asha Bakari Makame au vipi, lakini nilichosema ni kwamba kwa wale wazee ambao hawajiwezi na hawawezi kufika katika maeneo hayo na wanayo haki, tushirikiane mimi na wao tukiuacha ule wasia alioufanya mwenzangu mwaka jana wa kwenda kutambua matatizo na akaweza kuyatafutia ufumbuzi. Kwa hiyo, na hili nitashirikiana nao ili kuyabaini maeneo na kama lipo na mtu amenyimwa haki kinyume na sheria aweze kupata haki yake, ndilo jibu ambalo nililisema na naendelea kulisema sasa hivi. Sasa mimi nadhani hilo ndio jibu la msingi. Ahsante.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kwamba nilikuwa nabadilisha mawazo kidogo na Mhe. Asha Bakari Makame, lakini nilikuwa namsikiliza kwa makini, ndio maana nilikuwa nasema pale Waziri nimemsikiliza vizuri, amesema watu waliozaliwa mwaka 1964 hao wanaelekea kuwa na umri mdogo, lakini niliotaja mimi ni umri mkubwa, amesema tuwatambue na baada ya kwisha kuwatambua, ndio tunataka ile haki kama itapatikana vipi. Mimi nipo tayari uniambie ni muda gani ili tushirikiane katika sehemu zetu mimi na wewe. Ni lini utanambia ili tufike hii sehemu kuwapata watu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Hassan Hamad Omar, mtu wa kisiwani na mimi mtu wa kisiwani, lakini nadhani lugha nyepesi niliyoisema kwamba mimi na yeye tutakwenda kuyatambua na kuyabaini hayo maeneo. Kwa hiyo, mimi nadhani tukubaliane kwamba tukimaliza shughuli tunachotakiwa kufanya sisi kama Mawaziri yale ambayo tumeshauriwa, yale ambayo tumeyakubali na kuyafanyia kazi. Kwa hiyo, mimi nadhani astahmili tu tumalize Baraza letu hili la bajeti kabla ya kwenda kwenye Bunge la Katiba tufanye hiyo kazi na hilo nililisema. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Sawa Mhe. Hassan Hamad Omar.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, kwa kauli ya Waziri hiyo, mimi nitamfuata, ni kawaida yangu nitamfuata simuachii. Nitafuatana naye na nitakwenda katika maeneo na naomba tuendelee.

Mhe.Mwenyekiti: Tunaendelea.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nilipochangia na mimi suala hili nilizungumza kama kuna wazee ambao wameshafika umri wa miaka 60, 70 na kuendelea mbele. Suala hili nilikuwa ninagombana sana na rafiki yangu Dkt. Mwinyihaji Makame alipokuwa yupo na bado suala hili halijapata ufumbuzi lipo. Nikawaambia kama hawa wazee ni wazee ambao kuwa umri wao, si watu wa kuhangaishwa hangaishwa sana na ni wazawa washazoea wameshajukuu wameshazaa, lakini sasa lazima wapate waende *Affidavity* na kuufuata huo *Affidavity* Mahakamani ni kazi kubwa. Kwa hivyo, nilitaka kama hawa wazee labda waonewe imani, Mhe. Waziri aseme hawa wazee tutawasaidia vipi, kwa sababu na wao wana haki katika nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, nilisema kama sheria tuliyopitisha kama mtu hana kitambulisho afungwe mwaka mmoja na nilithubutu kumwambia kwamba basi hawa wazee tuwakamate tuwafunge, kwa sababu hawana hivi vitambulisho na ni haki zao. Kwa hivyo, ninamuomba Mhe. Waziri, hebu anipe ufafanuzi kwa hawa wazee tunaweza kuwasaidia vipi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum SMZ: Mhe. Mwenyekiti, mimi sidhani kama suala lake linatofautiana na lile la Mhe. Hassan Hamad Omar. Nilishasema jibu ndio lile lile. Kwa hivyo, kama Mhe. Subeit na yeye yumo katika kundi hilo na wengine ambao kama Mhe. Rufai Said Rufai, wamesema hili, lakini nimewajibu kwa pamoja. Kama Mhe. Subeit, unataka lazima na wewe nikujibu maalum, jibu ni lile lile ambalo nimemjibu Mhe. Hassan Hamad Omar, tukimaliza *Inshaallah* tuungane twende tukaifanye hiyo kazi.(*Makofi*)

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, sina nia ya kucheleweshe wala sina nia ya kuwa nizuiwe, lakini alivyouliza Mhe. Hassan, aliuliza Mhe. Hassan kwa jimbo lake la Kojani. Angesema kama kila mmoja aliyekuwemo humu suala hili linamuhusu, tungekuwa tusisimame, lakini alikuwa anamjibu Mhe. Hassan. Kwa hivyo, kama ni kwa sote tuendelee. (*Makofi*)

Kifungu 0201 Utawala Unguja-	Shs.1,702,220,000.00
Kifungu 0301 Afisi Kuu Pemba-	Shs.237,180,000.00
Jumla ya Fungu-	**Shs.1,639,400,000.00**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 09 - OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA IDARA MAALUM

Kifungu 0901 Idara ya Uratibu ya Idara Maalum-

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, hapa nimesimama kwa mambo mawili; Moja ni marekebisho tu kwa sababu ya kuweka rekodi sawa. Ilitokea kosa kama hili imeandikwa hapa Idara ya Uratibu ya Idara Maalum, lakini ukisoma *component* yake ni uimarishaji wa Serikali za Mitaa ambayo haziwezi kuwa ni shughuli za Idara ya Uratibu wa Idara Maalum.Imeekwa hivyo katika hicho kifungu alichokisoma, lakini pia, imeekwa katika jumla ya kifungu. Kwa hivyo, nilikuwa ninafikiri kunahitajika marekebisho.

Mhe. Mwenyekiti, lakini la pili, hili nitaka naombe kiongozi wa shughuli za serikali anisaidie katika Baraza hili. Nimuomba Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, tumechangia wengi na Mhe. Hamza Hassan Juma na mimi kuhusu miradi mbali mbali, lakini *specifical* ni mradi wa *ZUSP* kwamba unasimamiwa na wizara hii, lakini fungu lake unaweza kulipata katika Wizara ya Fedha na ukitazama katika kitabu hichi cha *volume one* cha kwanza ukifungua ukurasa 252 unaukuta mradi wa *ZUSP*.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hili mimi nilikuwa naomba nipate kauli ya serikali. Hivyo, naomba kiongozi wa shughuli za serikali aniambie kwamba, kwa nini miradi hii ya kisekta ambayo ina idara zake za kisekta? Kwa nini yote mafungu yake ya fedha tusiyapate katika mafungu ya maendeleo ya wizara zile hapo, ndio tunapata kuwasimamia, yote yahamishiwe katika Wizara ya Fedha ambayo inaleta ugumu wa uwajibikaji na hata katika kuhoji kwetu sisi, kwa sababu yote yamekusanywa pamoja hata kuhoji unakuja kupata nafasi moja huwezi kuhoji.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, naomba kiongozi wa shughuli za serikali aweze kunisaidia, kwa nini utaratibu huu tukubali uendelee. Mafungu ya maendeleo yasikae katika wizara zake za kisekta, yakaachiwa katika Wizara ya Fedha yote kwa pamoja, kwa nini kukafanya hivyo?

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru ndugu yangu Mhe. Ismail Jussa Ladhu na niwashukuru Wajumbe wote kwa namna ambavyo tumeshirikiana vizuri tokea asubuhi katika kupitisha bajeti hii ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum.

Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwamba tuuchukue huu ushauri anaouzungumzia Mhe. Jussa ili ukafanyiwe kazi na serikali. Kwa kuwa jambo hili limeshaanza kitambo na miradi inaendelea. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Jussa atupe muda tushauriane, tukae pamoja kati ya Wizara ya Fedha na wizara nyengine zinazohusika zenye miradi ya namna hiyo ili tuone njia gani muafaka ambayo iweze kutekelezeka kwa nia na madhumuni yale yale ya usimamizi mzuri wa matumizi ya fedha za serikali na uwajibikaji ulio sahihi, ili miradi hii ya maendeleo ifanye wajibu uliokusudiwa kwa wakati na kwa ufasaha zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, namuomba Mhe. Ismail Jussa Ladhu atupe nafasi jambo hili tulishughulikie kwa sababu kulitolea majibu ya haraka haraka hapa, inawezekana tukenda kinyume na mambo ambayo kiutaalamu pengine yatahitaji yaendelee kama yalivyopangwa kwa sasa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, nimuombe sana aturuhusu, lakini ninamuhakikishia tu baadae leo leo tutakutana tuone tatizo lipo wapi na namna gani ya uwajibikaji na baadae tutampa taarifa nzuri Mhe. Ismail Jussa Ladhu.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Ismaili Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza niseme jambo moja. Kama Wajumbe tuna haki tunapotaka kauli nzito ya juu kwa kiongozi wa serikali kuweza kupewa na ndio utaratibu wa kawaida katika Mabunge yote. Kwa hivyo, mara nyengine ina uzito wake kupata kauli kama hizo, lakini la pili, niseme sio tatizo kuhusu tuendelee kwa sababu sio nia yangu kukwamisha, lakini naomba serikali ichukue kama alivyosema Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwamba wanakwenda kulikalia na ndio tupate jawabu katika kikao hichi.

Mhe. Mwenyekiti, isije ikawa kama alivyosema Mhe. Haroun Ali Suleiman mara nyingi kulikalia wenyewe ikawa umelikalia halinyanyuki tena hilo. Ninasema hivi kwa sababu hayajesha Wizara ya Fedha, bado haijaja hapa na nina hofia kwa sababu yaliyotukwaza Wajumbe wengi humu ni kukwamisha bajeti kuu ya serikali kwa sababu ina matatizo ya Kikatiba, lakini kukwamisha bajeti ya wizara hatujazuiliwa humu.

Mhe. Mwenyekiti, sasa ninahofia tusije tukafika pahala tukaja tukakwamisha bajeti ya Wizara ya Fedha kwa sababu haturidhiki na haya tutakuja kuona katika kila wizara itakayokuja. Wizara nyingi zimekwamisha miradi yake ya maendeleo kwa sababu ya Wizara ya Fedha kuwa waroho kujikumbatia wao peke yao miradi yote ya miradi. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, ninasema ninakubali tuendelee, lakini Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais ajue kwamba patakuja kuwa na kirandanda humu ndani katika Wizara ya Fedha, kwa sababu hatuwezi kukubali kwamba yote mafungu yote ya fedha na unaona ikiwa miradi midogo midogo tu hapa utaona Mradi wa Serikali za Mitaa umeachiwa wizara hii kwa sababu pana milioni mia mbili.

Mhe. Mwenyekiti, lakini miradi yote mikubwa yenye fedha nzito wamekumbatia wenyewe wakubwa na niliwahi kusema juzi hapa kama tunahisi wizara nyengine hazina kazi Wizara ya Fedha moja, basi ibakishwe peke yake, wafanye kazi zote wao, tujue tunakuja kupitisha bajeti moja.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, ninakubali, lakini kwa sharti kwamba ikifika Wizara ya Fedha, tuje tupate kauli hatuwezi kukubali tena kwamba tutashindwa kusimamia kiuwajibikaji, wizara zinazohusika kwa sababu mafungu yote ya maendeleo wameyachukua katika Wizara ya Fedha na ikifika Wizara ya Fedha wanakwambia hili lipo katika wizara inayohusika, hatuwezi kukubali tena.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, ninasema ninakubali kauli yake Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa sharti kwamba leo hili anakwenda kukaa nalo hili walipatie ufumbuzi waje watujibu humu ndani ikifika wakati wake.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana, tunaendelea.

Kifungu 0901 Idara ya Uratibu wa Idara Maalum-	Shs.200,000,000.00
Jumla ya Fungu-	**Shs.200,000,000.00**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 17 - JESHI LA KUJENGA UCHUMI

Kifungu 0201 Utawala Unguja-	Shs.150,000,000.00
Jumla ya Fungu-	**Shs.150,000,000.00**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 18 - CHUO CHA MAFUNZO

Kifungu 0201 Idara ya Vituo vya Mafunzo-	Shs.200,000,000.00
Jumla ya Fungu-	**Shs.200,000,000.00**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum SMZ: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli hapa tumefanya marekebisho na zimebaki milioni mia moja, lakini vile vile, kwenye kile kifungu ambacho alisimama Mhe. Ismail Jussa Ladhu, tulikwishakufanya masawazisho, lakini ninakiri kwamba karatasi hiyo haijafika, lakini iwepo kwenye *Hansard* kwamba zile milioni mia mbili ni Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na sio Idara Maalum.

FUNGU 18 - CHUO CHA MAFUNZO

Kifungu 0201 Idara ya Vituo vya Mafunzo-	Shs.100,000,000.00
Jumla ya Fungu-	**Shs.100,000,000.00**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 29 - KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO

Kifungu 0201 Utawala-	Shs.500,000,000.00
Jumla ya Fungu-	**Shs.500,000,000.00**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza linarudia)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum SMZ: Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha ya wizara yangu pamoja na marekebisho yake, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza hili liyakubali makisio hayo. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Kazi na Utumishi wa Umma: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja ilikubaliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijaahirisha naomba nitoe tangazo kwamba munaarifiwa wale walioalikwa chakula Ikulu gari zipo nje hapo mukitoka zitawapeleka. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya hayo, tunaahirisha kikao hadi kesho asubuhi saa tatu. (*Makofi*)

(Saa 8.14 mchana Baraza liliahirishsa hadi tarehe 04/06/2014 saa 3.00 asubuhi)